# Walimu wa Kanisa



*Walimu wa Kanisa* wa kwanza kutangazwa walivyochorwa na Pier Francesco Sacchi mwaka 1516 hivi. Kuanzia kushoto mbele ni Augustino, Gregori I, Jeromu na Ambrosi.

**Mwalimu wa Kanisa** ni jina la heshima ambalo kwa nadra Kanisa Katoliki linampa mtakatifu ambaye katika maisha, mafundisho na maandishi yake alionyesha na kueneza mwanga wa pekee katika masuala ya imani, maadili na maisha ya kiroho.

"Tamko la kwamba mtakatifu fulani ni mwalimu wa Kanisa lote linategemea utambuzi wa karama maalumu ya hekima ambayo alijaliwa na Roho Mtakatifu kwa faida ya Kanisa ikabainishwa na athari njema ya mafundisho yake katika Taifa la Mungu" (Papa Benedikto XVI, Barua ya Kitume ya tarehe 7 Oktoba 2012).

Mpaka sasa, katika miaka karibu 2000 ya historia ya Kanisa wanaume 31 na wanawake 4 tu wamepewa heshima hiyo.

Wa kwanza kutangazwa (mwaka 1298) ni mababu wa Kanisa wanne muhimu zaidi upande wa Magharibi:

- Gregori I (540 hivi - 604) - 1298 *
- Ambrosi wa Milano (340 hivi - 397) - 1298 *
- Augustino wa Hippo, *Doctor Gratiae* (354 - 430) - 1298 *
- Jeromu (347 - 420) - 1298 *

Mwaka 1568 walitangazwa mababu wa Kanisa wanne muhimu zaidi upande wa Mashariki, pamoja na Thoma wa Akwino, mwalimu bora wa Karne za Kati upande wa Magharibi.

- Yohane Krisostomo (347 hivi - 407) - 1568 *
- Basili (329 hivi- 379) - 1568 *
- Gregori wa Nazianzo (329 - 390 hivi) - 1568 *
- Atanasi wa Aleksandria (295 hivi - 373) - 1568 *
- Thoma wa Akwino, *Doctor Angelicus* au *Doctor Communis* (1225 hivi - 1274) - 1568

Baadaye waliendelea kutangazwa kama ifuatavyo:

- Bonaventura wa Bagnoregio, *Doctor Seraphicus* (1217 hivi - 1274) - 1588

- Anselm wa Canterbury, *Doctor Magnificus* (1033 hivi - 1109) - 1720
- Isidori wa Sevilia (560 - 636) - 1722 *
- Petro Krisologo (580 hivi - 450 hivi) - 1729 *
- Leo I (400 hivi - 461) - 1754 *
- Petro Damiani (1007 - 1072) - 1828
- Bernardo wa Clairvaux, *Doctor Mellifluus* - (1090 - 1153) - 1830
- Hilari wa Poitiers (315 hivi - 367) - 1851 *
- Alfonso Maria wa Liguori, *Doctor Zelantissimus* (1696 - 1787) - 1871
- Fransisko wa Sales (1567 - 1622) - *Doctor Caritatis* 1877
- Sirili wa Aleksandria, *Doctor Incarnationis* (370 hivi - 444) - 1883 *
- Sirili wa Yerusalemu (315 - 386 hivi) - 1883 *
- Yohane wa Damasko (676 hivi - 749 hivi) - 1883 *
- Beda (672 hivi - 735) - 1899 *
- Efrem Mshamu (306 hivi - 373) - 1920 *
- Petro Kanisi (1521 - 1597) - 1925
- Yohane wa Msalaba, *Doctor Mysticus* (1542 - 1591) - 1926
- Roberto Bellarmino (1542 - 1621) - 1931
- Alberto, *Doctor Universalis* (1205 hivi - 1280) - 1931
- Antoni wa Padua, *Doctor Evangelicus* (1195 - 1231) - 1946
- Laurenti wa Brindisi, *Doctor Apostolicus* (1559 – 1619) - 1959
- Teresa wa Yesu (1515 - 1582) - 1970
- Katerina wa Siena (1347 - 1380) - 1970
- Teresa wa Mtoto Yesu, *Doctrix Amoris* (1873 - 1897) – 1997
- Hildegarda wa Bingen (1098 hivi - 1179) - 2012
- Yohane wa Avila (1500 hivi- 1569) - 2012

Mwaka wa kutangazwa ukifuatwa na nyota unaonyesha watakatifu wanaoheshimiwa na Waorthodoksi pia, ingawa kwao hakuna cheo cha mwalimu wa Kanisa.

Tofauti na orodha hiyo, hapa chini tutawapitia mmojammoja kufuatana na historia ya Kanisa, kuanzia mababu wake wa karne IV hadi mwalimu wa mwisho aliyefariki mwaka 1897 tu.

**Kwa Kiswahili**



Masomo ya Breviari - ed. Ndanda Mission Press - Ndanda 1978

Maisha ya Watakatifu – ed. T.M.P. Book Department – Tabora 1989

MAURICE SOSELEJE – Kalendari Yetu Maisha ya Watakatifu – Toleo la Pili – ed. Benedictine Publications Ndanda-Peramiho – Ndanda 1986 - ISBN 9976-63-112-X


# MABABU WA KANISA

## Atanasi (295 hivi - 373)



Atanasi wa Aleksandria anayeitwa *Mkuu* alikuwa Patriarki wa Kanisa Katoliki la madhehebu ya Misri kati ya mitaguso mikuu miwili ya kwanza.

Maisha yake yote yalihusika na juhudi kubwa za kufafanua imani sahihi juu ya umungu wa Yesu Kristo na juu ya Utatu: ndiye aliyeitetea kuliko wote, hata akaitwa mapema "nguzo ya Kanisa" (Gregori wa Nazianzo).

Alipozaliwa (mwaka 295 hivi) dhuluma za Dola la Roma dhidi ya Wakristo zilikuwa zikielekea kilele na kikomo chake.

Alizaliwa na kukulia katika jiji la Aleksandria, ambalo wakati huo lilikuwa likiongoza kimataifa kwa ustaarabu na elimu. Wakristo wa huko walikuwa na chuo muhimu cha katekesi, lakini kulikuwa pia na maelekeo ya hatari, hasa wafuasi wengi wa Gnosi, mbali na wale wa dini za jadi zilizoabudu miungu mingi.

Alipata elimu na malezi mazuri na tangu ujanani alihusiana na wamonaki wa jangwa la Tebais, halafu uzeeni (356-362) aliishi monasterini.

Mwaka 319 askofu Aleksanda wa Aleksandria alimpa daraja ya ushemasi na kumfanya katibu wake.

Akiwa bado shemasi, mwaka 325 alimsindikiza na kumsaidìa kwenye Mtaguso I wa Nisea ulioitishwa na Kaisari Konstantino Mkuu hasa kwa lengo la kujadili mafundisho ya padri wa Aleksandria, jina lake Ario, kuhusu dhati ya Yesu Kristo. Huyo alisema Neno wa Mungu si Mwanae halisi, bali kiumbe tu, ingawa cha Kimungu kwa namna fulani. Hivyo alikataa pia uwezekano wa binadamu kushiriki umungu kwa njia ya Kristo.

Dhidi ya Ario, aliyefuatwa mapema na watawala na maaskofu wengi, huo Mtaguso mkuu wa kwanza ulitunga kanuni ya imani ambamo ulitumia neno la Kigiriki ‛ομοούσιος (*homoousios*, yaani "wa dhati ileile" ya Baba), ili kukiri kwa namna wazi usawa kamili wa Mungu Baba na Mwana aliyezaliwa naye bila kuumbwa.

Atanasi akishikilia msimamo huo moja kwa moja, pengine kwa ukali, dhidi ya waliokataa ungamo hilo na kupinga uteuzi wake, akijivutia chuki ya Waario wa aina zote na dhuluma ya serikali iliyodai maelewano ili umoja wa dola usivunjike.

Mara baada ya kushika nafasi ya marehemu askofu Aleksanda mwaka 328 (alipokuwa na umri wa miaka 30 tu), Atanasi alionyesha hatakubali maelewano tofauti na imani iliyoungamwa na umati wa maaskofu huko Nisea. Ushindani wake na serikali ulifikia kilele alipokataa agizo la Konstantino la kumrudisha Ario kwenye ushirika.

Atanasi alipaswa kustahimili dhuluma za serikali, hata akafukuzwa katika jimbo lake walau mara tano na kupelekwa uhamishoni tangu miaka michache baada ya kuchaguliwa Patriarki wa Aleksandria na wa Misri yote hadi mwaka 366, ambapo Kaisari alilazimishwa na umati amrudishe Aleksandria. Katika miaka 30, kwa jumla aliishi miaka 17 uhamishoni akiteseka kwa ajili ya imani.

Kumbe, akiwa mbali na Aleksandria, alitetea na kueneza hata Trier (Ujerumani) na Roma (Italia) imani ya Nisea pamoja na umonaki. Baada ya kurudishwa Aleksandria, aliendelea kuleta upatanisho ndani ya Kanisa na kulipanga upya.

Katika mapambano yake aliungwa mkono na Sinodi ya Roma ya mwaka 341 na ile ya Sardica ya mwaka 343.

Ingawa alipatwa na vurugu nyingi maishani, Atanasi aliandika sana: hotuba, barua, lakini pia vitabu juu ya imani, historia, ufafanuzi wa Biblia, pamoja na maisha ya Kiroho. Kitabu chake maarufu kimojawapo kinahusu umwilisho wa Neno; humo aliandika kuwa Neno wa Mungu "alifanyika mtu ili sisi tuweze kufanywa Mungu".

Lakini kitabu chake kilichosambaa zaidi na kuathiri zaidi Kanisa labda ni "Maisha ya Antoni" ambacho kilieneza umonaki haraka mashariki na vilevile magharibi.

Atanasi hakuwa mtu wa nadharia tu, bali hasa mchungaji aliyeona mapema hatari iliyofichika katika uzushi wa Ario, yaani kurudia Upagani wa Kigiriki. Hamu yake ilikuwa kulinda kikamilifu "mapokeo, mafundisho na imani ya Kanisa Katoliki ambayo Bwana aliitoa, Mitume waliihubiri na mababu waliitunza".

Hivyo alitetea uwepo wa Utatu "kikwelikweli" na kusisitiza kwamba Neno hakuumbwa bali alizaliwa na kuwa na umungu uleule wa Baba. Mwana ana utimilifu wa umungu na ni Mungu kamili. Baba na Mwana wana hali ileile ya milele. Hiyo ni muhimu kuhusu ukombozi, kwa sababu tusingeweza kuokolewa bila Mungu mwenyewe kujifanya mtu. Ndiyo sababu Bikira Maria anaweza kuitwa Mama wa Mungu. Roho Mtakatifu hawezi kuwa kiumbe ndani ya Utatu, bali ni Mungu yuleyule.

Kwa mafundisho yake na kwa upendo wake motomoto kwa Kristo, tangu zamani anaheshimiwa na Wakatoliki, Waorthodoksi na Waorthodoksi wa Mashariki kama mtakatifu na mmojawapo kati ya mababu wa Kanisa walio muhimu zaidi. Anakumbukwa pia katika kalenda za Waanglikana na Walutheri.

Mwaka 1568 Papa Pius V alimuongezea sifa ya mwalimu wa Kanisa.

Wote wanaadhimisha sikukuu yake kila mwaka tarehe 2 Mei, tarehe ya kifo chake mwaka 373.

## Efrem (306 hivi - 373)



Efrem wa Siria alikuwa mtawa na shemasi, mwanateolojia na mwanashairi pamoja, maarufu hasa kwa tenzi zake nyingi ajabu ambazo alizitunga kwa lugha ya Kiaramu na ambazo zinatumika hadi leo katika liturujia na kutokeza imani kwa namna bora.

Ndiye mwakilishi muhimu zaidi wa Ukristo wa Kisiria.

Alizaliwa Nisibi, leo Nusaybin, Uturuki Kusini Mashariki, mipakani kwa Siria, mwaka 306 hivi katika familia ya Kikristo, akabatizwa alipokuwa na umri wa miaka 18. Hakuoa, ingawa hakuna hakika kama mtindo wake wa maisha unaweza ukaitwa umonaki.

Kisha kulelewa na Yakobo, askofu wa Nisibi (303-338), alianzisha naye chuo cha teolojia katika mji huo.

Kwa muda mrefu na bidii nyingi alifanya kazi ya ushemasi, akihubiri na kufundisha teolojia na maisha ya Kiroho kwa wamonaki na walei wa Nisibi hadi mwaka 363, ambapo Wakristo walifukuzwa na Waajemi kutoka mji huo.

Hapo naye pia akahamia Edesa, leo Urfa, Uturuki, alikoendelea kuhubiri hadi alipofariki tarehe 9 Juni 373 kutokana na maradhi aliyoambukizwa wakati wa kuwahudumia wagonjwa.

Alitetea imani sahihi dhidi ya uzushi wa mazingira yake (Uorigene, Uario na Gnosi) na kufanya umisionari kati ya wasio Wakristo.

Maandishi yake yanatokeza kuliko mengine yote Ukristo ulivyo kadiri ya mapokeo ya Kisemiti, yaliyo jirani na asili yake ya Kiyahudi kuliko yale ya Kigiriki na ya Kilatini yaliyotokea katika Dola la Roma. Pamoja na hayo, Efrem aliwahi kutengeneza mazingira na kwa namna fulani hata misamiati ya mafundisho rasmi juu ya Kristo yatakayokuja kutolewa na mitaguso mikuu ya karne V.

Mbali na vitabu vyake vya kupinga uzushi na vya kufafanua Biblia, vingine vyote vinafuata ushairi, na hata hotuba zake zilikuwa na mtindo huo. Ni kati ya watu waliotunga mashairi mengi zaidi katika historia ya fasihi. Inakadiriwa aliandika mistari milioni tatu kwa heshima ya Bikira Maria tu katika miaka 360-370. Ni kati ya waenezaji wakuu wa heshima hiyo, akisisitiza kwamba, kama vile hakuna ukombozi bila Yesu, vilevile hakuna umwilisho wake bila Maria. Fumbo hilo lilizidisha hadhi ya wanawake, ambao Efrem anawazungumzia daima kwa heshima ya dhati.

Ili kuelewa mafundisho yake, ni lazima kuzingatia daima kwamba alifanya teolojia kwa ushairi: huo ulimwezesha kuchimba mafumbo kwa njia ya mifano inayopingana ili kusisitiza maajabu yaliyofanywa na Mungu.

Kwa mfano, katika utenzi kuhusu Kuzaliwa kwa Kristo aliandika: "Bwana alimuingia Maria akawa mtumishi; Neno alimuingia akawa mkimya ndani ya Maria; ngurumo ilimuingia na sauti yake ikawa tulivu; Mchungaji

alimuingia akawa Mwanakondoo ndani ya Maria akatoka akilia. Wewe uliyepanga yote, tumbo la Mama yako liligeuza utaratibu wa mambo. Yeye alimuingia tajiri, akatoka fukara: Aliye Juu alimuingia akatoka duni. Aliye uangavu alimuingia na kuvaa, akatoka ana sura nyonge… Yeye anayelisha wote aliingia akasikia njaa. Yeye anayenywesha wote aliingia akasikia kiu. Yeye anayepamba vyote alimtoka Maria akiwa uchi na tupu".

Teolojia yake inakuwa liturujia, muziki: kweli alikuwa mtunzi mahiri akiunganisha kutafakari juu ya imani na kuimba sifa za Mungu. Ni katika hali hiyo kwamba ukweli unang'aa katika mafundisho yake kwa watu yaliyo rahisi kukaririwa na kuimbwa. Ndiyo mbinu ya kufana aliyotumia katika sikukuu ili kueneza imani ya Kanisa.

Ni mwanateolojia ambaye, juu ya msingi wa Biblia, anafikiri kishairi fumbo la ukombozi wa wanadamu ulioletwa na Kristo, Neno wa Mungu aliyefanyika mtu.

Efrem alitumia pia mifano mingi ya viumbe mbalimbali, kwa kuwa kwake vyote vinashikamana, na ulimwengu ulioumbwa na Mungu ni kitabu cha kusomwa pamoja na Biblia.

Kwa ubora wa mashairi yake kuhusu imani kwa jumla ameitwa "kinubi cha Roho Mtakatifu".

Tangu zamani anaheshimiwa na Wakatoliki, Waorthodoksi na Waorthodoksi wa Mashariki kama mtakatifu na babu wa Kanisa.

Papa Benedikto XV tarehe 5 Oktoba 1920 alimuongezea sifa ya mwalimu wa Kanisa.

Sikukuu yake inaadhimishwa kila mwaka tarehe 9 Juni, siku ya kifo chake kilichotokea Edesa mwaka 373.

## Hilari (315 hivi - 367)



Hilari wa Poitiers alikuwa askofu wa mji huo (nchini Galia, leo Ufaransa), mwanateolojia, mwanafalsafa na mwandishi.

Alichangia teolojia, k. mf. kuhusu Ufunuo, akiunganisha mitazamo ya Ukristo wa mashariki na ya ule wa magharibi.

Alizaliwa mwaka 315 hivi katika familia ya kisharifu, lakini si ya Kikristo.

Maandishi yake yanaonyesha alipata elimu nzuri kuhusu fasihi, akavutiwa mapema na falsafa na kutafuta ukweli. Akitafakari hatima ya binadamu na kusoma Biblia, hatimaye aliongokea Ukristo akabatizwa mwaka 345 hivi.

Alikuwa baba wa nyumbani alipochaguliwa askofu wa Poitiers mwaka 353.

Mwaka 354 tu alikuja kujua Kanuni ya Imani ya Nisea, akaanza kuitetea katika sinodi na mitaguso dhidi ya uzushi wa Ario.

Kwa ajili hiyo mwaka 356, kwa ombi la maaskofu Waario, alipelekwa na Kaisari Kostanzo II uhamishoni Frigia (leo katika Uturuki).

Akiishi huko miaka mitano iliyofuata alipata nafasi ya kuchimba mafundisho ya mababu wa Kanisa la Mashariki, hata akaanza kuandika kitabu cha Kilatini juu ya Utatu (*De Trinitate*).

Humo anasimulia safari yake kuelekea imani ambayo aliiungama katika ubatizo akiwa tayari kuishika daima na hata kuifia. Hilari anajenga teolojia yake juu ya maneno ya kubatizia yaliyoagizwa na Yesu, akisisitiza ukweli wa majina "Baba" na "Mwana" yanayomaanisha kuwa dhati yao ni moja.

Anajitahidi kuonyesha sehemu mbalimbali za Agano la Kale ambazo pia zinadokeza umungu wa Mwana na usawa wake na Baba. Kuhusu sehemu za Agano Jipya zinazoweza kuleta utata, anafundisha kutofautisha zile zinazosema juu ya Yesu kama Mungu na zile zinazosema juu yake kama mtu.

Aliandika: "Mungu hajui kuwa chochote ila upendo, hajui kuwa yeyote ila Baba. Wenye upendo hawana kijicho, na yule ambaye ni Baba ni hivyo kikamilifu". Kwa sababu hiyo Mwana ni Mungu kweli pasipo upungufu wowote. "Yule anayetokana na aliye mkamilifu ni mkamilifu vilevile kwa sababu yeye ana yote, ametoa yote".

Binadamu wanapata wokovu kwa Kristo tu, Mwana wa Mungu na Mwana wa Adamu, ambaye kwa kujifanya mtu ameunganika na watu wote. "Kwa kuhusiana na mwili wake, wote wanaweza kumfikia Kristo, mradi wavue nafsi yao ya awali kwa kuipigilia msalabani; mradi tunaachana na maisha yetu ya kwanza na kuongoka ili tuzikwe pamoja naye katika ubatizo wake tukitarajia uzima".

Huko uhamishoni aliandika pia "Kitabu cha Sinodi" ambamo kwa faida ya maaskofu wenzake wa Galia, alikusanya na kufafanua maungamo ya imani na hati nyingine za sinodi za mashariki za wakati ule.

Kabla na baada ya vitabu hivyo, aliandika ufafanuzi wa Zaburi na sehemu nyingine za Biblia, kuanzia Injili ya Mathayo, mbali ya tenzi za dini na vitabu vya historia. Kati ya maandishi yake yote, mengi yametufikia.

Kuhusu Zaburi, alizifafanua kwa mtazamo huu: "Bila shaka mambo yote yanayosemwa katika Zaburi yanatakiwa kueleweka kadiri ya tangazo la Injili, hivi kwamba, haidhuru roho ya unabii imesema kwa sauti gani, yote yaweze kuhusianishwa na ujuzi wa ujio wa Bwana wetu Yesu Kristo, wa umwilisho, mateso na ufalme, na uwezo na utukufu wa ufufuko wake". Hivyo katika Zaburi zote aliona fumbo la Kristo na la mwili wake, yaani Kanisa.

Aliporuhusiwa kurudi kwao aliwajibika tena katika uchungaji wa jimbo lake, lakini aliathiri Kanisa hata nje ya mipaka hasa kwa mafundisho yake; hivyo alikuwa mhusika mkuu wa Mtaguso wa Paris (361) uliotumia misamiati ya Mtaguso I wa Nisea, na kwa kutumia nguvu na busara pamoja, alifaulu kurudisha Waario wengi katika Kanisa pamoja na kueneza Ukristo.

Kutokana na juhudi zake aliitwa "Atanasi wa magharibi".

Kati ya wanafunzi wake muhimu zaidi, yupo Mt. Martin wa Tours, aliyeanzisha monasteri karibu na Poitiers halafu akawa askofu mmonaki wa kwanza katika Kanisa la Magharibi.

Alifariki mwaka 367.

Tangu zamani anaheshimiwa na Kanisa Katoliki, Waorthodoksi, halafu na Waanglikana kama mtakatifu na babu wa Kanisa.

Wakatoliki wanamheshimu pia kama mwalimu wa Kanisa tangu mwaka 1851, alipotangazwa na Papa Pius IX.

Sikukuu yake inaadhimishwa kila mwaka tarehe 13 Januari.

## Sirili wa Yerusalemu (315 - 386 hivi)



Sirili wa Yerusalemu alikuwa askofu wa mji huo nchini Israeli kuanzia mwaka 348 hadi kifo chake (386 hivi) akijihusisha sana na mabishano kuhusu umungu wa Yesu Kristo hata akadhulumiwa na Waario na serikali ya Dola la Roma.

Alizaliwa mwaka 315 katika familia ya Kikristo mjini Yerusalemu au karibu nao. Baada ya kupata elimu bora upande wa lugha na fasihi, iliyokuwa msingi wa ujuzi wake wa kidini wenye kutegemea Biblia, alipadirishwa na askofu Masimo.

Alipokufa (au alipoondoshwa) huyo, Sirili alichaguliwa kuwa askofu wa Yerusalemu na kuwekwa wakfu na Akasio, askofu mkuu wa Kaisarea Baharini,. Alipewa daraja hiyo kwa sababu alidhaniwa kuelekea uzushi wa Waario, hivyo hata Wakatoliki walimuona amekubali uzushi. Kumbe alikuwa hatumii neno "homousios" lililopitishwa na Mtaguso I wa Nisea, kwa sababu hakupenda kutumia maneno yasiyopatikana katika Biblia, tena aliogopa litatafsiriwa vibaya.

Basi, alikuja kubishana na Waario mapema juu ya umungu wa Yesu, pamoja na kutetetea hadhi ya Kanisa la Yerusalemu kwamba halitakiwi kuwa chini ya Kaisarea. Kwa sababu hiyo mara tatu alifukuzwa kutoka nchini mwake (357, 360, 367-378).

Kaisari Valens alipofariki, Sirili aliweza kurejea Yerusalemu na kurudisha umoja na amani kati ya waamini.

Mwaka 381 alishiriki Mtaguso I wa Konstantinopoli akitoa mchango mkubwa. Baada ya hapo, usahihi wa imani yake, uhalali wa uaskofu wake na stahili za uchungaji wake vilithibitishwa na barua ya maaskofu wa mashariki kwa Papa (382).

Moyo wake wa kichungaji unaonekana hasa katika kitabu chake *Catecheses*, yaani mafundisho 24 kwa wakatekumeni na kwa Wakristo wapya aliyoyatoa mwaka 350 hivi akiwa katika Kanisa la kaburi la Yesu na pengine.

Humo anawaeleza masharti ya ubatizo, uongofu, sakramenti, kweli za Ukristo, sala ya Bwana na hatimaye mafumbo waliyoyashiriki katika liturujia.

Alifanya hivyo akiwaelekeza kwa Kristo, kiini cha ulimwengu, kwa kulinganisha Maandiko Matakatifu ya Agano la Kale na Agano Jipya na kutegemea mapokeo ya Kanisa la Yerusalemu pamoja na kupinga hoja za Wapagani, Wamani, Wakristo wa Kiyahudi na Waario.

Ni kati ya vitabu vya zamani vilivyo muhimu zaidi kuhusu katekesi, kikiwa wazi upande wa mawazo na wa ufafanuzi wake na kutumia mifano mingi. Kwa pamoja hotuba hizo zinaongoza kuelewa maana ya kuzaliwa upya.

Humo tunaona alivyotaka Wakristo wawe na imani ya dhati, na alivyowaelekeza njia ya kuishi kadiri ya imani hiyo: kuanzia Ubatizo, kupitia Ekaristi hadi maisha matakatifu. Kaulimbiu yake ilikuwa: "Mkristo anambeba Kristo". Kwake imani na maadili vinakwenda pamoja.

Aliwaambia wakatekumeni: "Nyinyi mmenaswa katika wavu wa Kanisa. Basi, mtekwe wazima; msikimbie, kwa sababu ni Yesu anayewavua, si kwa lengo la kuwaua bali la kuwafufua baada ya kifo. Hakika, mnapaswa kufa na kufufuka… Fieni dhambi zenu na kuishi kwa uadilifu tangu siku hii".

Baada ya ubatizo aliwaambia: "Wakati uleule nyinyi mlikufa na kuzaliwa; na yale maji ya wokovu yalikuwa kwa pamoja kaburi lenu na mama yenu… Kwenu wakati wa kufa umekuwa pia wakati wa kuzaliwa".

Ugumu wa Sirili katika kuruhusu ubatizo wa wakatekumeni na udhati wa imani aliowafikishia ni ushahidi wa uhai wa Ukristo katika karne IV.

Aliona ubatizo kuwa "ukombozi wa wafungwa, msamaha wa makosa, kifo cha dhambi na kuzaliwa upya kwa roho" na alikanusha uwezekano wa kuokolewa kwa wasioupata ama kwa maji ama kwa damu.

Kuhusu ekaristi, alikuwa mwanateolojia wa kwanza kufafanua uwemo halisi wa Mwili na Damu ya Kristo kama tokeo la badiliko la dhati za mkate na divai likisababishwa na Roho Mtakatifu kuitwa juu ya vipaji hivyo. Alifananisha badiliko hilo na lile la maji kuwa divai kwenye arusi ya Kana. Vilevile, Sirili alieleza jinsi ekaristi ilivyo sadaka ya kiroho na ya maombezi.


Alifariki mwaka 386 au 387.

Tangu zamani anaheshimiwa kama mtakatifu na babu wa Kanisa.

Mwaka 1883 Papa Leo XIII alimuongezea sifa ya mwalimu wa Kanisa.

Sikukuu yake inaadhimishwa kila mwaka tarehe 18 Machi.

# Basili (329 hivi - 379)



Basili wa Kaisarea alikuwa askofu mkuu wa mji huo (leo Kayseri nchini Uturuki). Anaitwa Basili Mkuu kwa sababu ni kati ya mababu wa Kanisa muhimu zaidi.

Alizaliwa mwaka 329 hivi huko Caesarea Mazaca, yaani Kaisarea ya Kapadokia , katika familia tajiri ya mhubiri maarufu Basili Mzee na ya Emelia wa Kaisarea, waliojulikana kwa imani yao. Walisaidiwa malezi na bibi wa Basili, Makrina Mzee. Babu yake alikuwa mfiadini. Wote wawili wanaheshimiwa kama watakatifu.

Familia ya Basili ilikuwa na watoto 10; kati yao wanaheshimiwa pia kama watakatifu Makrina Kijana aliyekuwa mmonaki, Petro wa Sebaste aliyekuwa askofu na mwanateolojia huko Armenia, Naukrasyo aliyekuwa mkaapweke, na hasa Gregori wa Nisa ambaye alifanywa na Basili kuwa askofu wa mji huo akaandika vitabu bora kuhusu teolojia na maisha ya Kiroho.

Basili alikuwa na vipawa vya pekee: akili kali, wema mkubwa, uwezo wa kupanga na kufanikisha mambo, nguvu katika utendaji, busara na kiasi katika yote. Ni kati ya wanakanisa kamili zaidi wa nyakati zote.

Bado mtoto alihamia mkoa wa Ponto hadi alipofiwa baba yake ambapo akarudi Kaisarea ili kupata walimu. Huko alikutana na Gregori wa Nazianzo, wakawa marafiki maisha yake yote.

Wote wawili walikwenda kusoma Konstantinopoli, halafu kwa miaka sita Athene, walipokutana na atakayekuwa Kaisari Juliano Mwasi. Ndiko alikoanza kufikiria maisha ya Kikristo hasa. Hata hivyo hakuacha kutia maanani elimudunia, aliyokuwa nayo kwa wingi, hasa kwa ajili ya malezi ya vijana, ambao daima aliwashughulikia sana.

Kutokana na mang'amuzi yake kuhusu vitabu vya Wapagani wa zamani, alihimiza upambanuzi: "Tukiwa na hekima, tutachota katika maandishi hayo vile ambavyo vinatufaa na vinalingana na ukweli, na tutapuuzia vile vingine."

Alipohama Athene mwaka 355 hivi, Basili alifanya kwa muda mfupi kazi ya wakili na mwalimu wa kuhubiri huko Kaisarea, lakini mwaka uliofuata alibadili maisha kisha kukutana na askofu Eustasi wa Sebaste.

Aliandika, "Siku moja, kama mtu aliyezinduka kutoka usingizi mzito, niligeuza macho yangu kwenye mwanga wa ajabu wa ukweli wa Injili… nikalia machozi mengi juu ya maisha yangu duni". Hapo, kwa kuvutiwa na Yesu, alianza kumtazama na kumsikiliza yeye tu, akijitosa katika sala, tafakuri juu ya Biblia na maandishi ya mababu wa Kanisa, pamoja na kutekeleza upendo, kwa kufuata pia mfano wa dada yake, Makrina, aliyekwishashika maisha ya kimonaki.

Baada ya kupata ubatizo, Basili alisafiri tena (357) kwenda Misri, Palestina, Siria na Mesopotamia ili kufahamu zaidi maisha ya kiroho na umonaki.

Ingawa aliguswa na utakatifu wa wamonaki maarufu aliokutana nao huko, kipeo cha ukaapweke hakikumvutia zaidi. Badala yake alielekea maisha ya kijumuia. Hivyo alirekebisha umonaki usiwe mbali mno na watu wa kawaida, bali uathiri maisha yao kwa roho ya Kikristo. Kiongozi halisi katika njia ya Mungu, hakuruhusu malipizi ya ajabuajabu, bali alidai utekelezaji wa matendo ya upendo.

Kisha kugawa mali yake kwa mafukara alikwenda kwa muda mfupi kuishi upwekeni karibu Neokaisarea mtoni Iris, lakini mwaka 358 alianza kupokea wafuasi, mmojawao ndugu yake Petro. Pamoja naye alianzisha monasteri huko Arnesi kwenye mkoa wa Ponto. Huko walijiunga hata mama yake, dada yake Makrina na wanawake wengine, wakijitoa kusali na kutekeleza matendo ya huruma.

Ni huko kwamba Basili aliandika vitabu kuhusu umonaki (Kanuni mbili) vilivyoathiri Kanisa lote hadi leo, hata akaitwa "baba wa umonaki wa mashariki". Mt. Benedikto wa Nursia mwenyewe, "baba wa umonaki wa magharibi", alimhesabu kama mwalimu wake. Kwa jumla mfumo wa umonaki haueleweki bila kumsikiliza Basili.

Mwaka 358 alimualika Gregori wa Nazianzo ajiunge naye, halafu kwa pamoja walitunga *Filocalia*, mkusanyo wa maandishi bora ya Origene. Baadaye Gregori akarudi kwao.

Basili alishiriki Mtaguso wa Konstantinopoli wa mwaka 360 alipokubali neno "homoiousios" kuwa sahihi kuelezea Yesu ni "kama" Mungu Baba, si "sawa" wala si "tofauti" naye. Baada ya kulaumiwa na askofu wake, Dianius wa Kaisarea, aliacha mtazamo huo akashika moja kwa moja Kanuni ya Imani ya Nisea.

Mwaka 362 Basili alipewa daraja takatifu ya ushemasi kwa kuwekewa mikono na askofu Melesyo wa Antiokia. Baadaye aliitwa na Eusebi wa Kaisarea arudi kwao, akapewa upadrisho mwaka 365.

Miaka iliyofuata Basili na Gregori walipambana na uzushi wa Ario ulioenea Kapadokia wakawa washindi katika midahalo. Hivyo Basili alikabidhiwa usimamizi wa mali ya jimbo la Kaisarea. Eusebi akamuonea kijicho akamruhusu arudi upwekeni. Lakini Gregori alimshauri arejee tena na kushika nafasi yake kama kiongozi halisi wa jimbo hilo.

Mwaka 370 Eusebi alipofariki, Basili alichaguliwa mwandamizi wake akapewa uaskofu tarehe 14 Juni 370. Hapo alikataa katakata mashinikizo ya Kaisari aliyetaka aunge mkono uzushi wa Ario; kinyume chake alijitahidi kurudisha umoja ndani ya Kanisa na kutetea haki ya kushika imani ya kweli kuhusu umungu wa Yesu.

Alitetea pia umungu wa Roho Mtakatifu ambaye aliandika kitabu kizima juu yake: "lazima alinganishwe na kutukuzwa pamoja na Baba na Mwana". Hivyo Basili ni kati ya mababu walioweka wazi fundisho la Utatu Mtakatifu: Mungu pekee, kwa kuwa ni upendo, ni nafsi tatu zinazounda umoja wa Kimungu, imara kuliko umoja wowote.

Pamoja na kuchunga kiroho waamini wa jimbo lake kubwa, na kujitahidi kuleta watu wote kwa Kristo, alizingatia mahitaji ya kimwili ya kila mmoja, akajitosa kwa ajili ya maskini, wezi na makahaba, akihimiza watawala kuinua hali ya wananchi hasa wakati wa maafa, na akilaumu hadharani walioshindwa kutoa hukumu kwa haki. Alianzisha mtaa wenye majengo kwa ajili ya mafukara, wageni na wagonjwa, uliokuja kuitwa Basiliade. Ulikuwa na hospitali, shule na viwanda.

Kama askofu wa Kaisarea alikuwa pia askofu mkuu mwenye majimbo 5 chini yake: hata huko alianzisha makimbilio kwa shida yoyote ile.

Kwa lengo la kushika kikamilifu udugu wa Kiinjili kama katika Kanisa la mwanzoni, alianzisha maisha ya pamoja katika "jamaa". Tofauti na monasteri za Pakomi, zilizofikia kuwa na watawa elfu, jamaa hiyo haikuwa na idadi kubwa wala ngome; tena haikuwa jangwani, bali karibu na mji wa Kaisarea. Tofauti na unyofu wa wamonaki wa jangwani, alitia maanani masomo ya kidini, na hasa maandishi ya Origene.

Akiwa askofu alitembelea mara nyingi jamaa hizo akisisitiza, pamoja na maendeleo ya kiroho, uhusiano na Kanisa lao: alitaka watawa wa kiume na wa kike wawe chachu inayofanya Wakristo wenzao wote wafuate utakatifu wa wito wao. Tena aliwakabidhi shughuli mbalimbali kama vile kuhubiri na hasa kuhudumia wenye shida. Mtindo huo ulisisitiza ushirikiano kati ya ndugu kuliko uongozi wa abati na miundo mikubwa.

Mhubiri mwenye nguvu, alishambulia uroho wa matajiri na ulegevu wa Wakristo wasiotimiza wajibu wao.

Pamoja na kuwajibika mfululizo kutekeleza matendo ya huruma, alirekebisha pia liturujia ya ekaristi na kustawisha matumizi ya Zaburi kati ya waamini, kiasi kwamba walizisali hata usiku; na kuhimiza waamini wapokee kila siku Ekaristi, chakula wanachohitaji ili kupata nguvu mpya ya kuishi kikamilifu kadiri ya neema ya ubatizo. Alisema ni furaha kubwa kuweza kushiriki Ekaristi iliyowekwa "ili kudumisha bila kikomo kumbukumbu ya Yule aliyekufa na kufufuka kwa ajili yetu".

Alipanga maisha ya Kanisa bila kukubali serikali iyaingilie. Alipodaiwa na mjumbe wa Kkaisari Valens alegeze msimamo wake dhidi ya Ario, Basili alimjibu, "Labda wewe hujawahi kuhusiana na askofu yeyote". Baada ya jibu hilo Kaisari alikwenda kushiriki misa yake akampa eneo kwa ajili ya Basiliade. Tukio hilo lilisaidia kuonyesha mipaka kati ya mamlaka ya serikali na ile ya Kanisa.

Basili aliwasiliana pia na Papa Damas I ili Kanisa la Roma litumie mamlaka yake kulaani uzushi wa Ario mashariki kama magharibi. Lakini hakuishi kirefu kutosha aone ushindi wa imani sahihi aliyoitetea. Juhudi zake kubwa za kutimiza vizuri wajibu wake kama askofu zilimmaliza tarehe 1 Januari 379, akiwa na umri wa miaka 49 tu.

Katika Kanisa alitekeleza kiaminifu mpango alioufanya mapema, wa kuwa "mtume na mtumishi wa Kristo, msimamizi wa mafumbo ya Mungu, mtangazaji wa Ufalme, kielelezo na kipimo cha uadilifu, jicho la Mwili wa Kanisa, mchungaji wa kundi la Kristo, mwalimu, baba na tabibu mpendevu, mfanyakazi pamoja na Mungu, mkulima wa Mungu, mjenzi wa hekalu la Mungu".

Kwa jinsi alivyomkazia macho Kristo na kupenda watu, alianza kuheshimiwa kama mtakatifu punde baada ya kifo chake, na mwaka 1568 Papa Pius V alimuongezea sifa ya mwalimu wa Kanisa.

Sikukuu yake inaadhimishwa kila mwaka tarehe 2 Januari.

Alifundisha kuwa mwanga wa fumbo la Mungu unarudishwa na binadamu aliye sura yake; ni hasa kwa kumtazama Kristo kwamba tunaweza kutambua hadhi yetu. "Zingatia ukuu wako, ukikumbuka ulivyogharimiwa: tazama bei ya ukombozi wako na kuelewa hadhi yako!"

Kwa namna ya pekee Wakristo wakijilinganisha na Injili, wanapaswa kuwatambua watu wote kama ndugu, tena kujiona wasimamizi wa mali waliyojaliwa ili wawajibike kila mmoja kwa ajili ya wenzake, "wakitekeleza maagizo ya Mungu mfadhili". "Macho ya mafukara wote yanaelekea mikono yetu kama vile ya kwetu yanavyoelekea ile ya Mungu tukiwa na shida".


Kuhusu hilo alitumia kishujaa maneno makali katika hotuba zake, kwa sababu anayetamani kumpenda jirani kama anavyojipenda, kadiri ya amri ya Mungu "hatakiwi kuwa na mali yoyote kuliko jirani yake". Hasa wakati wa maafa alihimiza waamini wasiwe "wakatili kuliko hayawani… kwa kujipatia vile ambavyo wote wanamiliki kwa pamoja au kwa kuteka vitu vilivyo mali ya wote".

**Kwa Kiswahili**

MT. BASILI WA KAISARIA, Kanuni za kimaadili – tafsiri ya Familia za Maamkio – Mapanda - ed. Ndanda Mission Press – Ndanda 2005 – ISBN 9976-63-674-X

PADRE FRIDOLIN, Maisha ya Mtakatifu Makrina - ed. N.M.P. - Ndanda

## Gregori wa Nazianzo (329 – 390 hivi)



Gregori wa Nazianzo alikuwa askofu, mwanateolojia na mwanashairi maarufu kutoka katikati ya nchi ambayo leo inaitwa Uturuki.

Alizaliwa mwaka 329 huko Arianzo, leo Güzelyurt, kijiji karibu na Nazianzo, mkoani Kapadokia, katika familia ya kisharifu ya watakatifu. Baba yake aliitwa Gregori Mzee na mama yake Nonna. Baba, aliyekuwa Myahudi, aliongokea Ukristo kwa msaada wa mke wake na hatimaye akawa askofu wa Nazianzo.

Gregori, aliyezaliwa miaka 4 baada ya Mtaguso I wa Nisea (325) uliolaani uzushi wa Ario, aliathiriwa na mapambano hayo ya kiimani maisha yake yote.

Mwenye akili kali na ubunifu mkubwa, alielekea sana upweke na maisha ya sala, lakini wema na ari yake, pamoja na ufasaha wa ajabu wa mahubiri yake vilimrudisha kati ya watu. Ila alipokabiliana na upinzani mkali, moyo wake mpole na mwepesi kuguswa ulimfanya akimbie tena upwekeni.

Kuhusu mwelekeo huo aliandika: “Sioni kitu kikuu kuliko hiki: kunyamazisha hisi zangu, kuinuka juu ya mwili wa ulimwengu, kujifungia ndani mwangu, kutoshughulikia tena mambo ya kibinadamu isipokuwa ya lazima kabisa; kuongea na nafsi yangu na Mungu, kuendesha maisha yanayopita vitu vinavyoonekana, kubeba rohoni taswira za Kimungu, safi daima, zisizochanganyikana na maumbo ya kidunia au madanganyifu, kuwa kweli kioo kamili cha Mungu na cha mambo yake, tena kuwa hivyo zaidi na zaidi, kwa kuchota mwanga kutoka mwanga… kufurahia kwa tumaini la sasa mema yajayo na kuongea na malaika, kuwa nimeacha tayari dunia ingawa naishi bado juu yake, nikiinuliwa na roho”.

Alisoma kwanza huko Kaisarea ya Kapadokia, alipofunga urafiki wa kudumu na Basili Mkuu, halafu katika vyuo bora vya wakati ule: Kaisarea ya Palestina, Aleksandria ya Misri, Konstantinopoli na hatimaye (350-357) huko Athene, Ugiriki.

Aliporudi kwao tu, ndipo alipobatizwa, ingawa mama yake alikuwa amemtoa kwa Mungu siku ileile ya kuzaliwa.

Baada ya kujiunga na Basili kwenye monasteri ya Annisoi, katika mkoa wa Ponto (358), na kumsaidia kutunga Filokalia, alirudi nyumbani alipotarajia kuishi upwekeni zaidi. Kumbe mwaka 361 baba yake aliamua kumpa upadrisho. Kwanza alikimbia, lakini baadaye alikubali kufuata maongozi ya Mungu yaliyozidi kumpeleka asikotaka mwenyewe, na akishinda silika yake ya aibu alitumia vipawa vyake kama mwandishi na mhubiri mahiri kwa ajili ya Kanisa.

Alisema, “Kama mtumishi wa Neno, nawajibika katika huduma ya Neno; nisikubali kamwe kuzembea katika jema hilo. Nathamini wito huo na kushukuru kwa ajili yake; unanipa furaha kuliko mambo mengine yote pamoja”.

Mwaka 372 Basili, akiwa askofu mkuu wa Kaisarea ya Kapadokia, alimteua kuwa askofu wa Sasima. Kutokana na upinzani wa Kaisari, Gregori hakuweza kamwe kwenda huko, akatawa Seleukia, lakini alipofiwa baba yake alirudi Nazianzo, aongoze Kanisa la huko.

Mwaka 379 aliitwa aongoze Wakristo wachache wa Konstantinopoli walioshika Kanuni ya imani ya Nisea. Majengo yote yalikuwa yanamilikiwa na Waario walioungwa mkono na serikali. Lakini Theodosi I alipotawazwa kama Kaisari mwaka 380 aliyatoa kwa hao Waorthodoksi.

Jijini huko, dhidi ya upinzani uliomzunguka, alitetea na kufafanua imani katika Utatu Mtakatifu kwa hotuba tano zilizomstahilia jina la "Mwanateolojia". Mwenyewe alieleza kuwa "teolojia" si "teknolojia", yaani haitegemei hoja za binadamu, bali inatokana na maisha ya sala na utakatifu. Udhati wa mafundisho pamoja na uzuri wa namna yalivyotolewa zinafanya hotuba hizo zituvutie hata leo.

Theodosi I alimtawaza Patriarki wa Konstantinopoli na kuhakikisha kwamba atambuliwe hivyo na Mtaguso I wa Konstantinopoli mnamo Mei 381.

Katika huo mtaguso mkuu majadiliano yalikuwa makali hata dhidi yake binafsi, kwa sababu alitetea kwa nguvu umungu wa Yesu Kristo na wa Roho Mtakatifu, pamoja na fumbo la Utatu mtakatifu. Alionja kwa mara nyingine alichokuwa amekilaumu kama mpenzi wa amani: “Tumemgawa Kristo, sisi tuliowapenda hivi Mungu na Kristo! Tumeambiana uongo kwa sababu ya Ukweli, tumefuga hisia za chuki kwa sababu ya Upendo, tumetengana kati yetu”.

Hatimaye, akikiri hawezi kusuluhisha, aliacha mtaguso aliokuwa anauendesha akaaga waamini katika kanisa kuu lililokuwa limejaa kabisa.

Mwishoni mwa mwaka 382 akawa askofu wa Nazianzo lakini, baada ya mwaka mmoja, alirudi upwekeni Arianzo, alipofariki tarehe 25 Januari mwaka 389 au 390.

Ni katika miaka hiyo ya mwisho, aliyoitumia katika masomo na maisha ya kiroho, kwamba aliandika sehemu kubwa ya mashairi yake, na hasa maisha yake mwenyewe, akipitia safari yake ya kiutu na ya Kikristo kama mtu wa Mungu aliyeonja mateso mengi katika ulimwengu uliojaa mabishano.

Mafundisho yake kuhusu Kristo, yanayotetea pia usahihi wa jina “Mama wa Mungu” kwa Bikira Maria, yalikuja kupitishwa na Mtaguso wa Efeso (431) na Mtaguso wa Kalsedonia (451).

Kama mwanashairi na mwanafasihi alitoa maandishi bora kuhusu imani. Zimetufikia hotuba 45, mbali ya tenzi (karibu beti 18,000!) na barua nyingi sana.

Tangu zamani anaheshimiwa na Kanisa Katoliki, Waorthodoksi, halafu na Waanglikana kama mtakatifu na mmojawapo kati ya mababu wa Kanisa muhimu zaidi.

Kwa Wakatoliki ni pia mwalimu wa Kanisa tangu mwaka 1568, alipotangazwa na Papa Pius V.

Sikukuu yake inaadhimishwa mwezi Januari tarehe 2, 25 au 30, kadiri ya madhehebu.


Gregori alihimiza kwanza sala, akisema, "Ni lazima tumkumbuke Mungu mara nyingi kuliko tunavyopumua", kwa kuwa sala ni mkutano wa kiu ya Mungu na kiu yetu: yeye ana kiu ya kutuona tuna kiu naye. Katika sala tunapaswa kuelekeza mioyo yetu kwake, kujiaminisha kwake kama sadaka ya kutakaswa na kugeuzwa. Katika sala tunaona vyote katika mwanga wa Kristo, tunaacha vinyago tunavyojifunika vianguke na tunazama katika ukweli na katika kumsikiliza Mungu, tukichochea moto wa upendo.

Pia alisisitiza ukamilifu wa utu wa Yesu, ukiwa pamoja na roho ya kibinadamu, kama sharti la wokovu wetu: "Kisichowahi kutwaliwa hakijaponywa". Kama yeye "asingekuwa na akili inayoweza kufikiri, angekuwaje mtu?" Kumbe, kwa kujifanya kweli mtu, ametuwezesha kuwa kama yeye: "Tujitahidi kuwa kama Kristo, kwa sababu Kristo naye amekuwa kama sisi: kugeuka miungu kwa njia yake, kwa sababu mwenyewe amekuwa mtu kwa njia yetu. Alijitwalia yaliyo duni zaidi ili atuzawadie yaliyo bora".

Bikira Maria, aliyempa Kristo umbile la mtu, ni kweli Mama wa Mungu; na kwa ajili ya kazi hiyo muhimu sana "alitakaswa kabla ya wakati". Yeye ni kielelezo na msaidizi wa kumkimbilia katika shida.

Kama binadamu, tunapaswa kushikamana: "Sisi sote ni kitu kimoja katika Bwana, matajiri na mafukara, watumwa na watu huru, wenye afya na wagonjwa pia; na mmoja ndiye kichwa kinachotegemewa na vyote: Yesu Kristo. Ni kama vile kwa viungo vya mwili mmoja, kila kimoja kinashughulikia kingine, na vyote kwa vyote. Huu ndio wokovu pekee kwa mwili wetu na roho yetu: kuwatendea kwa upendo… Ukiwa mzima na tajiri, punguza shida za yeyote aliye mgonjwa na fukara; kama hujaanguka, nenda kumsaidia yeyote ambaye ameanguka na anaishi kwa mateso; ukiwa na furaha, umfariji yeyote mwenye huzuni; ukiwa na hali njema, umsaidie yeyote aliyepigwa na mabaya. Umthibitishie Mungu shukrani yako kwa kuwa unaweza kusaidia, si mtu wa kuhitaji msaada… Uwe tajiri si kwa mali tu, bali pia kwa huruma; si kwa dhahabu tu bali pia kwa uadilifu, au afadhali kwa uadilifu tu. Zidi sifa ya jirani yako kwa kujionyesha mkarimu kuliko wote; ujifanye Mungu kwa wenye mashaka, ukiiga huruma ya Mungu".

## Ambrosi (340 hivi - 397)



Aureli Ambrosi alikuwa askofu wa Milano kuanzia mwaka 374 hadi kifo chake. Ndiye aliyemuongoa na kumbatiza Augustino wa Hippo.

Kati ya mambo ya pekee aliyoacha ni urithi wa tenzi na liturujia ya pekee inayoendelea kutumika Milano na sehemu nyingine kadhaa za Italia na Uswisi ("liturujia ya Kiambrosi").

Ambrosi alizaliwa mwaka 340 hivi katika familia ya Kikristo ya Dola la Roma mjini Trier, leo nchini Ujerumani, akakulia huko.

Baba yake, aliyeitwa Ambrosi Aureliani, alikuwa liwali wa Galia (leo Ufaransa); mama yake alijulikana kwa akili na imani yake. Ndugu zake, Satiro na Marselina wanaheshimiwa pia kama watakatifu.

Alipofiwa baba, Ambrosi alihamia Roma (353) pamoja na mama aliyemuandaa kufuata nyayo za baba yake katika siasa. Alisomea huko, hasa fasihi, sheria na hotuba.

Liwali Anicius Probus kwanza alimpa nafasi katika halmashauri halafu (370) akamfanya gavana wa Liguria na Emilia, akiwa na makao makuu huko Milano, mji wa pili wa Italia. Ambrosi aliendelea na ugavana hadi mwaka 374 alipochaguliwa askofu wa Milano.

Ni kwamba, baada ya kifo cha askofu Ausensi aliyefuata uzushi wa Ario, Ambrosi alikuwa amefika kanisani atulize ghasia kati ya Waario na Wakatoliki. Kumbe alipohutubia umati, akashangiliwa na pande zote mbili, "Ambrosi, askofu! Ambrosi, askofu!". Alitaka kukataa, kwa kuwa hajabatizwa, lakini hatimaye alikubali.

Alipewa mara ubatizo, kipaimara na ekaristi, halafu wiki moja baadaye daraja takatifu ya uaskofu (tarehe 7 Desemba, ambayo imekuwa sikukuu yake hadi leo) akatoa kwa Kanisa na mafukara dhahabu na fedha zake zote.

Kama askofu, zaidi ya useja, alishika juhudi za kitawa, akajitahidi kupata elimu ya Biblia na teolojia hasa kutoka vitabu vya Origene akaitumia vema katika kuhubiri, akifafanua kwa upana na udhati maandiko matakatifu aliyoyatafakari kwanza. Hivyo alieneza magharibi mtindo wa Lectio Divina ulioanzishwa na mtaalamu huyo wa Misri.

Augustino aliandika kwamba kila alipokwenda kumuona Ambrosi alimkuta amefikiwa na umati wa watu wenye shida mbalimbali, ambao alijitahidi kwa kila namna kuwasaidia. Kila mara kulikuwa na foleni ndefu ikisubiri kuongea naye ili kupata faraja na tumaini. Akibaki kidogo peke yake, alilisha au mwili kwa kula au roho kwa kusoma.

Mwenye nguvu na udumifu, pamoja na kipawa cha kuhisi nini inawezekanika, aliongoza jimbo vizuri ajabu kama mchungaji halisi, mwenye msimamo na busara, na hasa wema na upendo. Hivyo hakufukuza mara wakleri waliofuata mafundisho ya Ario.

Mwaka 378 alikutana na Kaisari Grasyano, aliyemuomba amfundishe imani sahihi, kinyume na mafundisho ya Ario. Baadaye Kaisari huyo alizidi kusimama upande wa Wakatoliki akatoa hati dhidi ya wazushi (22 Aprili 380) halafu akaieneza kwa Wapagani, akiwaondolea fadhili zao za awali. Mwaka uliofuata wote wawili walishiriki Mtaguso wa Aquileia ili kuimarisha imani sahihi katika dola.

Baada ya Grasyano kuuawa (383), ilimbidi Ambrosi azidi kupambana na wafuasi wa Ario, mmojawao akiwa Kaisari Masimo aliyedai (386) awaachie makanisa mawili ya Milano. Ambrosi alikataa katakata, akisema, "Ukinitaka mwenyewe, niko tayari kutii: unipeleke gerezani au kifoni, sitapinga; lakini sitasaliti kamwe Kanisa la Yesu Kristo. Sitaita watu kunisaidia; nitakufa kwenye altare lakini si kuikimbia. Sitahimiza watu kupiga kelele lakini Mungu tu ataweza kuwatuliza". Hivyo alihamia pamoja na wafuasi wake basilika lililogombaniwa wakaendelea kulitumia usiku na mchana. Kadiri ya Augustino, aliyeguswa sana na umoja huo, ndiyo mwanzo wa nyimbo za Ambrosi: "Umati wenye imani ulikesha, ukiwa tayari kufa pamoja na askofu wao… Sisi pia, ingawa vuguvugu kiroho, tulishiriki katika mhemko wa wote".

Ikulu haikupendezwa na msimamo wa Ambrosi, lakini ilimuogopa na kumhitaji katika mapambano ya siasa. Mahusiano yaliendelea kuwa magumu. Hatimaye Theodosi I, Kaisari wa Mashariki, alipoangamiza (390) watu 7,000 huko Thesalonike (Ugiriki), Ambrosi alitisha kumtenga na Kanisa asipofanya toba kama mfalme Daudi, akamruhusu kupokea tena ekaristi baada tu ya miezi kadhaa ya malipizi.

Mtetezi wa wale wote walionyanyaswa, alipambana vilevile na seneti ya Roma na malkia ili kutetea siasa ya Kikristo kweli. Msimamo wake ulibaki kielelezo kwa Kanisa la Magharibi hata likaendelea kudai uhuru na mara nyingi kushindana na mamlaka ya serikali zisizotenda haki.

Ambrosi alipaswa pia kupambana na Wapagani waliotaka kufanya tena dini ya jadi kuwa dini rasmi ya Dola la Roma badala ya Ukristo. Alifaulu kumfanya Theodosi I atoe hati zake maarufu za mwaka 391.

Mtume wa upendo, alisaidia yeyote aliyemkimbilia, hata akauza vyombo vya ibada ili kukomboa watumwa, akisema, "Ikiwa Kanisa lina dhahabu, si kwa ajili ya kuitunza, bali ili liwape wanaohitaji".

Tarehe 4 Aprili 397, siku ya Ijumaa Kuu, Ambrosi alifariki huku amenyosha mikono yake kama Yesu msalabani, akaheshimika mara kama mtakatifu. Masalia yake, ambayo ni kati ya maiti za zamani zaidi zilizopo nje ya Misri, yanatunzwa katika kanisa lake mjini Milano.

Ambrosi aliandika sana, ila si vitabu vyake vyote vimetufikia: vilikuwepo ishirini hivi vya ufafanuzi wa Biblia na vingine juu ya mafumbo ya imani na juu ya maadili. Tunazo pia hotuba za mazishi, barua, mashairi na tenzi hasa kwa ajili ya liturujia.

Kwa jumla maandishi yake ni ya kichungaji kuliko ya kinadharia, pia kutokana na jinsi alivyopata uaskofu ghafla. Alijaribu kuziba pengo la ujuzi wa teolojia, lakini bila mafanikio makubwa. Ndiyo sababu anategemea sana mababu waliomtangulia.

Kuhusu Kristo, anatofautisha ndani yake hali mbili (umungu na utu) na vilevile utashi wa Kimungu na ule wa kibinadamu. Alikuwa hachoki kusema, "Kwetu Kristo ni kila kitu!" akifafanua, "Ukiwa na donda linalohitaji kuponywa, yeye ndiye mganga; ukiwa na joto la homa, yeye ndiye burudisho; ukilemewa na dhuluma, yeye ndiye haki; ukihitaji msaada, yeye ndiye nguvu; ukiogopa kifo, yeye ndiye uzima; ukitamani mbingu, yeye ndiye njia; ukiwa gizani, yeye ndiye mwanga… Onja na kuona jinsi Bwana alivyo mwema: heri mtu anayemtumainia!"

Kuhusu ukombozi, alidhani kifo cha Yesu kilikuwa gharama iliyolipwa kwa shetani ili kuokoa watu.

Kuhusu Bikira Maria, alimuona hakuwa na dhambi maisha yake yote.

Kuhusu kitubio, alionelea kwamba kwa dhambi kubwa sana kitolewe mara moja tu, tena hadharani.

Tangu zamani anaheshimiwa kama babu wa Kanisa.

Mwaka 1298 Papa Bonifasi VIII alimuongezea sifa ya mwalimu wa Kanisa.

### Kwa Kiswahili

> MT. AMBROSI WA MILANO, Juu ya Sakramenti za kikristo (Explanatio Simboli – De Sacramentis – De Mysteriis) – tafsiri ya G. M. Brandolini na T. Serra – ed. Ndanda Mission Press – Ndanda 2004 – ISBN 9976-63-664-4

## Yohane Krisostomo (347 hivi - 407)



Yohane Krisostomo, yaani "Mdomo wa dhahabu", alivyoitwa kutokana na ubora wa mahubiri yake, alikuwa Patriarki wa Konstantinopoli. Ari yake ilisababisha apendwe na vilevile achukiwe sana. Hatimaye alifukuzwa na Kaisari na kufa uhamishoni.

Yohane alizaliwa Antiokia ya Siria, leo Antakya, nchini Uturuki, katika familia tajiri ya Kikristo mwaka 347 hivi, wakati ambapo mji huo ulikuwa unafuata Konstantinopoli na Aleksandria tu kwa umuhimu upande wa mashariki wa Dola la Roma. Katika karne IV huko zilitokea vurugu nyingi kwa msingi wa dini. Mjini kulikuwa na maaskofu wawili walioshindana: Melesyo na Paulino. Yohane aliishi ujana wake katika mazingira hayo, akikosa utulivu na kupenda vyakula na maigizo.

Baba yake, Sekundo, aliyekuwa askari kiongozi, alifariki mapema na kumuacha mtoto mdogo pamoja na dada yake kwa mama yao, Anthusa, mwenye umri wa miaka 22 tu, ambaye alimlea vizuri sana upande wa utu na wa imani vilevile.

Baada ya masomo yote, alifundishwa tena na Libanio, mhubiri maarufu kuliko wote wa wakati ule ingawa Mpagani, ambaye alisema juu yake, "Angekuwa kati ya wanafunzi wangu bora, kama Kanisa lisingeniibia". Kumbe Yohane akaja kumzidi, ila upande wa kuhubiri Neno la Mungu.

Alipofikia miaka 18 alikutana na askofu Melesyo akamuomba ubatizo (alioupata mwaka 368) akaanza kufuata kozi za Diodoro wa Tarso, maarufu kwa ufafanuzi wa Biblia usiofuata sana maana ya kiroho bali maneno yenyewe.

Alipomaliza masomo hayo (367-372), na kupewa daraja ndogo akajifungia upwekeni miaka minne akasoma teolojia, hasa Injili na nyaraka za Mtume Paulo. Katika pango alimoishi miaka miwili tena, afya yake ikawa mbovu ikamrudisha Antiokia kwenye wito wake halisi: uchungaji. Uzoefu wa kutafakari Neno la Mungu upwekeni ulikuwa umestawisha ndani yake msukumo mkubwa wa kushirikisha wengine kwa kuhubiri Injili.

Alitunga juu ya upadri kitabu kilichoathiriwa sana na Gregori wa Nazianzo. Humo alieleza kuwa umonaki si njia pekee ya kulenga ukamilifu; bali kutoa huduma za kipadri kwa faida ya waamini kati ya vishawishi vingi vya ulimwengu ndiyo njia bora ya kumtumikia Mungu. Aliandika kwamba angetakiwa kuchagua kati ya matatizo ya kuongoza Kanisa na utulivu wa maisha ya kimonaki angechagua mara elfu huduma ya kichungaji.

Miezi ya baridi kati ya miaka 380–381 alipewa na Melesyo daraja ya ushemasi na mwaka 386 akawa kasisi na msaidizi mkuu wa askofu Flaviano, akihubiri katika kanisa muhimu zaidi la Antiokia.

Wakati huo alisema, “Mtu mmoja mwenye ari anatosha kubadilisha mwenendo wa umati”. Maneno hayo yakawa kaulimbiu yake kama kiongozi wa kiroho na mchungaji wa watu akiwatia moyo kufuata maadili.

Sifa yake kama mhubiri iliongezeka, hasa Antiokia ilipokabili ghadhabu ya Kaisari kwa uasi wa mwaka 387, hata wasikilizaji wakaanza kujiandikia kumbukumbu za maneno yake. Pamoja na hayo mwenyewe aliendelea kutunga vitabu mbalimbali.

Mwaka 397 Patriarki Nektario wa Konstantinopoli alipofariki, kulikuwa na ushindani mkubwa kwa kushika nafasi yake, mpaka Kaisari Arcadio, kinyume cha matarajio ya wote, alipomchagua Yohane, ambaye hakuwa na hamu hiyo. Alihamia huko kwa kutumiwa tu nguvu na udanganyifu, bila kujua namna ya kuhusiana na vigogo.

Huko Konstantinopoli aliongoza Kanisa kwa bidii nyingi ili kulirekebisha, akishambulia ufisadi na anasa ya viongozi, akijipatia hivyo maadui wengi kwenye ikulu. Hivyo maisha yake hayakuwa na amani, tofauti na hamu ya moyo wake mpole.

Mwenyewe aliendelea kushika maisha magumu ya usahili, unyenyekevu na uchangamfu kama kielelezo kwa wote, akitumikia watu na kutumia mali yake kwa ajili ya mafukara na wagonjwa na kudai wasaidizi wake pia wafanye vilevile. Kwa usimamizi wake mzuri alianzisha na kuendesha miundo mbalimbali ya misaada, hata akaitwa “Mtoasadaka”.

Isitoshe, katika mahubiri yake alipendekeza Kanisa la Konstantinopoli lifuate kielelezo cha lile la kwanza la Yerusalemu na hivyo lichangie ujenzi wa jamii mpya ambapo wote waishi kama ndugu: hakuna wa kuachwa nyuma, kwa kuwa kila mmoja ni muhimu, si jamii tu. Hivyo alichangia sana mafundisho ya Kanisa kuhusu masuala ya jamii.

Kama mchungaji halisi, aliwatendea wote kwa wema, akiheshimu wanawake kwa namna ya pekee na kuwajibika kwa ustawi wa ndoa na familia.

Alihimiza waamini washiriki katika liturujia, aliyoipamba kwa ubunifu izidi kupendeza.

Alipambana kwa nguvu na uzushi na kuleta nidhamu katika majimbo yaliyo chini yake, akiwafukuza mapadri wengi wasiofaa, na hata askofu wa Efeso na wengine watano waliopata madaraka kwa dhambi ya usimoni. Kwa hilo alilaumiwa kuwa alitumia mamlaka nje ya mipaka yake.

Pia alilazimisha wamonaki wazururaji warudi katika monasteri zao, ila alipokea wengine kutoka Misri waliokuwa wametengwa na Kanisa kwa uamuzi wa Patriarki Teofilo wa Aleksandria, ambaye alichukia hilo pia.

Mwanzoni alitegemezwa na ikulu, lakini baada ya kumlaumu malkia Eudoksia kwa kujipatia mali ya mjane, na kuishi kwa anasa, uhusiano uliharibika, akazidi kusingiziwa na kutukanwa.

Mwaka 402 maadui wake wengi, wakiwemo maaskofu, waliomba msaada wa patriarki Teofilo wa Aleksandria, ambaye Kanisa lake lilikuwa linashindana na yale ya Konstantinopoli na Antiokia. Teofilo mwenyewe alikuwa amelazimika kujitetea katika sinodi iliyoongozwa na Yohane kuhusu mashtaka ya wamonaki dhidi yake.

Basi, mwaka 403, katika sinodi ya Mwaloni, karibu na Kalsedonia, Teofilo alifika pamoja na maaskofu saba wa Misri na wengine 29 waliokuwa wote upande wake, akamfanya Yohane afukuzwe na Kaisari, ila kesho yake malkia alimrudisha baada ya umati kudai hivyo kwa nguvu.

Miezi miwili baadaye uhusiano wa Yohane na Eudoksia ulichafuka tena, askofu alipolaumu ujenzi wa sanamu ya malkia karibu na kanisa, hata alisema maadhimisho kwa ajili yake yalikuwa ya kipagani akamfananisha na Herodia mwenye hamu na kichwa cha Yohane Mbatizaji.

Masingizio na njama viliendelea, hata aliomba msaada wa Papa Inosenti I na maaskofu wengine muhimu wa magharibi, lakini huo haukuweza kuwahi: mtaguso, uliotakiwa na Kanisa la Roma ili kupatanisha pande mbili za Dola na makanisa yake yote, haukuweza kufanyika.

Basi, tarehe 9 Juni 404 Yohane alifukuzwa jimboni moja kwa moja. Kwa miaka mitatu aliishi Kukuso, kwenye milima ya Armenia, akitenda kazi kubwa hata kwa kuandika barua nyingi ili kuwatia moyo wafuasi wake waliodhulumiwa vilevile.

Kutokana na wingi wa watu waliomtembelea, mwaka 407 alihamishwa tena aende mahali pagumu zaidi, huko Pitiunte, mashariki kabisa kwa Bahari Nyeusi, lakini tarehe 14 Septemba 407 alifariki huko Comana Pontica akiwa njiani. Maneno yake ya mwisho yalikuwa: "Utukufu kwa Mungu kwa yote".

Mwaka 438, Kaisari mwingine, Theodosi II, alirudisha masalia yake Konstantinopoli ambako yalipokewa na umati kwa shangwe.

Maandishi yake ni mengi sana, kuliko ya mababu wengine wote wa Kigiriki. Sehemu kubwa ni mahubiri (zaidi ya 700) aliyoyatoa kwa kawaida wakati wa liturujia, vitabu vya ufafanuzi wa Biblia, vya teoloja n.k. mbali ya barua 241 zilizotufikia.

Kama alivyopendekeza mwenyewe kwa waamini wake baada ya yeye kupelekwa uhamishoni, tunaweza kujilisha maandishi yake badala ya kumsikia akihubiri.

Kwa jumla hakuwa mwanateolojia mwenye mwelekeo wa nadharia, bali wa kichungaji, akilenga daima maisha yaendane na mawazo na maneno. Ndiyo mada kuu ya katekesi zake bora kwa waliojiandaa kubatizwa. Akikaribia kifo, aliandika kwamba thamani ya binadamu inategemea “ujuzi sahihi wa mafundisho ya kweli na unyofu wa maisha”: hayo mawili yanatakiwa kuendana.

Aliendeleza mapokeo ya Kanisa na kutoa mafundisho ya kuaminika wakati wa fujo kuhusu imani.

Alifundisha “kujua viumbe kuanzia Muumba”, ili viwe kama ngazi ya kumfikia. Zaidi ya hayo, kwa kuwa kwetu ni vigumu kufanya hivyo, Mungu mwenyewe alijishusha akatupa Maandiko matakatifu kama barua inayokamilisha ujuzi wetu juu yake. Isitoshe, alitwaa mwili akawa kweli “Mungu pamoja nasi”, ndugu yetu hata kifo chake msalabani. Hatimaye yeye anaingia maisha yetu kwa njia ya Roho Mtakatifu ili kutugeuza kwa ndani.

Kuhusu Kristo, Yohane alimkiri Mwana kuwa na hali moja na Baba. Pia kwamba alizaliwa na Maria, bikira kabla ya kujifungua, wakati wa kujifungua na baada ya kujifungua.

Anaitwa pia “Mwalimu wa Ekaristi” kutokana na upana na utajiri wa mafundisho yake kuhusu sakramenti ya Mwili na Damu ya Kristo.

Tangu zamani anaheshimiwa kama mtakatifu na babu wa Kanisa.

Mwaka 1568 Papa Pius V alimuongezea sifa ya mwalimu wa Kanisa.

Sikukuu yake inaadhimishwa kila mwaka tarehe 14 Septemba.

## Jeromu (347 - 420)



Jeromu au Yeronimo alikuwa mmonaki, padri na mtaalamu wa Biblia, aliyemudu vizuri lugha zote za kitabu hicho pamoja na Kilatini hata akawa mwandishi bora wa lugha hiyo kati ya mababu wa Kanisa.

Alizaliwa mwaka 347 huko Strido, sehemu za Dalmatia, leo nchini Korasya, akasomea hata Roma miaka ya 360-367, akijipatia elimu ya hali ya juu, aliyoiendeleza maisha yake yote, pia kwa safari nyingi magharibi na mashariki zilizomwezesha kufahamiana na watu wengi maarufu.

Katika ujana alivutiwa na maisha ya kidunia, lakini mvuto wa Ukristo ulishinda. Maisha yake yote alijilaumu sana kwa makosa yake ya ujanani, akazidi kutambua jinsi mtazamo wa Kipagani unavyopingana na maisha ya Kikristo.

Alibatizwa huko Roma akiwa na umri wa miaka 19, akaenda Aquileia kujiunga na jumuia ya askofu Valeriani akaendelelea moja kwa moja kupambana kiume na tabia yake ngumu iliyochanganya ukali na machozi rahisi, unyofu na elekeo la kinyongo, maisha magumu na hisia kali, uadilifu na hamaki, hisani na uchungu wa maneno.

Miaka 375-377 akiishi kama mkaapweke katika jangwa la Kalchis, kusini kwa Alepo, Siria, pamoja na kunaliki vitabu, aliendeleza ujuzi wake wa Kigiriki na kuanza kufundishwa Kiebrania na Myahudi aliyeongokea Ukristo.

Mwaka 379, kisha kupewa upadri na askofu Paulino wa Antiokia, alikwenda Konstantinopoli alipokamilisha ujuzi wake wa lugha ya Kigiriki chini ya Gregori wa Nazianzo.

Baada ya kuishi kama mmonaki miaka 3 akarudi Roma (382) na kuanza kutafsiri vitabu vya Origene, mpaka alipoteuliwa na Papa Damas I kuwa karani na mshauri wake kutokana na sifa aliyokuwanayo kama mtawa na msomi. Wakati huo alikamilisha ujuzi wake wa Kiebrania kwa msaada wa mwalimu wa dini ya Kiyahudi, na baada yake akazidi kutegemea elimu ya Kibiblia ya dini hiyo badala ya mbinu za Origene.

Akishika kazi, saumu, sala na makesha, alivuta wengi kumfuata Kristo kwa karibu zaidi, hasa wanawake wa koo bora za Roma waliojifunza pia Kigiriki na Kiebrania ili wazidi kuelewa na kutekeleza Neno la Mungu chini yake.

Baada ya Papa huyo kufa (385), upinzani dhidi yake mjini ulizidi, hivyo akahamia Mashariki ya Kati, ambapo alihiji Nchi Takatifu na kutembelea wamonaki wa Misri.

Hatimaye alianzisha na kuongoza monasteri kadhaa za kike na za kiume zenye elimu ya hali ya juu, akaishi katika mojawapo huko Bethlehemu kuanzia mwaka 386 mpaka kufa kwake, akitafsiri na kufafanua Biblia hadi dakika yake ya mwisho (420).

Alimuandikia Mt. Paulino wa Nola mwongozo wa maisha yake: "Jitahidi kujua duniani kweli zile zitakazodumu milele mbinguni… Je, tangu hapa duniani mtu hajisikii kukaa katika ufalme wa mbinguni anapoishi na maandiko hayo, anapoyatafakari bila kujua wala kutafuta kingine chochote?"

Aliandika pia, "Mtu angewezaje kuishi bila kujua Maandiko, ambayo kwa njia yake anajifunza kumfahamu Kristo mwenyewe, aliye uzima wa waamini?" Kwa njia ya Biblia "Mungu anasema kila siku na waamini". "Ukisali, unasema na Bwanaarusi; ukisoma, ni yeye anayesema nawe".

Alimuandikia padri Neposyani: "Soma mara nyingi Maandiko ya Kimungu; tena afadhali mikono yako isitue kamwe Kitabu kitakatifu. Jifunze humo unachotakiwa kufundisha… Usibandukane hata kidogo na mafundisho ya mapokeo uliyofundishwa, hivi kwamba uweze kuhubiri kadiri ya imani sahihi na kupinga wanaoikanusha… Matendo yako yasiachane kamwe na maneno yako, isije ikatokea kwamba unapohubiri kanisani mtu aweze kujisemea, 'Mbona basi mwenyewe hafanyi hivyo?' Angewezaje kujadili mfungo mwalimu aliyeshiba? Hata mwizi anaweza kulaumu uroho; lakini katika padri wa Kristo, akili na maneno vinatakiwa kulingana".

Pia aliandika kwamba kila mmoja anatakiwa kuwa na ushirika na "ukulu wa Mt. Petro. Najua kwamba Kanisa linajengwa juu ya mwamba huo". "Mimi nipo pamoja na yeyote aliyeunganika na mafundisho ya Mt. Petro".

Pamoja na hayo, "katika ufafanuzi wa Maandiko matakatifu tunahitaji daima msaada wa Roho Mtakatifu".

"Tumpende Yesu Kristo, tukilenga daima kuungana naye: hapo hata yaliyo magumu yataonekana rahisi kwetu".

Kuhusu makanisa, aliandika: "Inafaa nini kupamba kuta kwa vito ikiwa Kristo anakufa kwa njaa katika nafsi ya fukara?" Tena, "Tumvike Kristo katika fukara, tumtembelee katika mtu anayeteseka, tumlishe katika mtu mwenye njaa, tumkaribishe katika yule asiye na nyumba".

Alimshauri hivi mama mmoja kuhusu malezi ya binti yake: "Hakikisha kwamba kila siku asome sehemu fulani ya Maandiko… Baada ya sala, lifuate somo, na baada ya somo, ifuate sala… Badala ya vito na mavazi ya hariri, apende Vitabu vya Kimungu… Kumbuka kwamba utaweza kumlea kwa mfano wako kuliko kwa maneno".

Mashauri yake mengine yalikuwa haya: "Uyapende Maandiko matakatifu, na hekima itakupenda wewe; uyapende kwa dhati, nayo yatakulinda; uyaheshimu, nayo yatakubembeleza. Yawe kwako kama ushanga wako na hereni zako". "Upende elimu ya Maandiko, nawe hutapenda tamaa za mwili".

Vulgata, tafsiri ya kwanza ya Biblia nzima ya Kikristo katika Kilatini ndiyo kazi yake muhimu zaidi. Aliianza kwa agizo la Papa Damas I mwaka 382, akaiendeleza kwa miaka 23. Tafsiri hiyo ilipitishwa rasmi na mtaguso wa Trento kwa tamko la kuwa haipotoshi kamwe imani, nayo ilitumika kama msingi wa tafsiri nyingine nyingi hadi karne XX, ikiathiri sana ustaarabu wote wa Magharibi. Hata hivyo tangu mwanzo ilikosolewa sana kwa kufuata mno msimamo wa Kiyahudi. Ndiyo sababu Jeromu alitaka kukataa vitabu vya Deuterokanoni.

Pia alitafsiri vitabu vingine, alitunga hotuba, barua pamoja na vitabu juu ya maisha ya Wakristo watunzi maarufu zaidi ya 100 (yeye akiwa mmojawao) na ya wamonaki mbalimbali, akilinganisha safari zao za kiroho, na vitabu vya kutetea imani kwa kupinga mafundisho ya wazushi.


Vilevile alihimiza wamonaki kuelekea ukamilifu, akafundisha vijana elimu ya kiutu na ya Kikristo na kupokea katika hoteli maalumu waliohiji Nchi Takatifu ili wasikose mapokezi kama ilivyowatokea Yosefu na Maria.

Tangu zamani anaheshimiwa kama mtakatifu na babu wa Kanisa.

Mwaka 1298 Papa Bonifasi VIII alimuongezea sifa ya mwalimu wa Kanisa.

Sikukuu yake inaadhimishwa kila mwaka tarehe 30 Septemba.

## Augustino (354 - 430)



Augustino wa Hippo alikuwa mtawa, mwanateolojia na hatimaye askofu wa Hippo, leo Annaba, Algeria.

Augustino ndiye kiongozi mkuu wa Kanisa Katoliki katika Afrika Kaskazini Magharibi mwanzoni mwa karne V. Wakati ule Ukristo ulikuwa dini iliyokubaliwa tayari katika Dola la Roma; dhuluma dhidi ya Wakristo zilikuwa zimekwisha rasmi mwaka 313.

Wenyeji wa sehemu hizo walikuwa Waberberi kama mama yake, lakini watu wengi wa mjini, kama baba yake, na wenye mashamba makubwa walikuwa na asili ya Ulaya, wakitumia lugha ya Kilatini na kuwa na utamaduni wa Ulaya Magharibi.

Mama yake (Monika, anayeheshimiwa kama mtakatifu) alikuwa Mkristo, kumbe baba (Patrisi) alifuata dini ya jadi ya kuabudu miungu mingi kabla hajabatizwa mwishoni mwa maisha yake.

Augustino alizaliwa Thagaste, leo Souk Ahras nchini Algeria, tarehe 13 Novemba 354, akaitwa *Aurelius Augustinus*. Alikuwa na wadogo wawili, mmoja mwanamume, Naviji, na mwingine wa kike, ambaye hatujui jina lake, ila kwamba baada ya kufiwa mume wake akawa mmonaki na abesi.

Monika alimuathiri sana Augustino na kumlea katika imani ya Kikristo. Mwanae aliweza kuandika kwamba alipokuwa ananyonya maziwa ya mama, alifyonza pia upendo kwa jina la Yesu. Akiwa mtoto alipokea chumvi

kama ishara ya kuingia ukatekumeni akabaki daima anavutiwa na Yesu, hata alipozidi kusogea mbali na Kanisa lake.

Wakati wote wa ujana wake alifuata anasa na uzushi, bila kujali machozi ya mama yake. Alipata elimu yake nzuri ya lugha na ya ufasaha wa kuhubiri huko Thagaste, Madaura na hata katika Chuo Kikuu cha Karthago (karibu na Tunis), ingawa hakuwa daima mwanafunzi mzuri, mbali ya kuwa na akili ya pekee. Alimudu kikamilifu Kilatini, lakini si sana Kigiriki.

Akiwa huko Karthago, mwaka 373 alisoma kitabu cha maadili cha Sisero ambacho kilibadilisha hisia zake hivi kwamba "matumaini yote ya bure yakawa hayana maana kwangu, nikatamani hekima isiyokufa kwa ari isiyosemeka moyoni mwangu".

Lakini kwa kuamini ukweli haupatikani pasipo Yesu, ambaye hatajwi katika kitabu hicho, alianza kusoma Biblia, ila hakupenda tafsiri ya Kilatini wala yaliyomo akiyaona tofauti na mtindo wa falsafa inayotafuta ukweli. Hivyo alisogea mbali na dini iliyoonekana kutotia maanani hoja za akili ambayo pamoja na imani ndizo "nguvu mbili zinazotuongoza kwenye ujuzi". Ndivyo alivyoandika baadaye, akitoa pia kauli mbili za msingi kuhusu kulenga ukweli: "Usadiki ili uelewe", halafu "uelewe ili usadiki".

Hapo, kusudi asiishi bila Mungu, alijitafutia dini ya kuridhisha hamu yake ya kujua ukweli na ya kuwa karibu na Yesu, akajiunga kwa karibu miaka 10 na Umani. Dini hiyo ilidai kufuata akili na kufafanua sababu ya mabaya kuwepo duniani kutokana na chanzo cha pili cha ulimwengu kilicho kinyume cha Mungu, ikikataa Agano la Kale ili kufuata Ukristo wa kiroho.

Augustino alipenda pia maadili ya dini hiyo kwa sababu yalikuwa yanawadai sana baadhi ya waumini tu, yakiwaacha wengine wote wasijali zaidi. Hatimaye Wamani walikuwa wanasaidiana kupanda chati katika jamii. Lakini alipokutana na askofu wao Fausto, alikosa imani nao kwa kuona alivyoshindwa kujibu maswali yake.

Baada ya kumaliza masomo, alifundisha Kilatini huko Thagaste (374), halafu namna ya kuhubiri huko Karthago (375-383), akaendelea kufanya hivyo nchini Italia, kwanza Roma (384), halafu Milano (384-386), makao makuu ya Dola, alipopata kazi ya heshima sana.

Wakati huo wote aliishi bila ndoa na mwanamke aliyemzalia mtoto wa kiume mwenye akili sana, Adeodatus.

Akiwa Milano akakutana na watu, hasa askofu Ambrosi, waliomvuta awe Mkristo Mkatoliki. Mahubiri bora ya Ambrosi, aliyokwenda kuyasikiliza kwanza ili kuzidi kupata mbinu za kutoa hotuba, yalizidi kumgusa moyoni na kumfanya asadiki mamlaka ya Biblia nzima inavyosomwa rasmi na Kanisa. Aliona uzuri na udhati wa masimulizi ya Agano la Kale yakifafanuliwa kiroho kama mifano ya mambo ya Agano Jipya inayomuelekea Kristo, kiini cha yote. Katika barua za Mtume Paulo, Augustino alimtambua Kristo kama mwokozi, si mwalimu tu.

Hasa aliguswa na maneno ya Rom 13:13-14 aliyoyasoma kwa kufungua tu kitabu kisha kumsikia mtoto wa jirani akiimba kwa kukariri, "Chukua usome, chukua usome". Alitambua ameambiwa mwenyewe na Mungu maneno hayo yakimdai aachane na matendo ya mwili akamvae Kristo.

Kisha kuongoka hivyo tarehe 15 Agosti 386, akiwa na umri wa miaka 32, aliacha kufundisha na hata kuishi na mama mtoto, akatawa kwa muda huko Cassiciaco, karibu na ziwa la Como, akiwa na Monika, Adeodatus na marafiki wachache, halafu akarudi Milano alipobatizwa na Ambrosi pamoja na mwanae na rafiki yake Alipio usiku wa Pasaka ya mwaka 387.

Baada ya kubatizwa na kunuia akaishi kitawa Thagaste, alirudi Afrika; njiani, huko Ostia, bandari ya Roma, alifiwa mamaye. Ndoto yake ilikuwa kujitosa katika maisha ya sala na masomo pamoja na marafiki wake. Lakini hiyo ilidumu miaka mitatu tu.

Mwaka 391 bila kutarajia alipewa daraja ya upadri huko Hippo, alipoanzisha monasteri, akigawa muda wake kati ya sala, masomo na mahubiri, halafu mwaka 395 akachaguliwa kuwa askofu msaidizi wa mji huo na mwaka 397 akawa askofu wa jimbo hilo. Ilimbidi akubali matakwa ya Mungu kwake, kwamba ajitoe kwa wengine na kuwashirikisha ujuzi wake ili kuishi kweli kwa ajili ya Kristo. "Kuhubiri mfululizo, kujadili, kusisitiza, kujenga, kuwa tayari kwa yeyote ni jukumu kubwa sana, ni mzigo mzito, ni juhudi ya ajabu". Ilikuwa kama wongofu wake wa pili.

Hapo alitegemeza maskini na mayatima, alisimamia malezi ya wakleri, akiwadai waishi pamoja, akaeneza monasteri za kiume na za kike. Alifanya adhimisho la ekaristi kuwa kiini cha maisha ya jumuia zake.

Mahubiri yake mengi yanaonyesha alivyojua kujadiliana na umati akitumia maneno rahisi na ya kawaida na hata ucheshi katika kulinganisha Neno la Mungu na mazingira yao.

Kwa tabia yake karimu na pendevu, hisia zake, uvumilivu na utayari wa kusamehe alijifanyia marafiki hata maadui kadhaa.

Maisha yake ya Kiroho, yaliyoongoza uandishi wa kanuni yake kwa watawa, yamefuatwa na mashirika mengi ya kiume na ya kike hadi leo.

Kwa miaka 35 mpaka kifo chake, mbali ya kutimiza majukumu yake mengi, aliendelea kueleza na kutetea imani sahihi ya Kikristo kwa mahubiri, maandishi na vitabu vingi sana (hata vya mitindo mipya) dhidi ya aina zote za uzushi za wakati ule: Wamani, Wadonati, Wapelaji na Waario. Hivyo tangu alipokuwa hai, hakuongoza Kanisa la Afrika Kaskazini tu, bali alitegemeza imani kila mahali.

Kwa njia hiyo amekuwa mwalimu muhimu sana katika Ukristo, hasa wa Magharibi (yaani Kanisa Katoliki na Uprotestanti uliotokea katika Kanisa hilo. Kwa mfano Martin Luther alimtaja kuwa baba yake wa kiroho pamoja na Mtume Paulo). Augustino alijilisha tunu za Kikristo na kutokeza utajiri wake wa dhati, akibuni mawazo na mifumo ya kulisha vizazi vijavyo. Hata nakala za vitabu vyake ni nyingi sana, zikithibitisha vilivyopendwa na kuenea.

Hivyo aliathiri sana ustaarabu wa Magharibi unaozidi kuenea leo duniani kote. Mawazo yote yaliyomtangulia yanakutana katika maandishi yake na kuwa chemchemi ya mafundisho kwa nyakati zilizofuata.

Tarehe 26 Septemba 426 alikusanya waamini ili kuwatambulisha padri Eraklio aliyemchagua kama mwandamizi wake naye aweze kutumia miaka yake ya mwisho katika kusoma kwa dhati zaidi Maandiko matakatifu. Watu walimkubalia kwa shangwe.

Miaka minne iliyofuata Augustino alifanya kazi kubwa kwa kumaliza vitabu mbalimbali na kuanza kuandika vingine. Kati ya vile vya wakati huo kuna "Retractationes" (yaani "Kupitia Upya" vile vilivyotangulia), ambamo tunaona unyofu wake kwa kuwa tayari kurekebisha baadhi ya mafundisho aliyowahi kuyatoa. Hivyo mpaka mwisho alionyesha alivyolenga ukweli kuliko yote.

Pia miaka hiyo alijadiliana na wazushi hadharani na kurudisha amani iliyohatarishwa na makabila ya kusini yakifaidika na matatizo kati ya Kaisari na jemadari wake Bonifasi.

Alimuandikia mpatanishi: "Ni utukufu mkubwa zaidi kuzuia vita vyenyewe kwa neno moja, kuliko kuangamiza watu kwa upanga, na vilevile kusababisha au kudumisha amani kwa amani kuliko kwa vita. Kwa sababu wanaopigana, ikiwa ni watu wema, bila shaka wanalenga amani, ila kupitia damu. Kumbe kazi yako ni kuzuia umwagaji damu".

Hata hivyo, tumaini lilitoweka Bonifasi alipoalika kwa hasira washenzi wa Kijerumani walioitwa Wavandali kutoka Hispania wavamie Afrika.

Augustino aliaga dunia akiwa Hippo tarehe 28 Agosti 430 wakati Wavandali walipokaribia kuteka mji wake baada ya kuuzingira miezi mitatu, huku wakibomoa makanisa na nyumba za vijijini na kuua au kukimbiza wakazi, wakiwemo watawa. Baadhi waliteswa na kuchinjwa, wengine walibakwa au kufanywa watumwa.

Mbele ya maovu hayo yaliyokomesha ustaarabu wa Kirumi, Augustino alizidi kutafakari fumbo la Maongozi ya Mungu ili kujifariji na kuwatuliza wengine kama alivyofanya miaka 20 ya nyuma, Roma ilipotekwa kwa mara ya kwanza na Waostrogoti. Aliona ustaarabu huo ulikuwa umechakaa, kumbe Kristo tu hazeeki kamwe na ni wa kutegemewa.

Hapo awali, alidhani mtu akiongoka na kubatizwa atafikia kwa urahisi ukamilifu unaoelekezwa na Hotuba ya Mlimani. Miaka ya mwisho alikiri kwamba Yesu tu alitekeleza sawasawa hotuba yake hiyo. Waamini wanahitaji daima kuongoka na kutakaswa naye ili kufanywa wapya. "Nimeelewa kwamba mmoja tu ni mkamilifu kweli… Kumbe Kanisa lote - sisi sote, tukiwa pamoja na Mitume - tunapaswa kusali kila siku: 'Utusamehe dhambi zetu kama tunavyowasamehe na sisi waliotukosea'". Ndio wongofu wake wa tatu, uliomfanya amalizie maisha yake kwa unyenyekevu wa hali ya juu.

Katika ugonjwa wa mwisho aliomba Zaburi za toba ziandikwe kwa herufi kubwa na kubandikwa ukutani aweze kuzisoma kutoka kitandani huku akijiaminisha kwa Mungu kwa machozi mengi usiku na mchana.

Ili kujiandaa zaidi kufa, siku 10 za mwisho hakuruhusu mtu kumtembelea, ila waliomletea chakula na dawa.

Kutokana na maisha, mafundisho na maandiko yake bora tangu zamani anaheshimiwa kama mtakatifu na babu wa Kanisa.

Mwaka 1298 Papa Bonifasi VIII alimuongezea sifa ya mwalimu wa Kanisa.

Sikukuu yake inaadhimishwa kila mwaka tarehe 28 Agosti.

Katika historia yote Augustino ni kati ya watu wenye akili kubwa zaidi, iliyopenya masuala yoyote, pamoja na ubunifu wa ajabu na moyo mpana. Aliunda upya teolojia ya mapokeo akiitia chapa yake mwenyewe.

Kati ya mababu wa Kanisa, ndiye aliyetuachia maandishi mengi zaidi, kuanzia yale maarufu sana yanayoitwa "Maungamo", kwa kuwa humo miaka 397-400 aliungama sifa za Mungu na ukosefu wake mwenyewe kwa kusimulia alivyoishi hadi miaka ya kwanza baada ya kuongoka.

Kila wakati ulifurahia zaidi kitu fulani katika Augustino. Siku hizi anapendwa hasa kwa unyofu wake katika kujichunguza na kutoa siri zake, akikiri makosa yake na kuyageuza yawe sifa kwa Mungu.

Uzingatifu wake wa fumbo la nafsi yake, ambamo fumbo la Mungu limefichama, ni mzuri ajabu, kiasi cha kubaki hata leo kilele cha kujitafiti kiroho. Aliandika: "Usiende nje, rudi ndani mwako; ukweli unakaa katika utu wa ndani; na ukiona umbile lako ni geugeu, panda juu yako. Lakini kumbuka, unapopanda juu yako, unapanda juu ya roho inayofikiri. Basi, ufikie pale mwanga wa akili unapowaka". Tena: "Naona ni lazima wanadamu warudishiwe tumaini la kupata ukweli".

Posidi, mtu wa kwanza kuandika habari za maisha ya Augustino (kwa Kilatini, "Vita Augustini"), alisema, "waamini wanamkuta daima hai" katika vitabu vyake. Kweli havionyeshi imepita miaka 1600 tangu viandikwe: humo anaonekana kama rafiki yetu wa wakati huu anayesema nasi kwa imani isiyozeeka.

Augustino mwenyewe aliviorodhesha 1,030, ambavyo si vyote.

Kazi yake kubwa haikuwa kuandika maelezo juu ya vitabu na maneno ya Biblia yenyewe alivyofanya Origene, bali kuingiza Biblia katika mazingira ya kiroho, ya kijamii na ya kisiasa ya wakati wake.

Hapo aliuliza maswali na kutoa majibu yaliyo muhimu mpaka leo, akitegemea mamlaka ya imani inayodhihirishwa na Biblia, maandiko ya Kimungu yasiyoweza kukosea yakisomwa katika mapokeo ya Kanisa lililoorodhesha vitabu vinavyoiunda.

Akilinganisha imani na akili, Augustino alichunguza hasa fumbo la Mungu (Ukweli mkuu na Upendo wa milele, unaohitajiwa na roho ili kupata amani) na fumbo la binadamu (ambaye ni sura na mfano wa Mungu). Huyo, katika roho yake isiyokufa, bado ana uwezo wa kuinuka hadi kwa Mungu, ingawa uwezo huo umeharibiwa na dhambi na unahitaji kabisa kurekebishwa na neema.

Teolojia yake kuhusu Utatu inaendeleza ile ya mapokeo na kuathiri Kanisa lote la Magharibi. Augustino anaweka wazi kuwa Nafsi tatu ni sawa lakini hazichanganyikani; tena anajaribu kuufafanua Utatu kwa kutumia saikolojia (akitumia mfano wa kumbukumbu, akili na utashi). Kitabu muhimu zaidi kuhusu Utatu (kwa Kilatini kinaitwa "De Trinitate") alikiandika miaka 399-420. Kilichukua muda mrefu kwa kuwa alisimamisha uandishi wake miaka minane "kwa sababu ni kigumu mno na nadhani wachache tu wanaweza kukielewa; basi kuna haraka zaidi ya kuwa na vitabu vingine tunavyotumaini vitafaidisha wengi".

Hivyo alielekeza nguvu zake kutunga vitabu vya katekesi kwa wasio na elimu (hasa "De Catechizandis Rudibus"). Akijibu hoja za Wadonati, ambao walitaka Kanisa la Kiafrika na kuchukia mambo ya Kilatini, alikubali kurahisisha lugha hata kufanya makosa ya kisarufi kusudi wamuelewe zaidi akifafanua umoja wa Kanisa ulivyo muhimu kwa mahusiano na Mungu na kwa amani duniani.

Hasa hotuba zake, zilizoandikwa na wengine wakati alipokuwa anazitoa kwa watu akiongea nao kirahisi, zimechangia kueneza ujumbe wake. Tunazo bado karibu 600, lakini zilikuwa zaidi ya 3,000.

Pia alifafanua upya imani kuhusu umwilisho wa Mwana wa Mungu, akiwahi kutumia misamiati iliyokuja kupitishwa na Mtaguso wa Kalsedonia (451): uwepo wa hali mbili (ya Kimungu na ya kibinadamu) katika nafsi moja. Lengo la umwilisho lilikuwa wokovu wa watu, hivyo hakuna anayeweza kuokoka bila Kristo aliyejitoa sadaka kwa Baba, "akitakasa, akifuta na kutangua makosa yote ya binadamu, akiwakomboa kutoka mamlaka ya shetani".

Katika suala la neema ndiye aliyefundisha kwamba watu wote wamerithi kwa Adamu dhambi ya asili iliyopoteza uhuru wa asili, ila kwa neema yake Mungu hufunua upendo wake kwao. Alisisitiza kwamba si binadamu anayemtafuta Mungu, bali Mungu ndiye anayemhurumia mwanadamu mwenye dhambi. Utakaso unaopatikana kwa imani unasababisha ondoleo kamili la dhambi zote kabisa. Halafu mwamini anazidi kufanywa mpya kwa mchakato utakaokamilishwa na ufufuko wa siku ya mwisho.

Mchakato huo wote ni kazi ya neema ya Mungu: bila hiyo, binadamu hawezi kuongoka, kukwepa dhambi na kufikia utimilifu wa wokovu. Hayo yote ni zawadi tu ya Mungu, kama vilivyo pia udumifu na stahili za mtu.

Sisitizo hilo la kwamba neema ni dezo, lilimuongoza Augustino kufundisha juu ya uteule, neema ambayo hakuna anayeweza kuikataa na ambayo inafikisha kwa hakika mbinguni. Kwa nini Mungu hawapi wote neema hiyo ni fumbo ambalo tuliinamie tu, kwa sababu hatuwezi kabisa kulielewa. Kwa vyovyote haiwezekani kumlaumu Mungu kwa ajili hiyo, eti si haki.

Mawazo hayo yalizidi kukaziwa na watu kama Martin Luther, Yohane Calvin na Janseni, namna iliyokataliwa na Kanisa Katoliki.

Juu ya uhusiano kati ya serikali na Kanisa Augustino katika miaka 413-426 aliandika kitabu "De Civitate Dei" (maana yake kwa Kilatini ni: *Mji wa Mungu*) alimoeleza kuna "miji" miwili: mji wa Mungu (yaani Yerusalemu wa mbinguni, au Kanisa) na mji wa dunia hii, yaani taratibu za kisiasa.

Katika "mji wa dunia hii" hali hubadilika: hakuna taratibu za kudumu. Augustino alifahamu taratibu za Waroma Wapagani waliotazama Makaisari wao kuwa miungu, na vilevile habari za demokrasia ya Kigiriki ya kale. Alifahamu habari za jiji la Roma lililoitwa "mji wa milele" lakini katika siku zake lilichomwa moto na maadui jinsi ilivyoitokea zamani miji ya Babeli na Yerusalemu. Kumbe mji wa pili, “mji wa Mungu”, ni mji wa upendo na undugu wenye neema yake.

Miji yote miwili iko pamoja ingawa zina taratibu tofauti. Mkristo ni raia wa miji yote miwili. Huitwa kuwa mwaminifu pande zote mbili. Lakini ajue kwamba mji wa dunia hii hauna shabaha ya kudumu na umeingiliwa na dhambi. Mkristo anaweza kushiriki katika taratibu za kisiasa akijua kwamba mawazo na mipango yote ya siasa havidumu. Utakaodumu ni utaratibu wa Mungu tu. Kwa kuwa mji wa Mungu unashiriki enzi yake, inafaa serikali isikie mawazo ya Kanisa, ambalo kwa njia yake Mungu ameamua kufunua mapenzi yake.

Augustino alijua jinsi Kaisari Theodosi I alivyotubu kanisani baada ya askofu Ambrosi wa Milano kumtenga kwa sababu aliwatuza wanajeshi wa serikali yake walioua watu wengi ovyo walipotuliza fujo katika mji wa Thesalonike. Theodosi I alipotaka kuingia katika ibada, askofu huyo alimtangaza hawezi kushiriki meza ya Bwana. Ilimbidi Kaisari akubali kosa mbele ya umati. Viongozi wa Kanisa la Magharibi wakafuata mara nyingi mfano wa Ambrosi na mafundisho ya Augustino wakishika msimamo imara mbele ya serikali mbalimbali.

Kuna aina mbili za matokeo ya urithi huo ulioathiri maisha na fikra za Wakristo kwa karne nyingi za baadaye.

Kwa upande mmoja Kanisa lilijaribu kutawala jamii na serikali katika nchi za Ulaya. Lilidai sheria zote za serikali zifuate taratibu za Kanisa. Viongozi wa serikali walitakiwa kusimikwa na wale wa Kanisa. Hoja hiyo huitwa "Uklerikali". Nguvu ya kisiasa ya Kanisa ilifikia kilele chake mwanzoni mwa karne XIII wakati wa Papa Inosenti III, halafu ilizidi kupungua hadi kupingwa kabisa na mapinduzi mbalimbali ya Ulaya na Amerika (kuanzia mapinduzi ya Ufaransa, mwaka 1789). Siku hizi wazo hili halipo tena lakini zamani lilileta matatizo mengi, kama vile ugandamizaji wa madhehebu yaliyokuwa tofauti na yale ya mtawala, na hata vita vya kidini.

Augustino aliingiza pia hoja ya "vita halali" katika Ukristo uliowahi kukataa ukatili na vita kama dhambi dhidi ya Mungu. Yeye alieleza kwamba wakati mwingine vita ni halali, na kama ni halali ni wajibu wa Mkristo pia. Maelezo hayo yalitumiwa baadaye na watawala na wanasiasa Wakristo kwa kutetea vita vya kila aina.

Lakini pia sehemu nyingine ya urithi huo imebaki, yaani kazi ya Kanisa ya kuzitetea haki za binadamu hata dhidi ya serikali inayoweza kuzigandamiza. Kwa mfano Wakristo walipinga sana siasa ya ubaguzi wa rangi Marekani na Afrika Kusini dhidi ya serikali zilizoutetea. Vilevile ndio wanaotetea haki za wakimbizi katika nchi nyingi hata kama serikali zimeshachoka mzigo wa kupokea wageni maskini kutoka nchi jirani.

### Kwa Kiswahili


MT. AUGUSTINO, Kanuni – tafsiri ya Mapadri Waaugustino – ed. Benedictine Publications Ndanda Peramiho – Peramiho 1992 – ISBN 9976-67-059-1

M. CULLEN, O.S.A., Maungamo ya Mtakatifu Augustino kwa Muhtasari – tafsiri ya E. Msigala, O.S.A. - ed. Benedictine Publications Ndanda Peramiho – Ndanda – ISBN 9976-63-643-1

M. CULLEN, O.S.A., Mtakatifu Monika: Mlinzi wa Akina Mama Wakristu – tafsiri ya E. Msigala, O.S.A. - ed. Benedictine Publications Ndanda Peramiho – Ndanda 2002 – ISBN 9976-63-641-5


## Sirili wa Aleksandria (370 hivi - 444)



Sirili wa Aleksandria alikuwa Patriarki wa jiji hilo la Misri (kuanzia tarehe 18 Oktoba 412 hadi kifo chake) na mwanateolojia.

Alishiriki mabishano ya karne IV kuhusu imani juu ya Yesu Kristo, akitetea dogma ya umoja wa Nafsi yake ya Kimungu kwa kutegemea daima mapokeo ya Kanisa na mamlaka ya mababu waliomtangulia, hasa Atanasi. Kwa ajili hiyo aliitwa "mlinzi wa usahihi" (wa imani).

Mtu wa hamaki na mwenye uwezo wa kufanikisha mambo yoyote, ni maarufu hasa kwa kumkomesha Nestori wa Konstantinopoli katika Mtaguso wa Efeso (431) uliomtangaza Bikira Maria kuwa Mama wa Mungu. Vilevile alikuwa mkali dhidi ya wazushi wengine, Wayahudi na Wapagani, na hata dhidi ya Yohane Krisostomo.

Kwa hakika ulikuwa wakati mgumu ambapo ukweli uliweza kushinda uzushi kutokana tu na wachungaji wenye msimamo mkali katika kulinda kundi la waamini walilokabidhiwa.

Sirili alizaliwa huko Theodosios, karibu na El-Mahalla El-Kubra ya leo, Misri, mwaka 370 hivi,

Miaka michache baadaye, mjomba wake Theofilo wa Aleksandria alipata kuwa Patriarki wa Aleksandria. Mama alibaki karibu na kaka yake, hivyo mtoto alipata malezi mazuri na elimu sanifu ya wakati ule: lugha (390-392), fasihi (393-397) hatimaye teolojia na Biblia (398-402).

Mwaka 403 alitumwa Konstantinopoli kushiriki "Sinodi ya Mwaloni" iliyomuondosha Patriarki wa mji huo, Yohane Krisostomo, na kulipatia Kanisa la Aleksandria kwa mpigo mmoja ushindi dhidi ya wapinzani wake wote wawili, Antiokia na Konstantinopoli.

Theofilo alipofariki tarehe 15 Oktoba 412, kisha kuongoza Kanisa la Misri kwa nguvu sana miaka 27, Sirili alichaguliwa Patriarki wa Aleksandria baada ya siku tatu.

Akitumia mamlaka yake katika jiji hilo lenye ushindani na fujo, alifunga makanisa ya Wanovasyani na kufukuza Wayahudi wengi.

Pia alitetea kwa nguvu msimamo wa teolojia ya Shule ya Aleksandria dhidi ya ile ya Antiokia na haki ya Kanisa la Aleksandria kuwa la pili duniani (baada ya Kanisa la Roma) na la kwanza Mashariki kote dhidi ya Kanisa la Konstantinopoli lililopendelewa na Mtaguso I wa Konstantinopoli (381). Hata hivyo mwaka 417 au 418 alikubali kurudhisha ushirika nalo ulilovunjika mwaka 406, Yohane Krisostomo alipofukuzwa moja kwa moja.

Ushindani huo ulikomaa tena mwaka 428 alipochaguliwa kuwa Patriarki wa Konstantinopoli mmonaki mkali Nestori, mwenyeji wa Antiokia kama Yohane huyo. Sirili alipata nguvu dhidi yake pale ambapo padri wa Antiokia alianza kuhubiri huko Konstantinopoli kwamba Bikira Maria hastahili kuitwa "Mama wa Mungu", ila "Mama wa Kristo". Waamini walipomshtaki kwa Nestori, huyo akamtetea kwa msingi wa teolojia ya Antiokia iliyosisitiza ukweli wa ubinadamu wa Yesu.

Kwenye Pasaka 429, Sirili aliwaandikia wamonaki barua dhidi ya Nestori ikitetea teolojia ya Aleksandria iliyosisitiza ukweli wa umungu wa Yesu. Nakala ilipofika Konstantinopoli, Nestori alihubiri dhidi yake. Ndio mwanzo wa mawasiliano makali kwa njia ya barua yaliyozidisha ushindani kati ya wanateolojia wa miji hiyo miwili.

Hali hiyo iliwafanya wote wawili wamuombe Papa Selestini I aingilie kati. Hapo sinodi iliyofanyika Roma mwaka 430 ilikubali hoja za Sirili dhidi ya Nestori.

Ili kumaliza mabishano hayo ya hatari, Kaisari Theodosi II aliitisha mtaguso mkuu huko Efeso, palipokuwa upande wa Sirili, ambaye alifungua na kufunga Mtaguso wa Efeso (431) kabla Nestori na wafuasi wake hawajafika; hivyo, mtaguso uliagiza Nestori aondoshwe madarakani na kupelekwa uhamishoni.

Lakini Yohane wa Antiokia na wengine wa upande wa Nestori walipofika Efeso siku nne baadaye, walifanya mtaguso wa kwao wakimhukumu Sirili kuwa mzushi, wakidai aondoshwe madarakani.

Hapo Theodosi II aliamua kuwaondosha na kuwafunga wote wawili; hivyo alimkamata Sirili, lakini huyo alikimbilia Misri akaleta fujo hadi kwenye ikulu, hata Kaisari alikubali kumfukuza Nestori arudi monasterini Antiokia. Matukio hayo ndiyo chanzo cha farakano la Waashuru linalodumu hadi leo.

Ili azidi kudhoofisha uzushi huo, Sirili alipata itolewe hukumu dhidi ya Theodori wa Mopsuestia, aliyewahi kuwa mwalimu wa Nestori, lakini baadaye mwenyewe akailaumu hukumu hiyo.

Hivyo, mwaka 433 alikubali kuafikiana na wafuasi wa teolojia ya Antiokia na kupatana nao.

Sirili aliandika sana: kwanza dhidi ya Waario, ila baada ya mwaka 428 alilenga Unestori. Aliandika vitabu mbalimbali vya ufafanuzi wa Agano la Kale (Torati nzima, Isaya na Zaburi) na Agano Jipya (Injili ya Yohane na ile ya Luka) na vya teolojia, pamoja na nyaraka rasmi kwa ajili ya Pasaka, hotuba na barua. Vitabu hivyo vilienea mapema wakati wa maisha yake hata katika tafsiri mbalimbali.

Katika kutetea msimamo wake, pamoja na shuhuda za Biblia, alitumia kuliko wote waliomtangulia zile za mababu wa Kanisa, na hata hoja za akili.

Pamoja na hayo, aliona imani ya Taifa la Mungu, yaani waamini wa kawaida, kama tokeo la mapokeo na hakika ya mafundisho sahihi: "Ni lazima tufafanue kwa watu mafundisho na maelezo ya imani namna isiyolaumika kabisa, na tukumbuke kwamba anayekwaza hata mmoja tu kati ya wadogo wanaomuamini Kristo atapatwa na adhabu isiyovumilika".

Mwanzoni alifundisha juu ya Yesu kwa kumuiga Atanasi, lakini alipozidi kubishana na Nestori alilazimika kutumia misamiati mipya iliyoelekea kukiri uwemo wa hali mbili ndani ya Kristo. Kwa hiyo katika barua yake ya pili kwa Nestori, iliyokuja kupitishwa na Mtaguso wa Kalsedonia (451), aliweka wazi: "Hivyo sisi tunatamka kwamba hali zilizounganika katika umoja wa kweli ni tofauti, bali kutoka zote mbili amepatikana Kristo na Mwana mmoja tu; si kwa sababu tofauti za hali hizo zimefutwa na umoja wake, bali kwa sababu umungu na ubinadamu, vilivyounganika katika umoja usiosemeka wala kufafanulika, vimetupatia Bwana, Kristo na Mwana mmoja".

Katika barua nyingine aliandika, "Mwana ni mmoja tu, Bwana Yesu Kristo ni mmoja tu, kabla ya umwilisho wake na baada ya umwilisho vilevile. Kwa kuwa Neno aliyezaliwa na Mungu Baba hakuwa Mwana mmoja na aliyezaliwa na Bikira Maria mwingine; bali tunasadiki kwamba yuleyule aliyezaliwa kabla ya nyakati ndiye aliyezaliwa pia kimwili na mwanamke".

Sirili alifariki Aleksandria mwaka 444, lakini mashindano yaliendelea hadi Mtaguso wa Kalsedonia na mbele zaidi.

Tangu zamani anaheshimiwa kama mtakatifu na babu wa Kanisa.

Mwaka 1883 Papa Leo XIII alimuongezea sifa ya mwalimu wa Kanisa.

Sikukuu yake inaadhimishwa kila mwaka tarehe 27 Juni.

## Petro Krisologo (380 hivi - 450 hivi)



Petro Krisologo alikuwa askofu mkuu wa Ravenna (wakati huo mji mkuu wa mwisho wa Dola la Roma la Magharibi, leo katika mkoa wa Emilia-Romagna huko Italia Kaskazini) aliyevutia umati wa watu kwenye imani kwa mafundisho yake yaliyo bora kwa hekima na ufasaha wa lugha.

Habari za maisha yake ni chache, tena si za hakika. Alichoandika Agnus, mwanahistoria wa Ravenna, mwaka 840 hivi, si cha kuaminika sana.

Petro alizaliwa huko Forum Cornelii, leo Imola, Italia, mwaka 380 hivi**.**

Alivyosimulia mwenyewe, alipewa ubatizo, malezi ya kidunia na ya kiroho na hatimaye daraja takatifu ya ushemasi na Korneli, askofu wa Imola.

Papa Sisto III (au Selestino I) alimteua kuwa askofu wa Ravenna mwaka 433. Chini yake Kanisa la mji huo lilipewa baadhi ya haki za jimbo kuu, kwa sababu ya kuwepo ikulu ya Dola. Muhimu zaidi, lilipata sifa kutokana na uchungaji wa Petro mwenyewe, mwenye ari pande zote, unaoshuhudiwa na hotuba zake nyingi.

Tunazo 183, hasa za kufafanulia Biblia na za kumsifu Bikira Maria na Yohane Mbatizaji.

Hotuba ya kwanza jimboni aliitoa mbele ya Gala Plasidia, binti wa Kaisari Theodosi I, ambaye baadaye akawa mtawala wa dola kwa niaba ya mwanae Kaisari Valentiniani III. Akishirikiana na malkia huyo mwenye imani, Petro alihamasisha ujenzi wa makanisa mazuri ajabu, hivi kwamba alipofariki yeye Ravenna, ambayo miongo michache ya nyuma ilikuwa kijiji kwenye madimbwi, iliweza kushindana na Konstantinopoli kwa mabasilika, vikanisa na monasteri, mbali na majumba.

Ni kati ya wachungaji bora wa wakati ule, akitekeleza mwenyewe kipeo cha askofu alichokichora hivi: “Kuwa ndani ya Kristo mtumishi huru wa wote”.

Uadilifu na ari yake vilimvutia waamini wengi waliomuita *Krisologo* (kutoka Kigiriki, "Neno la dhahabu") kwa sababu ya mvuto wa kiroho na ufasaha wa mahubiri yake.

Petro alifafanua vizuri hasa fumbo la umwilisho na Kanuni ya Imani ya Mitume, akipinga uzushi wa Ario na ule wa Eutike. Alimuandikia huyo mwaka 449 ili akubali maamuzi ya Papa Leo I: “… kwa sababu mwenye heri Petro, ambaye anaishi na kuongoza akiwa katika ukulu wake mwenyewe, anawapa ukweli kuhusu imani wale wanaoutafuta”.

Alifariki katika mji wake wa kuzaliwa tarehe 2 Desemba 450.

Tangu zamani anaheshimiwa kama mtakatifu na babu wa Kanisa.

Mwaka 1729 Papa Benedikto XIII alimuongezea sifa ya mwalimu wa Kanisa.

Sikukuu yake inaadhimishwa kila mwaka tarehe 30 Julai.

## Leo Mkuu (400 hivi - 461)



Leo I alikuwa Papa kwa miaka 21, kuanzia 29 Septemba 440 hadi kifo chake, wakati usalama wa Roma ulikuwa unatishwa na makabila yasiyostaarabika. Alimfuata Papa Sisto III. Jina lake la kuzaliwa pia lilikuwa Leo.

Ndiye Papa wa kwanza kuitwa "Mkuu" kutokana na mchango mkubwa alioutoa upande wa dini na wa siasa vilevile, akiwajibika kuhudumia taifa la Mungu kwa kila namna. Ni kati ya Mapapa bora waliolipatia Kanisa la Roma sifa na kuliimarishia mamlaka yake wakati ambapo ile ya serikali ya jiji hilo ilikuwa inafifia zaidi na zaidi.

Alizaliwa na familia ya kisharifu ama Roma ama katika mkoa wa Toscana (Italia ya kati) mwaka 400 hivi.

Kutokana na umaarufu wake, mwaka 431, akiwa shemasi tu, pengine aliandikiwa na Sirili wa Aleksandria ili amuunge mkono dhidi ya Juvenali wa Yerusalemu. Wakati huohuo Yohane Kasiano alimuandikia kitabu dhidi ya Nestori wa Konstantinopoli. Hasa malkia wa Magharibi alimteua kuwapatanisha maofisa wakuu wa Galia (leo Ufaransa).

Akiwa huko, Papa Sisto III alifariki (11 Agosti 440), na Leo alichaguliwa na umati kwa kauli moja kushika nafasi yake. Tarehe 29 Septemba alianza kazi yake kama Papa ambayo ilichangia sana kukusanya mamlaka ya Kanisa lote katika jimbo la Roma, aliloliunda upya pamoja na majimbo mengine ya Italia.

Ili kuimarisha nafasi hiyo ya Kanisa pekee la Magharibi lililoanzishwa na mitume wenyewe, alijitafutia hati maalumu kwa Kaisari Valentiniano II. Hiyo haikupendeza Wakristo wa Mashariki.

Nafasi bora ya kusisitiza kwa busara mamlaka hiyo hata upande huo wa pili wa Dola la Roma ilitolewa na mabishano kuhusu nafsi ya Yesu Kristo yaliyosababishwa na Eutike kukanusha ubinadamu halisi wa Kristo. Katika waraka maarufu aliomuandikia Patriarki Flavianus wa Konstantinopoli (449) ili kumuangalisha kuhusu uzushi wa mtu huyo, Leo alifafanua wazi namna umungu na utu wa Kristo yanavyounganika katika nafsi yake.

Hata hivyo mwaka huohuo mtaguso unaojulikana kama Wizi wa Efeso ulipuuzia waraka huo usisomwe, ukamtetea Eutike. Hapo Leo akashika uongozi wa mapambano dhidi yake.

Mwaka 451 katika Mtaguso wa Kalsedonia, baada ya barua yake kwa Flavianus kusomwa, maaskofu wote 350 walisimama na kulia: "Ndiyo imani ya mababu... Mtume Petro amesema kwa njia ya Leo..." Hivyo ilithibitishwa imani katika hali mbili za Kristo zisizochanganyikana wala kutenganika.

Pamoja na hayo, mabalozi wa Leo hawakuwekwa kati ya viongozi wa mtaguso, na kanuni ya 28 ilidai Kanisa la Konstantinopoli kuwa muhimu sawa na la Roma. Kwa hiyo Leo aliikataa, akisisitiza nafasi ya kwanza ya Roma ili kudumisha umoja hasa katika kipindi hicho cha fujo.

Vilevile, Leo alipambana kwa nguvu na Wapelaji, Wamani na Waprishila, akitetea daima imani kadiri ya mapokeo ya mitume; vilevile alipambana na ushirikina wa Wapagani.

Wakati Dola la Roma lilipokuwa likisambaratika, Leo alipata umaarufu pia kwa kutumia mamlaka yake ya kiroho tu ili kuzuia uvamizi wa Roma uliohofiwa kufanywa na Atila, mfalme wa Wauni (452) na ili kupunguza madhara ya ule uliofanywa na Wavandali kwa wiki mbili (455). Tena alistawisha matendo ya huruma mjini kwa waliopatwa na njaa, dhuluma na ufukara, kama vile umati wa wakimbizi.

Leo aliunganisha vizuri ajabu unyenyekevu wake mwenyewe na hakika ya ukuu wa cheo chake kama mwandamizi wa Mtume Petro, akiingilia kati masuala mbalimbali magharibi na mashariki vilevile kwa njia ya barua na ya mabalozi wake.

Umuhimu wa Upapa wa Leo, ambao ulidumu muda mrefu kuliko Mapapa karibu wote, ni katika kusisitiza hata kwa madondoo ya Biblia mamlaka ya pekee ambayo Kanisa la Roma linayo juu ya makanisa yote duniani kutokana na Mtume Petro kuwekwa na Kristo na kufia Roma walipo waandamizi wake. Ndilo fundisho linalojitokeza mfululizo katika barua zake 143 na hasa katika hotuba 96 zilizopo hata leo.

Humo unajitokeza utajiri na uwazi wa mafundisho aliyoyatoa kwa lugha sahili na safi. Ndio mkusanyo wa kwanza wa hotuba za Kipapa zilizochangia sana ustawi wa Kanisa baadaye.

Aliunganisha matendo ya ibada na maisha ya kila siku ya Wakristo, k.mf. saumu na matendo ya huruma. Alionyesha kuwa liturujia ya Kikristo si kumbukumbu ya matukio yaliyopita, bali utimiaji wa mambo yasiyoonekana katika maisha ya kila mmoja. Hivyo ni lazima Pasaka iadhimishwe kila wakati wa mwaka, "si kama jambo la zamani, bali kama tukio la leo". Hata siku hizi Liturujia ya Roma inazidi kutumia matini yake mengi na kufuata mtindo wake bora katika sala.

Tangu zamani anaheshimiwa kama mtakatifu na babu wa Kanisa.

Mwaka 1754 Papa Benedikto XIV alimuongezea sifa ya mwalimu wa Kanisa.

Sikukuu yake inaadhimishwa kila mwaka tarehe 10 Novemba, siku aliyofariki Roma mwaka 461.

## Gregori Mkuu (540 hivi - 604)



Gregori I alikuwa Papa kuanzia 3 Septemba 590 hadi kifo chake.

Jina lake la kuzaliwa pia lilikuwa Gregorius. Kutokana na umuhimu wake katika historia, hasa ya Kanisa na ya Italia, aliongezewa lile la Magnus, yaani "Mkuu".

Lakini mwenyewe, aliposikia kuwa Patriarki wa Konstantinopoli alijiita "Patriarki wa ekumene" (yaani wa kimataifa), aliitikia kwa kujiita "Servus servorum Dei" (yaani "Mtumishi wa watumishi wa Mungu"), jina linalotumiwa na Mapapa hata leo. Akijali umoja wa kidugu katika Kanisa lote, aliona unyenyekevu unatakiwa kuwa adili la msingi la kila askofu kama lilivyokuwa kwa Kristo aliyetuosha miguu. Jina hilo alilojichagulia lilidhihirisha kabisa namna yake ya kuishi na kutenda. Hamu yake ilikuwa kuishi kama mmonaki, akizama daima katika Neno la Mungu, lakini kwa kumpenda yeye alijifunza kuwa mtumishi wa wote katika nyakati za tabu.

Gregori alizaliwa Roma, Italia mwaka 540 hivi katika familia ya ukoo maarufu wa Anici, akiwa mtoto wa seneta Gordianus na wa Silvia, ambao wanaheshimiwa kama watakatifu. Shangazi zake Emiliana na Tarsila, wakiishi nyumbani mwao kwa sala na toba kama mabikira wa Kristo, walimtia pia hisia za Kikristo kweli. Kati ya mababu wake kulikuwa na Papa Felisi II (483-492) na Papa Agapito I (535-536).

Alipokuwa na umri wa miaka 25 tu alifuata nyayo za baba yake katika shughuli za utawala na mwaka 572 alichaguliwa kuwa mkuu wa jiji la Roma. Kutokana na ugumu wa nyakati hizo, kazi hiyo ilimdai awajibike katika masuala mengi tofauti ikimuandaa kwa majukumu yake ya baadaye.

Kwa namna ya pekee alidumisha hisi ya kuwepo haja ya utaratibu na nidhamu katika mambo yote. Ndiyo sababu baadaye, akiwa Papa, alihimiza maaskofu waendeshe shughuli zao kwa kufuata mfano wa uwajibikaji na utekelezaji wa sheria wa watawala wa kisiasa.

Hata hivyo maisha hayo hayakuweza kumridhisha. Kwa hiyo, baada ya muda mfupi aliyaacha, na akivutiwa na mfano wa Benedikto wa Nursia, aligeuza nyumba yake mjini kuwa monasteri na kujifanya mmonaki, halafu akajitahidi katika maisha ya sala na kutafakari Biblia na maandishi ya mababu wa Kanisa. Pia alianzisha monasteri 6 katika kisiwa cha Sisilia. Maisha hayo ya kuhusiana na Bwana tu yalimuandaa kutoa mafundisho yake bora na yalizidi kumvutia hadi mwisho, kama alivyoandika mara nyingi baadaye.

Lakini mapema, kutokana na sifa na mang'amuzi yake, Papa Pelaji II alimfanya shemasi akamtuma kama balozi wake kwenye ikulu ya Konstantinopoli, alipobaki miaka sita akiendelea kuishi kimonaki na wenzake kadhaa kati ya fahari za mazingira ya Kikaisari. Majukumu yake makuu yalikuwa kukomesha mabaki ya mabishano kuhusu ubinadamu wa Kristo na hasa kupata msaada wa Kaisari dhidi ya uvamizi wa Walombardi nchini Italia. Hata miaka hiyo ilimuandaa kwa kazi zake za baadaye.

Aliporudi Roma, mwaka 586, akarejea monasterini, lakini Papa huyohuyo alimfanya katibu wake. Ilikuwa miaka migumu kwa mvua za mfululizo, mafuriko na njaa mjini Roma na sehemu mbalimbali za Italia. Hatimaye tauni ilifyeka watu wengi, Pelaji II akiwa mmojawao.

Hivyo tarehe 3 Septemba 590 alishangiliwa na wakleri, maseneta na umati wa watu kwa kauli moja awe Papa wa 64. Ndiye mmonaki wa kwanza kufikia Upapa, ingawa hakutaka, hata akajaribu kukimbia, lakini bure. Ilimbidi akubali mapenzi ya Mungu, akaanza mara kuwajibika.

Mapema alionekana kuwa na mitazamo na maamuzi sahihi na kujitokeza kama mtendaji bora upande wa Kanisa na hata upande wa jamii na siasa (kwa sababu hiyo aliitwa "Mrumi wa mwisho"), ingawa alikuwa na afya mbovu, kiasi cha kulazimika mwishoni kubaki kitandani kwa siku kadhaa. Hasa mafungo makali ya kimonaki yalikuwa yamesababisha matatizo makubwa ya tumbo.

Tena sauti yake ilikuwa ndogo kiasi kwamba mara nyingi ilimbidi kumpa shemasi kazi ya kutangaza hotuba yake alipoendesha ibada makanisani kati ya waumini waliomheshimu sana kwa kuona anawafanya wajisikie salama. Hotuba hizo zinaonyesha alivyotekeleza alichoandika: "Ni lazima mhubiri achovye kalamu yake katika damu ya moyo wake; hapo ataweza kufikia masikio ya majirani wake".

Aliwasiliana na viongozi wa nchi mbalimbali za Ulaya, na hasa wa kabila la Wafaranki ambalo lilikuwa la kwanza kati ya yale ya Kijerumani kuingia Ukatoliki moja kwa moja tena lilijitokeza lenye nguvu kuliko yote.

Vilevile alifanikisha uongofu wa makabila ya aina hiyo yaliyoteka Uingereza, alipomtuma kama mmisionari Augustino wa Canterbury, priori wa monasteri yake ya Mt. Andrea.

Alilinda pia Roma dhidi ya uvamizi wa Agilulf, mfalme wa Walombardi, lakini, kinyume na Kaisari aliyewaona ni washenzi na wavamizi tu ambao wadhibitiwe au kuangamizwa, Gregori, kwa mtazamo wa kichungaji, alijenga nao uhusiano mpya ili kuwaleta kwenye Kanisa Katoliki kutoka uzushi wa Ario, kama alivyofanya pia na Wavisigoti wa Hispania na wale walioendelea kufuata dini za jadi.

Akilenga amani ya kudumu nchini Italia, kwa msaada wa Theodolinda, malkia Mkatoliki wa Walombardi, alifanikiwa kwanza kusimamisha mapigano na kabila hilo kwa miaka mitatu (598-601), na kuanzia mwaka 603 kwa muda mrefu zaidi.

Lakini mafanikio yake hayo, yaliyoandaa mengine kwa siku za mbele, yalimfanya achukiwe na watu wa Konstantinopoli.

Alipambana na matatizo mengine ya Italia, kama vile mafuriko, njaa, tauni, akisimamia kwa usawa masuala ya kijamii yaliyopuuziwa na wawakilishi wa Kaisari. Kwa mapato ya mali ya Kanisa, aliyoisimamia vizuri na kwa kuzingatia haki, kati ya mambo mengine alilisha wenye njaa na kukomboa watumwa. Alishughulikia hata huduma ya maji. Alirekebisha liturujia ya Kiroma, akipanga matini ya zamani na kutunga mengine mapya, pamoja na kushughulikia muziki wa ibada za Kilatini ambao kwa heshima yake unaitwa wa Kigregori.

Vitabu vyake, hasa vya maadili na vya ufafanuzi wa Maandiko matakatifu unaolenga utekelezaji, barua 848 zilizotufikia pamoja na hotuba mbalimbali vinashuhudia kazi zake nyingi na ujuzi wake wa Biblia.

Pia aliandika maisha ya watakatifu kadhaa wa Italia walioishi si zamani sana, kama vile Benedikto wa Nursia ambaye tunamfahamu kwa njia hiyo tu. Ni kwamba rafiki yake, Petro shemasi, alidhani wakati ule maadili yameharibika kiasi cha kuzuia upatikanaji wa watakatifu wapya kama walivyotokea zamani. Basi, Gregori alimuonyesha kwamba, kinyume chake, utakatifu unawezekana daima, hata katika mazingira magumu. Masimulizi ya maisha yao yanaendana na hoja za kiteolojia zinazofafanua masuala mbalimbali.

Kitabu kingine kilichoacha athari kubwa ni "Mwongozo wa Kichungaji" kwa ajili ya maaskofu, ambao ulitafsiriwa mapema hata kwa Kigiriki na kwa Kisaksoni. Alikiandika mwanzoni mwa Upapa wake akautekeleza mwenyewe. Humo anasisitiza ukuu wa cheo hicho na majukumu yanayoendana nacho, ambayo yanadai askofu awe kielelezo kwa wote. Kwa ajili hiyo anapitia kwa makini aina mbalimbali za waumini na saikolojia zao ili kuonyesha namna ya kuwasaidia. Hatimaye anakazia unyenyekevu wa kutojiona sawa mbele ya Hakimu mkuu kutokana na mafanikio fulanifulani: "Mtu anaporidhika kwa kutimiza maadili mengi, ni vema afikirie mapungufu yake na kujinyenyekesha: badala ya kuzingatia mema aliyofanya, ni lazima azingatie yasiyofanyika". Kwake uchungaji ni "ars artium", yaani sanaa kuu kuliko zote.

Katika maandishi yake, hakukusudia kamwe kutoa mafundisho mapya, bali kuwa mwangwi mnyenyekevu wa mapokeo ya Kanisa. Alieneza mafundisho ya Augustino, akisisitiza kama yeye hali ya dhambi ya binadamu, nafasi ya kwanza ya neema katika wokovu pamoja na imani katika uteuzi wa watakaookoka uliofanywa na Mungu. Pia alichangia ustawi wa fundisho la uwepo wa toharani.

Mtu huyo alikuwa wa ajabu kuliko kazi zake, akivutia kwa nguvu na upendevu wa tabia. Ndani mwake upana wa moyo na roho ya Kikristo vilitegemeza yote.

Inawezekana kusema ndiye Papa wa kwanza kutumia mamlaka upande wa siasa pia, lakini bila kuweka pembeni majukumu yake ya kiroho: yeye alifanya hivyo kama mtu aliyeungana kweli na Mungu na hivyo aliweza kuona la kufanya. Kwake ilikuwa muhimu kila mmoja atafakari matukio ya maisha katika mwanga wa Neno lake kwa sababu historia ya wokovu haikumalizika zamani, bali inaendelea moja kwa moja hata katika nyakati ngumu kama zile alizozipitia mwenyewe.

Alifariki Roma tarehe 12 Machi 604.

Tangu zamani anaheshimiwa kama mtakatifu na babu wa Kanisa.

Mwaka 1298 Papa Bonifasi VIII alimuongezea sifa ya mwalimu wa Kanisa.

Sikukuu yake inaadhimishwa kila mwaka tarehe 3 Septemba, siku aliyochaguliwa kuwa Papa.

## Isidori wa Sevilia (560 - 636)



Isidori alikuwa askofu mkuu wa Sevilia, maarufu kwa elimu yake kubwa aliyowarithisha hasa watu wa Ulaya Magharibi wa Karne za Kati.

Alizaliwa na Severianus na Turtura huko Cartagena, Hispania, mwaka 560, akiwa wa nne kati ya watoto watano, ambao wanne kati yao wanaheshimiwa na Kanisa Katoliki kama watakatifu: Leandro wa Sevilia, Fulgensi, Florentina wa Cartagena naye mwenyewe. Kati yao, watatu walikuwa maaskofu, na wa kike alikuwa mtawa.

Kaka yake, Leandro, msomi aliyeshika maisha magumu, ndiye aliyemlea kwa nidhamu kubwa baada ya kifo cha baba yao, akimtengenezea mazingira ya kimonaki ambamo awajibike katika masomo akitumia maktaba yao kubwa ili kujiandaa akabili matatizo ya wakati ule.

Kutokana na matatizo hayo, akiwa bado mtoto ilimbidi aonje uchungu wa kupelekwa uhamishoni. Hata hivyo alichangamkia utume wake wa kurudisha katika Kanisa Katoliki na ustaarabu wa Kirumi nchi yao iliyotekwa na Wavisigoti Waario.

Kisha kuwa mkleri huko Sevilia, mwaka 599 Isidori alimrithi Leandro kama askofu wa jimbo kuu hilo akaliongoza kwa miaka 37, akijitahidi pande zote: katika teolojia, liturujia, sheria za Kanisa n.k.

Kama rafiki yake Gregori Mkuu, ilimbidi Isidori pia asifuate elekeo lake la kujisomea bali ajitose kwa upendo kushughulikia wokovu wa watu wake. Ndivyo alivyoandika: "Mtu wa Kanisa upande mmoja anatakiwa kuwa amesulubiwa kwa ulimwengu kwa kufisha mwili wake, upande mwingine anatakiwa kukubali uamuzi wa Kikanisa - unapotokana na mapenzi ya Mungu - wa kuwa awajibike kwa unyenyekevu kutawala, hata asipotaka… Kwa kuwa watakatifu hawatamani kushughulikia mambo ya dunia na wanaugua kwa ndani pale ambapo kwa mpango wa fumbo wa Mungu wanabebeshwa majukumu kadhaa… Wanafanya wanachoweza ili

kuyakataa lakini wanakubali kile walichotaka kutupa na wanafanya walichopendelea kukwepa. Kwa sababu wanaingia dhati ya moyo na humo wanatafuta kujua utashi wa fumbo wa Mungu unawaomba nini. Hapo wakitambua kwamba imewapasa kunyenyekea mipango ya Mungu, wanainamisha mioyo yao kwa nira ya matakwa yake”.

Kwa msingi huo, alipojadili suala la ubora wa maisha ya sala, aliandika: “Yesu mwokozi ametuachia mfano wa maisha ya utendaji pale ambapo wakati wa mchana aliwajibika kufanya ishara na miujiza mjini, lakini alionyesha maisha ya sala hasa alipojitenga mlimani na kutumia usiku kusali… Hivyo mtumishi wa Mungu, akimuiga Kristo, awajibike katika sala hasa bila kujikatalia maisha ya utendaji. Isingekuwa vizuri kufanya tofauti. Kwa sababu, kama vile tunavyopaswa kumpenda Mungu kwa kuzamia sala, tunapaswa pia kumpenda jirani yetu kwa matendo”.

Alishika nafasi ya maana katika matukio ya nchi yake wakati huo ilipotawaliwa na kabila la Kijerumani la Wavisigoti, ambao aliwavuta kutoka uzushi wa Ario kwenye imani ya Mtaguso I wa Nisea na ya Mtaguso I wa Konstantinopoli. Katika hilo alifurahia sana wongofu wa Hermenegild, mrithi wa ufalme wao.

Alishiriki Mtaguso IV wa Toledo (633) uliolenga kuunganisha liturujia maalumu ya Kihispania. Ndiye mwakilishi bora wa liturujia hiyo, aliyoirekebisha na kuistawisha. Alipokaribia kufa, aliamua kupokea kitubio cha hadharani kadiri ya ibada aliyoitunga mwenyewe.

Kutokana na malezi aliyoyapata, alistawisha fasihi na elimu yoyote, ya Kikristo na ya kidunia, kuliko watu wote wa wakati wake.

Aliandika sana juu ya mambo mbalimbali: sayansi, historia, teolojia, maadili, sheria za Kanisa na ufafanuzi wa Biblia, akitumia madondoo yenye asili na aina tofauti sana, ingawa pengine bila kuyasanisi kwa mpango wa kuridhisha. Juhudi yake ilikuwa kutopoteza chochote cha zamani kilichoweza kusaidia siku za mbele.

Vitabu muhimu zaidi ni vile 20 vya *Etymologiae*, ambavyo aliviandika hasa kwa ajili ya malezi ya wakleri na vilikusanya ujuzi wote wa wakati ule, vikatumika sana katika Karne za Kati. Hivyo alipata kuwa kiungo kati ya mababu wa Kanisa, ambaye ni wa mwisho wao upande wa magharibi, na hatua iliyofuata.

Alifariki Sevilia tarehe 4 Aprili 636. Tangu zamani anaheshimiwa kama mtakatifu na babu wa Kanisa.

Mwaka 1722 Papa Inosenti XIII alimuongezea sifa ya mwalimu wa Kanisa.

Ni msimamizi wa mtandao na wa wanafunzi.

Sikukuu yake inaadhimishwa kila mwaka tarehe 4 Aprili.

## Yohane wa Damasko (676 hivi – 749 hivi)



Yohane wa Damasko (kwa Kiarabu Yuḥannā ibn Sarjūn) alikuwa mmonaki, padri na mwanateolojia kutoka mji mkuu wa Siria.

Alizaliwa Damasko mwaka 676 hivi, labda katika familia ya Kiarabu ya Kikristo. Hata hivyo alijisikia mrithi wa utamaduni wa Bizanti na kuandika kwa Kigiriki.

Babu yake, Manṣūr, alikuwa wa kwanza katika familia kupewa vyeo vikubwa chini ya utawala wa Kiislamu wa halifa Mu'awiya bin Abi Sufyan na wa waandamizi wake.

Baba yake pia alikuwa mwanasheria, akafuatwa na Yohane ambaye bado kijana alipata kuwa mshauri wa halifa wa Damasko na msimamizi wa mali yake. Lakini baadaye kidogo huenda akahukumiwa na kukatwa mkono wa kushoto.

Hapo (mwaka 700 hivi) alihama mji huo na kujiunga moja kwa moja na monasteri ya Mt. Saba, kati ya Bethlehemu na Yerusalemu, ambapo alipewa upadrisho.

Alihubiri na kuandika sana hadi kifo kilipompata huko Palestina akiwa na umri wa miaka 73 (mwaka 749 hivi).

Katika maandishi yake alikusanya mafundisho ya mababu waliomtangulia, yeye akiwa wa mwisho kati yao. Kitabu chake maarufu zaidi kinaitwa *Kuhusu Imani Sahihi*. Pia ametuachia tenzi bora kwa ajili ya liturujia.

Alitumia nguvu zake zote hasa kutetea matumizi ya picha na sanamu katika Ukristo dhidi ya waliotaka kuziteketeza kwa kushikilia makatazo ya Agano la Kale, lakini pia kwa kujilinganisha na Uislamu kwa malengo ya kisiasa.

Hoja zake zilitegemea hasa umwilisho wa Mwana wa Mungu tumboni mwa Bikira Maria. "Zamani Mungu, akiwa hana mwili wala sura, hakuchorwa kwa picha. Lakini, kwa kuwa sasa ameonekana katika mwili na kuishi kati ya watu, mimi nachora upande ule wa Mungu ulioonekana. Siabudu maada, bali Muumba wa maada ambaye alipata kuwa maada kwa ajili yangu, akakubali kuishi katika maada na kuniokoa kwa njia ya maada. Kwa hiyo sitaacha kuheshimu maada ile ambayo wokovu wangu umepatikana kwa njia yake. Ila siiheshimu kikamilifu kama Mungu! Ingewezaje kuwa Mungu kile kilichopewa kuwepo kutoka utovu wa vyote?… Hata hivyo mimi naheshimu na kustahi pia maada nyingine yote iliyoniletea wokovu, kwa kuwa imejaa nguvu na neema takatifu. Je, mbao za msalaba uliobarikiwa mara tatu si maada?… Na je, wino, na kitabu kitakatifu sana cha Injili, si maada? Je, altare ya ukombozi inayotupatia Mkate wa uzima si maada?… Na, muhimu kuliko yote, je, mwili na damu ya Bwana wetu si maada? Basi, ama tunatakiwa kufuta umbile takatifu la vitu hivyo vyote, ama tunatakiwa kulikubalia mapokeo ya Kanisa heshima ya picha za Mungu na za marafiki wake ambao wametakaswa na jina walilopewa, na kwa sababu hiyo wanatawaliwa na neema ya Roho Mtakatifu. Basi, usiikosee maada: haitakiwi kudharauliwa, kwa sababu hakuna kilichofanywa na Mungu ambacho ni cha kudharauliwa".

Hivyo Yohane alikuwa kati ya wale wa kwanza waliotofautisha ibada inayotupasa kwa Mungu tu na heshima inayoweza kutolewa kwa malaika na watakatifu wake na hata kwa picha zinazowachora, ambayo imestawi hasa katika Makanisa ya Mashariki hadi leo. Kwa jumla ni mtazamo mpya, chanya, juu ya ulimwengu: maada yenyewe inaweza kufanywa chombo cha neema kwa kuitiwa Roho Mtakatifu.

Alipewa ushindi na Mtaguso II wa Nisea (787) baada ya kifo chake.

Tangu zamani anaheshimiwa kama mtakatifu na babu wa Kanisa.

Mwaka 1883 Papa Leo XIII alimuongezea sifa ya mwalimu wa Kanisa. Ni msimamizi wa wachoraji.

Sikukuu yake inaadhimishwa kila mwaka tarehe 4 Desemba.

# WASIO MABABU WA KANISA

## Beda (672 hivi - 735)



Beda maarufu kama Mheshimiwa tangu enzi za uhai wake  alikuwa mmonaki, padri, mwanateolojia na mwanahistoria nchini Uingereza.

Hasa anafahamika kwa kitabu chake "Historia ya Kikanisa ya Taifa la Waingereza" (kwa Kilatini: *Historia Ecclesiastica Gentis Anglorum*). Akiona Kanisa lilivyozidi kustawi kati ya mataifa mapya, alipenda kuonyesha lisivyobanwa na ustaarabu moja, bali linakumbatia kila aina ya utamaduni ili kuikamilisha katika Kristo.

Karibu yale yote tunayoyajua kuhusu maisha ya Beda yamo katika sura ya mwisho ya *Historia Ecclesiastica*, aliyoimaliza mwaka 731 hivi, ambapo anadokeza kuwa yuko katika mwaka wa 59 wa maisha yake, hivyo alizaliwa 672–673.

Habari nyingine tunazipata katika barua ya mwanafunzi wake Cuthbert kuhusu kifo chake.

Beda hasemi kitu kuhusu asili yake, lakini kuna dalili kuwa familia yake ilikuwa na hali nzuri katika jamii.

Kumbe anataja mahali alipozaliwa kama "maeneo ya monasteri hii", yaani monasteri pacha ya Wearmouth na Jarrow, Northumbria, leo Uingereza Kaskazini Mashariki.

Alipofikia umri wa miaka 7, alitumwa monasterini ili apate malezi kutoka kwa abati Benedikto Biscop, halafu kwa Ceolfrith. Beda haelezi kama lengo la awali lilikuwa awe mmonaki baadaye. Lakini ndivyo ilivyotokea, akatumia maisha yake yote huko "kuimbia sifa za Mungu, kusoma, kufundisha na kuandika", alivyosema mwenyewe.

Alipofikia miaka 19 tu (692 hivi) alipewa daraja takatifu ya ushemasi, na alipofikia miaka 30 (702 hivi) alipata upadrisho.

Mtaalamu wa biolojia na historia, lakini hasa teoloja, alifaulu kufanya Biblia ieleweke kwa urahisi kupitia mahubiri yake sahili iliyofuata mfano wa mababu wa Kanisa.

Alipata kuwa kati ya wasomi wakuu wa Karne za Kati za mwanzo, akifaidika na magombo mengi muhimu aliyoletewa na maabati wake kutoka safari zao nyingi za ng'ambo.

Sifa ya ufundishaji na uandishi wake ilisababisha afanye urafiki na watu bora kadhaa wa wakati huo, ambao walimtia moyo kudumu katika kazi hiyo kwa faida ya wengi.

Mwaka 701 hivi aliandika vitabu vyake vya kwanza kwa ajili ya madarasa.

Aliendelea kuandika maisha yake yote, akimaliza vitabu zaidi ya 60, vingi vikiwepo hadi leo.

Biblia ilikuwa daima chanzo kikuu cha teolojia yake. Baada ya kuchunguza nakala ipi ni sahihi zaidi, aliifafanua Kikristo, akijitahidi kuelewa vizuri maneno yanasema nini, lakini kwa mwanga wa Kristo aliye ufunguo wa Maandiko yote katika umoja wake wa dhati. Kwake matukio ya Agano la Kale na ya Agano Jipya yanakwenda pamoja kuelekeza kwa Kristo.

Mada nyingine aliyoipenda sana ni historia ya Kanisa, kutokana na imani ya kwamba Roho Mtakatifu anazidi kufanya kazi ndani yake. Hivyo alipitia wakati wa Mitume, halafu mababu wa Kanisa na Mitaguso mikuu sita ya kwanza na kulinganisha tarehe za matukio mengi na ujio wa Yesu Kristo, akichangia kufanya wote wakubali kalenda iliyoenea sasa kila mahali, ikihesabu miaka kuanzia Kristo.

Vilevile alihesabu kitaalamu tarehe sahihi ya Pasaka, iliyo kiini cha mwaka mzima wa liturujia, akihimiza Wakristo wenyeji wa Uingereza na Ireland wakubali wote utaratibu wa Roma kuhusu mambo hayo. Kweli alichangia kuunganisha katika Ukristo mataifa ya Ulaya.

Hotuba zake zilifaulu kuongoza waamini waadhimishe vema mafumbo ya imani na kuyatekeleza maishani, huku wakitarajia ujio wa pili wa Yesu ili kuingizwa naye katika liturujia ya mbinguni.

Akifuata masisitizo ya mababu kama Ambrosi, Augustino na Sirili, alifundisha kwamba sakramenti hazimfanyi mtu "awe Mkristo tu, bali Kristo mwenyewe". Kila anayepokea kwa imani Neno la Mungu kwa mfano wa Maria anaweza kumzaa Kristo upya. Na Kanisa, kila linapobatiza watu, linakuwa "Mama wa Mungu" kwa kuwazaa kwa njia ya Roho Mtakatifu.

Alihimiza walei wawe na bidii katika kupata mafundisho ya dini na kuwashirikisha mapema watoto wao. Pia wasali mfululizo kwa kutolea matendo yao yote kama sadaka ya kiroho pamoja na Kristo.

Mwanashairi, aliandika tenzi kwa Bikira Maria ambazo ni kati ya zile bora zaidi zilizowahi kuandikwa.

Mwaka 708 baadhi ya wamonaki wa Abasia ya Hexham walimshtaki kuwa mzushi, lakini alifaulu kujitetea.

Mwaka 733 alisafiri hadi York, Lindisfarne na sehemu nyingine.

Alipougua, hakuacha kazi yake, akidumisha furaha ya dhati iliyojitokeza katika kusali na kuimba.

Alifariki tarehe 26 Mei 735 akazikwa Jarrow lakini masalia yake yakahamishiwa kwenye kanisa kuu la Durham katika karne XI.

Mwaka 1899 alitangazwa na Papa Leo XIII kuwa mtakatifu na mwalimu wa Kanisa.

Sikukuu yake inaadhimishwa kila mwaka tarehe 25 Mei.

## Petro Damiani (1007 - 1072)



Petro Damiani alikuwa mkaapweke wa urekebisho wa Wabenedikto wa Camaldoli nchini Italia.

Mmonaki halisi na mwenye msimamo pengine mkali, alitoa ushuhuda wazi wa umuhimu wa kumpa Mungu nafasi ya kwanza na kulenga utakatifu bila kupatana na uovu hata kidogo.

Kutokana na juhudi zake kubwa kwa urekebisho wa Kanisa lote ulioanzishwa na Mapapa wa wakati wake, alifanywa kardinali askofu na kuwa kati ya watu muhimu zaidi wa karne XI. Athari yake inadumu hata leo katika Kanisa Katoliki.

Petro Damiani alizaliwa mwaka 1007 mjini Ravenna nchini Italia katika familia ambayo iliwahi kuwa maarufu, lakini baadaye ikawa na hali duni kidogo.

Alikuwa wa mwisho kati ya ndugu 7: mkubwa wao aliitwa Damian, ambaye baadaye akawa padri na mmonaki.

Alibaki yatima mapema, akalelewa na wakubwa wake, hasa dada Roselinda na kaka Damian aliyemfanya mwanae. Kama shukrani kwake akajiongezea jina la Damiani, yaani wa Damian.

Damian alijitahidi kumsomesha mdogo wake huko Ravenna, halafu Faenza, alipobaki tangu mwaka 1022 hadi 1025. Baadaye Petro alihamia Parma ili kusoma lugha ya Kilatini, aliyoimudu vizuri sana, na sayansi za jamii (1026-1032).

Kisha kuhitimu masomo yake alianza kazi ya ualimu, halafu akarudi Ravenna akafundisha kwa miaka mitatu, iliyotosha kumpatia umaarufu, wanafunzi wengi na pesa. Inawezekana kwamba kwa wakati huo ameshaingia ukleri kwa daraja ndogo au hata ushemasi. Upadrisho alipewa na askofu mkuu Gebeardo wa Eichstätt (1027-1044).

Wakati alipoendelea na ualimu, alizidi kuvutiwa na umonaki akaanza kutimiza desturi kadhaa za kitawa (kukesha, kufunga n.k.), akizidi kujitenga na ulimwengu na kuzama katika sala.

Uamuzi wa kubadili maisha ulifikiwa alipotambua anajipendea bado kwa sababu akiwa mezani na kipofu alimpa mkate wa kifukara kuliko ule aliojipatia.

Basi, baada ya kukutana na wakaapweke wawili wa Fonte Avellana, palipokuwepo monasteri maarufu iliyoanzishwa na mtakatifu Romwald miaka michache ya nyuma, akawafuata aishi upwekeni huko, kulipokuwa na hali ngumu kabisa.

Monasteri hiyo ilikuwa wakfu kwa Msalaba mtakatifu, fumbo alilolipenda kuliko yote, hata akajiita "Petro, mtumishi wa watumishi wa msalaba wa Kristo". Alisema, "Wasiopenda msalaba wa Kristo, hawampendi Kristo".

Baadaye alipaswa kwenda kuhubiria watu na kurekebisha monasteri mbalimbali. Ili aweze kurekebisha wengine, hakuacha kujirekebisha kwa maisha ya uadilifu.

Huko Fonte Avellana aliombwa awafundishe na kuwalea Wakamaldoli wenzake, kazi aliyoendelea nayo hata katika Abasia ya Pomposa (1040-1042), akijitahidi kukomaza roho zao.

Mwaka 1042 priori wa Fonte Avellana alimtuma kurekebisha monasteri ya Mt. Vinsenti huko Furlo (karibu na Urbino), ambako aliandika maisha ya Romwald.

Mwishoni mwa mwaka 1043 alirudi Fonte Avellana, akachaguliwa kuwa priori wa jumuiya hiyo yenye wamonaki 20 hivi, kazi aliyoifanya kwa miaka 14, akihimiza uzingatifu wa upweke hapo na katika sehemu nyingine za Italia.

Wakati huo mgumu aliwasaidia Mapapa kwa maandishi yake, pia alichangia kulirekebisha Kanisa pamoja na mmonaki mwingine, Ildebrando wa Soana (ambaye baadaye akawa Papa Gregori VII na anaheshimiwa kama mtakatifu).

Sura ya Kanisa kama "Bibiarusi wa Kristo" aliyoichora vizuri katika maandishi yake haikulingana na hali halisi. Ndiyo sababu hakusita kulaumu upotovu wa wamonaki na wakleri, hasa kutokana na desturi ya vyeo vya kidini kutolewa na watawala wa kisiasa. Kwa ajili hiyo alitembelea majimbo mbalimbali ya Italia akionya maaskofu na hata kumfanya Papa awaondoe madarakani baadhi yao.

Alikwenda pia Ujerumani mara kadhaa kama mgeni wa Kaisari.

Alihudhuria sinodi za Roma za miaka 1047, 1049, 1050, 1051 na 1053 kuhusu dhambi ya usimoni akafaulu hasa kwa kupitisha sheria ya kuwa Papa achaguliwe na makardinali tu, bila kuingiliwa na viongozi wa siasa wala watu wengine.

Chini ya Papa Leo IX (1049-1054) na waandamizi wake Stefano IX, Nikolaus na Aleksanda II upana wa juhudi zake uliongezeka tena, akafanywa pia priori wa Ocri.

Hatimaye mwaka 1057 alifanywa na Papa Stefano IX kuwa kardinali askofu wa Ostia awe mshauri wake wa karibu kabisa (alipewa uaskofu mwaka 1058). Petro Damiani hakufurahia uteuzi huo, kwa jinsi alivyojisikia wito wa kuishi upwekeni, lakini akatii na kuhamia Roma.

Akitumwa na Papa sehemu mbalimbali za Italia na Ufaransa, Petro Damiani alistawisha urekebisho hasa kwa: kupambana na serikali zilizojiingiza katika uteuzi wa viongozi wa Kanisa,tena mara nyingi kwa njia ya rushwa;kusisitiza mamlaka ya juu ya Papa, kiini cha miundo ya Kanisa;kurudisha elimu na maadili katika maisha ya mapadri, akiwaelekeza kufuata mifano ya wamonaki.
Petro Damiani alimuomba mara kadhaa Papa amruhusu kurudi upwekeni. Baada ya miaka 10 alikubaliwa arejee Fonte Avellana (1067) na kuacha vyeo vyake vyote.

Kumbe miaka miwili baadaye akatumwa tena Frankfurt, Ujerumani (1069) ili kujaribu kumzuia Kaisari Henri IV asimpe talaka mke wake Bertha.

Mwaka 1071 alikwenda Montecassino ili kutabaruku kanisa la abasia hiyo maarufu.

Mwanzoni mwa mwaka uliofuata alirudi Ravenna ili kuleta amani ndani ya Kanisa baada ya Papa kukataza ibada zote ili kumuadhibu askofu mkuu wa huko aliyemuunga mkono Antipapa.

Akiwa njiani kurudi ugonjwa wa ghafla ulimlazimisha kusimama katika monasteri ya Santa Maria Vecchia Fuori Porta karibu na Faenza ambapo alifariki usiku wa tarehe 22 Februari 1072.

Mara baada ya kifo chake alianza kuheshimiwa kama mtakatifu kwa jinsi alivyotumia nguvu zake zote, za kiroho na za kimwili, kwa Kristo na Kanisa, akibaki kujiona daima "Petro, mtumishi wa mwisho wa wamonaki".

Mwaka 1828 Papa Leo XII alimuongezea sifa ya mwalimu wa Kanisa.

Sikukuu yake inaadhimishwa kila mwaka tarehe 21 Februari.

Aliandika vitabu muhimu vya aina mbalimbali vilivyoenea sana kuhusu liturujia, teolojia na maadilidini, mbali ya maisha ya Mt. Romwald, kanuni kwa ukaapweke, barua, hotuba na sala. Ndiye mwandishi bora wa karne XI.

Katika kanuni hiyo alisisitiza nidhamu ya mkaapweke ambaye, katika kimya cha ugo ana wito wa kuishi usiku na mchana katika sala, akifunga chakula vikali na kirefu; lakini pia anapaswa kutekeleza kwa bidii upendo wa kidugu kwa kumtii priori mara na kwa moyo wote.

Akisoma na kutafakari kila siku Maandiko matakatifu, Petro alitambua maana ya fumbo ya Neno la Mungu na kukuta humo lishe yake ya Kiroho. Kuhusu jambo hilo alifananisha chumba cha mkaapweke na "sebule ambamo Mungu anaongea na watu".

Kwake, ukaapweke ni kilele cha maisha ya Kikristo, "hali bora" kwa kuwa mmonaki, kisha kupata uhuru kutoka vifungo vya maisha ya kidunia na vya nafsi yake mwenyewe, anapokea "mahari kutoka kwa Roho Mtakatifu na roho yake yenye heri inakuwa imeunganika na Bwanaarusi wake wa kimbingu".


Mtu wa sala hasa, Petro alikuwa pia mwanateolojia safi: fikra zake juu ya mada mbalimbali zilimuongoza kwenye hatima muhimu. Kwa mfano, alifafanua imani kuhusu Utatu mtakatifu kwa namna wazi na hai. Uchunguzi wa kitaalamu wa fumbo hilo ulimfanya azame katika maisha ya ndani ya Mungu kama mzunguko wa upendo kati ya Nafsi zake tatu, halafu ahitimishe na maadili kwa maisha ya kijumuia na kwa mahusiano kati ya Wakristo wa Mashariki na wa Magharibi waliotenganika kuhusu mada hiyo.

Vilevile tafakuri yake juu ya Kristo ina athari za maana kwa maisha ya kila siku, kwa kuwa ndiye kiini cha Maandiko yote, hivyo anatakiwa kuwa kiini cha maisha ya mmonaki ili "Kristo aweze kusikika katika maneno yetu, Kristo aweze kuonekana katika maisha yetu, naye aweze kuhisika katika mioyo yetu". Muungano wa dhati na Kristo unawapasa pia wale wote waliobatizwa, ambao wasizamie kabisa shughuli, matatizo na mahangaiko ya kila siku hata kusahau kwamba Yesu anatakiwa kuwa kweli kiini cha yote.

Jinsi alivyopenda uzuri, alitazama ulimwengu wote kama msanii, akivumbua ndani yake mifano mingi sana ya maisha ya Kiroho na ya umungu. Kwa nadra vinapatikana vitabu vya kupendeza na kusisimua kama vya kwake.

Kwa ajili hiyo na kwa mchango wake katika urekebisho wa Kanisa, Papa Leo XII alimtangaza mwalimu wa Kanisa mwaka 1828.

## Anselm (1033 hivi- 1109)



Anselm alikuwa kati ya wanafalsafa na wanateolojia muhimu zaidi wa Karne za Kati huko Ulaya.

Baada ya kujiunga na monasteri ya Wabenedikto wa Bec huko Ufaransa, alipopata sifa kama kiongozi wa kiroho na mlezi, kama mhubiri wa mrekebishaji wa umonaki, alichaguliwa (1093) kuwa askofu mkuu wa Canterbury (Uingereza).

Sala, masomo na utawala ndiyo mambo yaliyojitokeza zaidi katika maisha yake aliyoyatumia katika nchi tatu tofauti. Maisha ya Kiroho ya dhati aliyokuwanayo yalimwezesha kuwa mlezi bora wa vijana, kiongozi mwenye busara na mtetezi wa uhuru wa Kanisa mbele ya serikali.

Anselm alizaliwa mwaka 1033 au 1034 mjini Aosta au karibu nao katika ufalme wa Borgogne (leo katika mkoa wa Valle d'Aosta, inapotumika lugha ya Kifaransa nchini Italia). Familia yake ilikuwa tajiri na ya kisharifu na upande wa mama ilihusiana na watawala wa Savoy.

Baba yake, Gundulf de Candia, mwenye asili ya Kilombardi, alikuwa mkali na kutapanya mali kwa anasa, tofauti na mama, Ermenberga wa Geneva, aliyekuwa na maadili mema ya dini. Ndiye aliyeshughulikia malezi ya kwanza ya Anselm, kifungua mimba, halafu akamkabidhi kwa Wabenedikto wa Aosta.

Kufuatana na ndoto aliyoipata, Anselm alijisikia kuitwa na Mungu kwa kazi muhimu na alipofikia umri wa miaka 15alitamani kuingia monasteri, lakini hakuruhusiwa kabisa na baba yake. Jambo hilo lilimfanya augue; lakini alipokuwa mahututi na kuomba kuvikwa kanzu ya Kibenedikto kama faraja ya mwisho, baba alimkatalia tena.

Kisha kupona na kufiwa mama yake aliacha masomo na kuishi kistarehe tu.

Alipofikia miaka 23, Anselm aliondoka nyumbani, akavuka milima ya Alps na kutangatanga katika Borgogne na Ufaransa akijitafutia mang’amuzi mapya. Baada ya miaka mitatu, akivutiwa na sifa ya Lanfranko wa Pavia (priori wa Abasia ya Bec), alikwenda Normandia mwaka 1059.

Chini ya huyo, Anselm alianza upya kusoma kwa bidii akawa mwanafunzi mpendwa na mshauri wake.

Mwaka uliofuata, kisha kuishi kidogo huko Avranches na kutathmini wito wake, aliingia rasmi malezi ya kitawa kama mnovisi akiwa na miaka 27 akapata upadrisho. Kuanzia hapo kanuni ya Benedikto wa Nursia iliathiri kabisa mawazo na maisha yake.

Juhudi za kiroho pamoja na masomo vilimfanya arudie katika ngazi ya juu zaidi urafiki na Mungu aliokuwanao utotoni.

Mwaka 1063 Lanfranko aliteuliwa abati wa Caen na Anselm akapewa nafasi yake kama priori wa Bec na mwalimu wa shule ya monasteri, ingawa alikuwa ameishi kama mmonaki miaka mitatu tu.

Alishika nafasi hiyo kwa miaka 15, akidhihirisha vipaji vyake kama mlezi mahiri, asiyebana vijana, bali akiwaachia nafasi ya kukua kwa uhuru wa kufaa. Ingawa alikuwa mkali kwake na kwa wengine kuhusu nidhamu ya kimonaki, alipenda zaidi kuhimiza kuliko kulazimisha.

Halafu akachaguliwa kwa kauli moja awe abati kutokana na kifo cha Herluin wa Bec, mwanzilishi wa abasia hiyo, kilichotokea mwaka 1078. Aliwekwa wakfu na askofu wa Evreux tarehe 22 Februari 1079.

Chini ya Anselm, Bec ikawa kituo bora cha elimu Ulaya, ikivutia wanafunzi kutoka nchi mbalimbali, ingawa masomo hayakuwa na nafasi ya kwanza katika umonaki.

Akiwa Bec aliandika vitabu vya kwanza vya falsafa, *Monologion* (1076) na *Proslogion* (1077–1078).

Humo aliandika, “Nakuomba, ee Mungu, nikufahamu, nikupende, nikufurahie. Nisipoweza kufikia furaha kamili katika maisha haya, niweze walau kusonga mbele siku kwa siku, mpaka furaha hiyo itakapokamilika”.

Vitabu hivyo vilifuatwa na *Majadiliano kuhusu Ukweli*, *Hiari* na *Anguko la Ibilisi*.

Wakati huo alijitahidi pia kulinda uhuru wa abasia dhidi ya mamlaka za nje.

Hapo katikati wamonaki wengi walikaribishwa Uingereza ili kuwaletea wenzao wa ng’ambo urekebisho uliozidi kuenea barani Ulaya. Mchango wao ulikubaliwa kiasi kwamba Lanfranko akawa askofu mkuu wa Canterbury.

Mara kadhaa Anselm alitembelea Uingereza kwa ombi la Lanfranko, ili kufundisha wamonaki na kumsaidia kusimamia mali ya abasia katika magumu yaliyofuatana na uvamizi wa Wiliamu I na Wanormani wenzake.

Kazi yake ilipendeza wenyeji wa huko kiasi kwamba Lanfranko alipofariki mwaka 1089, mwenyewe alichaguliwa kushika nafasi yake kama askofu mkuu wa Canterbury.

Kuanzia Desemba 1093, alipopata daraja hiyo, alishindana mara kadhaa na wafalme wa Uingereza Wiliamu II na Henri I, ili kutetea uhuru wa Kanisa lisiingiliwe na serikali; kwa sababu hiyo mara mbili ilimpasa kwenda uhamishoni (1103-1106). Katika msimamo wake aliungana na Papa. Hatimaye upatanisho kati ya mfalme na Papa ulimwezesha kurudi Canterbury, alipolakiwa na wakleri na walei kwa shangwe.

Anselm, kabla hajafariki huko tarehe 21 Aprili 1109, alitumia miaka yake ya mwisho kulea wakleri katika maadili na kufanya utafiti katika masuala mbalimbali ya teolojia.

Kitabu maarufu zaidi alichokiandika miaka hiyo ya mwisho kati ya Uingereza na Italia, kinaitwa *Cur Deus homo?* (*Kwa nini Mungu kawa mtu?*) na kimeathiri kwa miaka elfu mtazamo wa Kanisa la Magharibi kuhusu fumbo la wokovu.

Anselm aliacha pia mkusanyo mkubwa wa *Sala* na wa *Tafakuri*, mbali na *Barua* nyingi, ambazo zinawezesha kuona mafungamano ya kirafiki aliyokuwa nayo kwa wanafunzi wake.

Anselm anakumbukwa si tu kama mwanateolojia, bali pia kama mwanafalsafa, hasa kwa utafiti wake kuhusu *unum argumentum*, yaani hoja kuu inayojitegemea na kujitosheleza katika kuthibitisha uwepo wa Mungu na sifa zake.

Mtu mwenye uwezo mkubwa wa kuchimba nadharia, Anselm alitafuta, kwa kufuata nyayo za Plato na Augustino wa Hippo, namna ya kukutanisha *imani* na *akili*. Aliona akili ya binadamu ni chombo muhimu cha utafiti wa teolojia, ingawa alidai kwanza imani. Hivyoalirithi kwa Augustino kauli *credo ut intelligam, intelligo ut credam* (yaani "nasadiki ili nielewe, naelewa ili nisadiki").

Utafiti wa ukweli unategemea imani, lakini hiyo peke yake haitoshi, inadai pia aina mbalimbali za uthibitisho wa akili. Katika hilo akili, sawa na imani yenyewe, ina mwongozo wa hakika katika mwanga wa Mungu ambao usipokuwepo akili haiwezi kabisa kupenya fumbo la Mungu. Kwa maneno mengine, akili haitoi matamko, bali inasaidia kuelewa imani.

Anselm ni kati ya wataalamu wa kwanza waliounganisha falsafa na teolojia, kadiri ya neno *fides quaerens intellectum* (yaani "imani inadai akili"), litakalokuwa msingi wa teolojia ya shule. Pamoja na kuchochea hamu kubwa ya kuelewa mafumbo ya Mungu kwa kutumia mantiki, yeye alilenga daima “kuinua akili izame ndani ya Mungu”, akiendelea kukiri kwamba kazi ya kumtafuta Mungu haina mwisho, walau duniani.

Aliweka bayana kwamba yeyote yule anayetaka kusoma teolojia hawezi kutegemea akili yake tu, bali anatakiwa kustawisha maisha ya imani ya dhati. Hivyo kazi ya mwanateolojia apitie hatua tatu: 1) imani, zawadi ambayo Mungu anatutolea bure nasi tuipokee kwa unyenyekevu; 2) mang’amuzi, yanayopatikana kwa kutekeleza Neno la Mungu katika maisha ya kila siku; 3) ujuzi halisi, unaotegemea si mpangilio wa fikra tu, bali sala hasa.

Ndiyo maana aliandika, “Ee Bwana, sijaribu kupenya ukuu wako, kwa sababu sithubutu kabisa kulinganisha uelewa wangu na ukuu huo; ila natamani kuelewa kwa kiasi fulani ukweli wako, ambao moyo wangu unausadiki na kuupenda. Kwa kuwa mimi sijitahidi kuelewa ili nisadiki, bali nasadiki ili nielewe. Kwa sababu nasadiki hii pia: kwamba nisiposadiki, sitaweza kuelewa”.

Anselm alimheshimu Bikira Maria kwa moyo wa kitoto: “Maria, ndiwe yule ambaye moyo wangu unajitahidi kumpenda, ndiwe yule ambaye ulimi wangu unatamani motomoto kumsifu”.

Mwaka 1163 alitangazwa kuwa mtakatifu.

Mwaka 1720 alitangazwa na Papa Klementi XI kuwa mwalimu wa Kanisa kutokana na ubora wa maandishi yake yaliyoandaa nyakati zijazo na kumfanya ajulikane kama mwanzilishi wa teolojia ya shule.

Sikukuu yake inaadhimishwa kila mwaka tarehe 21 Aprili.

## Bernardo (1090 - 1153)



Bernardo wa Clairvaux alikuwa mmonaki, padri, abati na mwenezaji mkuu wa urekebisho wa Citeaux wa shirika la Benedikto wa Nursia.

Aliitwa "Babu wa mwisho" kwa sababu alitetea na kustawisha teolojia ya mababu wa Kanisa wakati wa kujitokeza teolojia mpya iliyoitwa "ya shule".

Ndiye mtu muhimu zaidi wa karne XII katika Kanisa Katoliki, ambalo linamheshimu kama mtakatifu (alivyotangazwa na Papa Aleksanda III mwaka 1174) na mwalimu wa Kanisa (alivyotangazwa na Papa Pius VIII mwaka 1830).

Sikukuu yake inaadhimishwa kila mwaka tarehe 20 Agosti.

Bernardo alizaliwa huko Fontaine-lès-Dijon, leo nchini Ufaransa, mwaka 1090. Alikuwa mtoto wa tatu kati ya saba waliozaliwa na Teshelino na Aleta, wote wa koo bora za watawala wadogo wa ufalme wa Borgogne (leo nchini Ufaransa).

Alisoma hasa lugha na hoja kwa Wakanoni wa kanisa la Nôtre Dame de Saint-Vorles, karibu na Châtillon-sur-Seine.

Kisha kurudi katika ngome ya baba yake huko Fontaines, mwaka 1111 alitawa pamoja na ndugu zake 5 na jamaa na marafiki kadhaa katika nyumba ya Châtillon, mpaka mwaka uliofuata akajiunga pamoja na wenzake 30 na monasteri ya Cîteaux (karibu na Dijon), iliyoanzishwa miaka 15 ya nyuma na Roberto wa Molesmes. Wakati huo ilikuwa chini ya Stefano Harding, abati wa tatu.

Urekebisho huo ulishika kwa bidii sana mashauri ya Kiinjili, hasa ufukara, bila kulemewa na mapokeo mengi ya ziada yaliyofuatwa katika monasteri ya kawaida.

Mwaka 1115, alipokuwa na miaka 25 tu, Stefano Harding alimtuma kuanzisha monasteri mpya, hivyo alihamia pamoja na wamonaki wenzake 12 katika mkoa wa Champagne, walipozawadiwa shamba kubwa karibu na mto Aube, wakaliita Clairvaux, yaani bonde angavu.

Akiwa hivyo na nafasi ya kutekeleza umonaki alivyouona yeye, alifaulu kuunganisha sala na masomo upande mmoja na utendaji mkubwa upande mwingine. Akiangalia hali ya monasteri nyingi, alisisitiza haja ya kuishi kwa kiasi katika chakula, mavazi na majengo na ya kushughulikia mafukara.

Kwa muda mfupi Abasia ya Clairvaux ikawa kivutio kikubwa kwa miito ya utawa hata ikaweza (kuanzia mwaka 1118) kutuma wamonaki wake kuanzisha sehemu nyingine kama vile huko Trois-Fontaines, Fontenay, Foigny, Autun, Laon. Bernardo alipokufa abasia za urekebisho wa Citeaux zilikuwa 343, ambazo kati yake 66

zilianzishwa au kurekebishwa naye, kutoka Hispania hadi Siria, kutoka Italia visiwani hadi Uswedi. Mbali ya kuwa mahali pa kuishi kidini, zilikuwa pia vyuo vya kilimo na ufundi.

Kipindi kilichotangulia mwaka 1130 Bernardo aliandikiana sana na watu wa kila aina. Mbali ya barua hizo nyingi, alitoa hotuba nyingi na vitabu mbalimbali.

Tangu mwaka 1130 alianza kushughulikia masuala mengi mazito ya Kanisa na ya Upapa. Kwa ajili hiyo ilimbidi aondoke utawani mara nyingi zaidi na zaidi hata kusafiri pengine nje ya Ufaransa, pia kwa kuanzisha monasteri za wanawake.

Maisha yake yote Bernardo akawa mtetezi shujaa wa imani sahihi na wa mamlaka ya Kanisa.

Katika maandishi yake ya kupinga uzushi, alimlenga hasa Abelardo, msomi mahiri aliyebuni namna mpya ya kufanya teolojia akitumia zaidi mantiki na hoja za falsafa. Kisha kupata hukumu ya Sinodi ya Sens ya mwaka 1140 dhidi ya baadhi ya mafundisho ya Abelardo, hatimaye alifaulu kupatana naye kwa msaada wa Petro Mhashamu wa Cluny.

Zaidi tena alipinga Wakatari, waliodharau ulimwengu wa maada pamoja na mwili wa binadamu, na hivyo walimkosea shukrani Muumba wa vyote.

Kinyume chake aliwajibika kutetea Wayahudi dhidi ya mashambulizi yaliyowapata mara nyingi zaidi na zaidi.

Miaka hiyohiyo Bernardo aliandika vitabu vyake maarufu zaidi, kama vile Hotuba juu ya Wimbo Ulio Bora

Alipatanisha Wakristo (na watawala wao) waliokuwa wanagombana. Vita vya msalaba vya mwaka 1147 vilifanikiwa kuungwa mkono na watu wa Ufaransa na Ujerumani kutokana na mahubiri yake.

Miaka ya mwisho alilazimika kupunguza safari zake, hivyo alipata nafasi zaidi kwa maandishi yake, akiyapitia upya na kuyaongeza.

Kitabu cha pekee cha mwaka 1145 ambacho kinaitwa "Kuzingatia" alikiandika kwa ajili ya mwanafunzi wake Bernardo Pignatelli ili kumuongoza katika majukumu yake mapya alipochaguliwa kuwa Papa kwa jina la Eugene III. Humo unajitokeza pia mtazamo wa dhati juu ya fumbo la Kanisa ambao kupitia fumbo la Kristo unaishia kuzama katika fumbo la Utatu.

Mwishoni mwa mwaka 1152 alikuwa ameishiwa nguvu, lakini alisafiri hadi Metz ili kutuliza fujo za mji huo.

Alipokuwa akirudi Clairvaux, akafariki Ville-sous-la-Ferté, tarehe 20 Agosti 1153.

Bernardo hakuelekea ujuzi unaotokana na mantiki, bali ule unaopatikana kwa kuzama katika mafumbo kwa sala ya kumiminiwa. Kwake ndiyo njia pekee ya kumfahamu kweli Mungu na kufikia amani na heri ya kuwa naye. Hivyo, akipinga teolojia ya shule iliyokuwa inaanzaanza, alishikilia mapokeo ya Biblia, ya mababu wa Kanisa, ya liturujia na ya umonaki, pia kwa lengo la kulinda imani sahili ya waamini wa kawaida.

Kwake upendo mkubwa zaidi na zaidi ndio lengo pekee la teolojia, alivyoeleza katika kitabu "Kumpenda Mungu". Safari hiyo ya roho ina hatua mbalimbali ambazo alizifafanua kinaganaga na ambazo zinakamilika katika ulevi wa upendo usiosemeka.

Tangu hapa duniani mtu anaweza kufikia muungano huo na Neno wa Mungu ambao Bernardo aliuita "arusi ya kiroho". Hapo Neno anaitembelea roho, anakomesha ndani yake dalili za mwisho za ukaidi, anaiangaza, anaiwasha na kuigeuza.

Fikra zetu kuhusu mafumbo ya Mungu ziko katika hatari ya kugeuka zoezi la bure la akili zisipotegemea imani ya dhati iliyolishwa na sala katika uhusiano wa dhati na Bwana: ndiyo "ujuzi wa watakatifu" ambao unatolewa na Roho Mtakatifu na kuhitajiwa na teolojia.

"Ni lazima tuendelee kumtafuta Mungu huyo, asiyetafutwa bado vya kutosha, lakini inaweza kuwa rahisi zaidi kumtafuta na kumpata katika sala kuliko katika mijadala". Mtume Yohane, aliyeegama kichwa chake kifuani pa Yesu, anabaki kielelezo cha mwanateolojia na cha mwinjilishaji bora.

Mbele ya hoja kali zilizozidi kutolewa katika mihadara ya shule, Bernardo alisisitiza kwamba Yesu tu ni "asali kinywani, wimbo sikioni, shangilio moyoni… Lishe yote ya roho ni kavu isipolainishwa na mafuta hayo; haina ladha isipotiwa chumvi hiyo. Unachoandika hakininogei nisiposoma Yesu ndani yake".

Ndiyo sababu mapokeo yamemuita “Doctor Mellifluus”, yaani “Mwalimu mtamu kama asali”, kwa jinsi masifu yake kwa Kristo yalivyobubujika kwa utamu.

Pamoja naye alimmiminia sifa Bikira Maria, kiasi kwamba miaka 150 hivi baada ya kifo chake, Dante Alighieri alimtia mdomoni maneno haya: “Bikira Mama, binti wa Mwanao, mnyenyekevu na mkuu kuliko viumbe, shabaha maalumu ya mpango wa milele”.

Bernardo hakuwa na shaka: ni kwa njia ya Maria kwamba tunamuendea Yesu (kwa Kilatini, “Per Mariam ad Iesum”). Ndiyo sababu alihimiza, “Katika hatari, katika huzuni, katika shaka, umfikirie Maria, umuitie Maria. Yeye asiache kamwe midomo yako, asibandukane kamwe na moyo wako; na ili uweze kupata msaada wa sala zake, usisahau kamwe mfano wa maisha yake. Ukimfuata, huwezi kusita; ukimuomba, huwezi kukata tamaa; ukimfikiria, huwezi kukosea. Akikutegemeza, hutajikwaa; akikulinda, huna la kuogopa; akikuongoza, hutaanguka kamwe; akiwa upande wako, utafikia lengo lako”.

Kulingana na mapokeo, Bernardo alishuhudia kwamba Maria yuko chini ya Kristo, lakini pia alisisitiza nafasi ya pekee aliyonayo katika mpango wa wokovu, kutokana na jinsi alivyoshiriki kikamilifu sadaka ya Mwanae.

Alimuambia hivi wakati wa kuhubiri, “Mama mwenye heri, kweli upanga ulichoma roho yako!… Ukali wa uchungu ulichoma roho yako kwa ndani hivi kwamba ni haki tukuite mfiadini, kwa sababu ndani mwako ushiriki wa mateso ya Mwanao unazidi kabisa kwa ukali mateso ya kimwili ya kufia dini”.

Katika vitabu vingi, hasa vya ufafanuzi wa Biblia, alivyoviandika, unajitokeza upendo hai uliomuongoza daima kama alivyoandika, “Upendo ndio nguvu kuu ya maisha ya kiroho”.

## Hildegarda (1098 hivi- 1179)



Hildegarda wa Bingen  alikuwa mmonaki wa shirika la Mt. Benedikto, na mtunzi wa vitabu vya aina mbalimbali kutoka Ujerumani.

Mwanamke huyo anazidi kusema leo kwa upendo wake kwa Kristo na kwa Kanisa (ambalo hata wakati wake alijeruhiwa na dhambi za watoto wake), kwa ujasiri wake katika kutambua ishara za nyakati, kwa jinsi alivyopenda viumbe, kwa utabibu wake na kwa sanaa zake.Hildegarda alizaliwa Bermersheim vor der Höhe, Rhineland, mwaka 1098 hivi, na Hildebert na Mekthilde katika familia tajiri ya kisharifu kama mtoto wa kumi, mgonjwa tangu mwanzo.

Katika kitabu chake “*Maisha”*, anasimulia kwamba alianza kupata njozi akiwa na miaka 3 tu, na kwamba alipofikia miaka 5 alianza kutambua ni karama kutoka kwa Mungu.

Labda kwa sababu hiyo wazazi wake walimtoa kwa Mungu akiwa na umri wa miaka 8, amtumikie utawani kulingana na Kanuni ya Mt. Benedikto,  wakamweka kwa malezi ya kiutu na ya Kikristo kwanza chini ya Uda wa Gölklheim, mjane aliyewekwa wakfu, halafu chini ya Jutta wa Sponheim, aliyekwisha kuvikwa shela katika monasteri changa ya wanawake Wabenedikto.

Hakuna kumbukumbu za miaka 24 aliyoishi na Jutta. Kwa vyovyote, walikuwa wamejifungia huko Disibodenberg, katika msitu wa Palatinate. Lakini Jutta pia alikuwa na njozi, jambo lililovutia wengi kumtembelea.

Jutta alimfundisha kusoma na kuandika, lakini hakuweza kumsaidia katika ufafanuzi wa Biblia. Inawezekana wakati huo ndio alipojifunza muziki na kuanza utunzi wake. Hildegarda alivikwa kimonaki na askofu Oto wa Bamberg akaweka nadhiri mwaka 1115.

Baada ya Jutta kufariki mwaka 1136, Hildegarda alichaguliwa na wamonaki wenzake kwa kauli moja kushika nafasi yake kama "magistra" (yaani mwalimu na kiongozi) wa jumuia yao ya kike.

Hapo alitimiza kazi yake kwa kutumia vipawa vyake kama mwanamke mwenye elimu na maisha ya Kiroho ya hali ya juu, akikabili vema majukumu ya uongozi. Alilenga hali bora jumuiani kwa busara na kiasi inavyodaiwa na Kanuni ya Mt. Benedikto.

Baada ya miaka michache, kutokana pia na wingi wa miito iliyojitokeza kujiunga naye, alimuomba Abati Kuno wa Disibodenberg aweze kuhamia hali ya kifukara zaidi huko Rupertsberg.

Alipokataliwa, alimkimbilia askofu mkuu Henry I wa Mainz: hatimaye akakubaliwa na abati akahamia na wenzake 20 hivi katika monasteri ya Rupertsberg mwaka 1150, ambapo paroko mmonaki Volmar akawa muungamishi na pia karani wake pamoja na sista Richardis wa Strade.

Mwaka 1165 Hildegarda alianzisha monasteri nyingine huko Eibingen, upande wa pili wa mto Rhine, akawa abesi wa zote mbili na kustawisha hasa maisha ya pamoja, elimu na liturujia. Alichochea watawa washindane katika kupeana heshima, kutumikiana na kutenda mema.

Ingawa Hildegarda alisema haiwezekani kuyasimulia aliyojaliwa kujua kwa mwanga wa Mungu kupitia hisi zake na alisita kuyashirikisha, mwaka 1141, akiwa na miaka 42, alisadiki Mungu amemuagiza ayaandike yote. Hata hivyo aliendelea kusita, akitamani uthibitisho wa watu wenye hekima kwa kuogopa amedanganyika.

Alipoomba shauri la Mt. Bernardo, alimuandikia: “Njozi inateka nafsi yangu yote: siioni kwa macho ya mwili bali inanitokea katika roho ya mafumbo… Natambua maana ya dhati ya maneno ya Zaburi, ya Injili na ya vitabu vingine, kama nilivyoonyeshwa katika njozi. Hiyo inawasha kama mwali wa moto katika kifua changu na katika roho yangu na inanifundisha kuelewa matini kwa dhati”. Alijibiwa kwamba asijali sana njozi, ila aendelee kutenda mema kwa bidii.

Kitabu cha *Maisha* yake kilianza kuandikwa na Godfrey wa Disibodenberg chini ya usimamizi wa Hildegarda.

Kati ya Novemba 1147 na Februari 1148, wakati wa Sinodi ya Trier, Papa Eugene III alipata habari za maandishi hayo akayathibitisha kuwa mafunuo ya Roho Mtakatifu, akimruhusu Hildegarda kuandika njozi zake na hata kuhubiri hadharani, tofauti na kawaida ya wanawake wa wakati ule.

Tangu hapo alizidi kuheshimiwa akaitwa “nabii wa kike wa Kijerumani”. Kwa mamlaka ya kiroho aliyopewa tena na Papa Adriani IV na Papa Aleksanda III, miaka yake ya mwisho alisafiri sana ili kusema na taifa la Mungu, bila kujali uzee na ugumu wa safari.

Katika nyanja za miji na katika makanisa makuu, kama yale ya Koln, Trier, Liège, Mainz, Metz, Bamberg na Würzburg, wote walimsikiliza kwa makini, hata alipozungumza kwa ukali, kwa kuwa waliamini ni mjumbe wa Mungu.

Watu wengi wa kila aina, wakiwemo maaskofu, maabati na watawala, walimuomba shauri. Ndiyo sababu tuna barua zake nyingi, karibu 400. Humo tunashuhudia alivyozingatia matukio ya wakati ule, akiyafafanua kwa mwanga wa fumbo la Mungu.

Kaisari Fredrick I aliposababisha farakano ndani ya Kanisa kwa kukubali Maantipapa walau watatu dhidi ya Papa Aleksanda III, Hildegarda hakusita kumuandikia alichosikia katika njozi: “Utajutia mwenendo huo mwovu kama wa mtu asiye na Mungu na anayenidharau! Sikiliza, ee Mfalme, ukitaka kuishi! La sivyo upanga wangu utakuchoma”.

Zimetunzwa hotuba 58 alizozitoa kwa masista wenzake kama ufafanuzi wa Injili ambazo zilitumika katika sikukuu za mwaka wa liturujia.

Nje ya monasteri alijitahidi kuimarisha imani na maisha ya Kikristo. Alihimiza hasa wamonaki na wakleri kuishi inavyodaiwa na wito wao, lakini alipinga sana Wakatari waliotaka urekebisho mkali wa Kanisa. Aliwalaumu kwa kujaribu kupindua umbile halisi la Kanisa akawakumbusha kwamba urekebisho halisi unategemea roho nyofu ya toba na mchakato mgumu wa wongofu kuliko mabadiliko ya miundo tu.

Maandishi yake yalitokana hasa na mang'amuzi yake ya juu katika sala, hivyo yanajitokeza kwa udhati, usahihi na upekee wa mitazamo. Kwa kutumia mawazo na maneno ya mazingira yake, na zaidi lugha ya kishairi na ya kifumbo, alifafanua Maandiko matakatifu kwa mwanga wa Mungu na kuhusiana na maisha yalivyo. Ndiyo sababu wale wote waliomsikiliza walijisikia haja ya kuishi Kikristo kweli.

Njozi zake zina maana kubwa upande wa teolojia, zikihusu matukio makuu ya historia ya wokovu na kufanana na zile za manabii wa Agano la Kale. Kwa mfano, katika kitabu chake maarufu zaidi, "Scivias" (yaani "Zijue Njia"), njozi 35 zinajumlisha habari za kuanzia uumbaji wa ulimwengu hadi mwisho wa nyakati.

Kwa hisia yake ya kike Hildegarda katika kiini cha kitabu chake anafafanua ndoa ya fumbo kati ya Mungu na binadamu iliyofanyika katika umwilisho. Juu ya msalaba iliadhimishwa arusi ya Mwana wa Mungu na Kanisa lililojazwa neema ili liweze kuzaa watoto wa Mungu wengine katika upendo wa Roho Mtakatifu.

Vitabu vingine viwili vinaripoti pia njozi zake: "Kitabu cha Stahili za Maisha" na "Kitabu cha Kazi za Mungu", ambacho wengi wanakiona kuwa bora kuliko vyote.

Akiwa msanii, alitunga tenzi, antifona na nyimbo ambazo zilikusanywa kwa jina la "Muziki wa Ulinganifu wa Mafunuo ya Kimbingu" na kutumika kwa furaha monasterini, zikieneza hali ya utulivu.

Maandishi yake mengine, yakizungumzia hata utabibu, sayansi na isimu, yanaonyesha wingi wa elimu uliokuwemo katika monasteri ya kike ya Karne za Kati, nayo yaliathiri watu wengi, yakichangia upyaisho wa teolojia, liturujia, sayansi na muziki.

Hakuna mwanamke wa Karne za Kati anayeweza kushindana na Hildegarda kwa wingi na ubora wa maandishi wala kwa upana wa mada alizozijadili.

Tena ndani mwake mafundisho na maisha yalilingana kabisa. Akilenga kutimiza matakwa ya Mungu nyuma ya Kristo, alitekeleza maadili yote mfululizo na kwa bidii, akitegemezwa na vitabu vya Biblia, liturujia na mababu wa Kanisa awe mali ya Bwana tu kadiri ya Kanuni ya Mt. Benedikto.

Masista wenzake waliomzunguka alipofariki Bingen am Rhein tarehe 17 Septemba 1179, walisema kuwa waliona miali miwili ya mwanga kutoka angani na kupitia chumba chake.

Toka zamani abesi huyo aliheshimiwa na Kanisa Katoliki, halafu na Waanglikana na Walutheri kama mtakatifu. Papa Benedikto XVI alithibitisha utakatifu wake tarehe 10 Mei 2012 na kumtangaza mwalimu wa Kanisa tarehe 7 Oktoba 2012.

Sikukuu yake inaadhimishwa kila mwaka tarehe 17 Septemba.

## Antoni wa Padua (1195 - 1231)



Antoni wa Padua, kwa jina la kiraia Fernando Martim de Bulhões e Taveira Azevedo - alikuwa padri na mtawa wa shirika la Ndugu Wadogo, maarufu hasa kwa mahubiri yake.

Ni mmojawapo kati ya watakatifu wanaoheshimiwa zaidi katika Kanisa Katoliki, pia kwa sababu ya miujiza mingi inayosemekana kupatikana kwa kukimbilia maombezi yake.

Waamini wengi wanapenda picha zinazomuonyesha akiwa na maua meupe pe, yakimaanisha usafi wa moyo wake, na akimshika mtoto Yesu mikononi, kadiri ya tukio la ajabu lililosimuliwa na vyanzo mbalimbali.

Kwa vipawa vyake vya pekee upande wa akili, elimu, busara, kiasi, ari ya kitume na sala hasa, alichangia sana maendeleo ya shirika lake.

Antoni aliishi katika kipindi cha mageuzi cha Karne za Kati. Maisha yake yaliandikwa kwa mara ya kwanza (*Vita prima au Assidua*) na mtawa asiyejulikana mwaka 1232 kufuatana na taarifa za askofu wa Lisbon, Soeiro II Viegas (1210-1232).

Alizaliwa na familia ya kisharifu karibu na kanisa kuu la Lisbon, Ureno, tarehe 15 Agosti 1195; huko alipata ubatizo halafu elimu.

Akiwa na miaka 15 alijiunga na shirika la Augustino wa Hippo katika monasteri ya Lisbon, halafu (1212) akahamia Coimbra ili kutulia zaidi. Katika mji huo maarufu kwa elimu alijitosa kusoma Biblia na mababu wa Kanisa, akijipatia ujuzi alioushirikisha baadaye kwa kufundisha na kuhubiri.

Huko Coimbra lilitokea jambo lililobadili kabisa maisha yake. Akiwa padri tayari, alihamia kwa Ndugu Wadogo (1220) kisha kuona masalia ya wafiadini 5 wa kwanza wa shirika hilo jipya yakitokea Moroko walipouawa na Waislamu. Ndipo alipojibadilishia jina kuwa Antoni.

Akitamani yeye pia kuwa mmisionari na kumfia Yesu, mwaka huohuo alikwenda Moroko pamoja na mwenzake mmoja, lakini baada ya kuugua huko miezi kadhaa alikubali kurudi Ureno.

Hata hivyo baharini meli yao ilipatwa na dhoruba iliyowatupa katika kisiwa cha Sicilia, ambapo walisikia kwamba mwezi Mei huko Assisi kutakuwa na mkutano mkuu wa shirika.

Hivyo mwaka 1221 alikwenda huko kushiriki huo mkutano maarufu ulioitwa "wa mikeka", na ndipo alipokutana na mwanzilishi, Fransisko wa Asizi, pamoja na kujua zaidi hali ya shirika, mipango yake ya kitume na mabishano kuhusu kanuni iliyokuwa inatungwa.

Akiwa mnyenyekevu sana, ingawa mwenye hekima na elimu kubwa, mkutano ulipokwisha alikuwa hajachaguliwa na mkuu yeyote wa kanda, mpaka ndugu Grasyano alipompeleka Montepaolo, karibu na Castrocaro, walipokuwepo watawa wengine 6, ili awasomee Misa. Aliishi huko mwaka mmoja akifanya kazi duni, pamoja na kusali na kujinyima.

Katikati ya mwaka 1222, watawa hao walikwenda Forlì kushiriki upadrisho. Askofu alipohitaji mhubiri atoe mawaidha kwa mapadri wapya, hakupatikana. Basi, mkubwa wake akamuagiza Antoni, ambaye akaja hivyo kujulikana kwa ubora wa mahubiri.

Ndipo alipoanza kazi hiyo kwa kutembelea mahali mbalimbali pa Italia na Ufaransa, akifundisha maadili kama ilivyokuwa desturi ya shirika lakini pia kuponda uzushi na kurudisha katika Kanisa Katoliki wengi walioliasi.

Kutokana na elimu yake alisisitiza umuhimu wa kuandaa ndugu wengine kwa kazi hiyo, lakini hakukubali kufanya hivyo mpaka aliporuhusiwa na Fransisko kufundisha teolojia huko Bologna (1223). Katika barua fupi aliyomuandikia, mwanzilishi huyo alimuita kwa heshimu "askofu wangu" na kumwekea sharti la kutozimisha roho ya sala kwa masomo.

Akiwa wa kwanza, au mmojawapo kati ya wale wa kwanza, kufanya kazi hiyo, aliweka misingi ya teolojia ya Kifransisko, iliyofikia kilele chake katika mafundisho na maandishi ya Bonaventura wa Bagnoregio na Yohane Duns Scotus.

Kutokana na uwezo wake katika kuhubiri, aliagizwa pia (1224) kwenda kuzuia uenezi wa uzushi wa Wakatari huko Ufaransa alipobaki miaka 2. Wakati huo alichaguliwa kuwa mhudumu wa jumuia kadhaa.

Baada ya kushiriki mkutano mkuu wa mwaka 1227, mtumishi mkuu mpya alimchagua Antoni kuwa mtumishi wa kanda ya Italia Kaskazini. Kwa miaka 3 iliyofuata, pamoja na kutembelea konventi za eneo hilo kubwa kama kiongozi, aliendelea na kazi ya kuhubiri huko na huko, akiwa amejichagulia Padova kama makao yake.

Ndani ya shirika, baada ya kifo cha Fransisko, yalikuwa yamezuka mabishano makali kati ya walioshikilia wasia wa mwanzilishi na wale waliotaka shirika liweze kushindana na mashirika mengine. Yeye na watumishi wengine kutoka kanda mbalimbali wakaona utatuzi unaweza kutokea kwa Papa tu.

Akipokea ombi lao, Papa Gregori IX (1227-1241) alitoa tamko rasmi la kwanza juu ya kanuni (1230), akitumia mamlaka yake ya Kipapa na hasa ujuzi wake wa nia ya Fransisko (akiwa ndiye aliyemsaidia kutunga kanuni alipokuwa bado kardinali, jina lake Ugolino).

Kuhusu wasia alitamka si sheria inayowabana Wafransisko wasiweze kufafanua kanuni yao wala kufafanuliwa na Kanisa, wala kuomba wala kupewa hati na fadhili za Papa. Sababu ya msingi ni kuwa Kanisa liko juu kuliko kanuni.

Kwa kukabili suala hilo kwa mtazamo wa sheria, Gregori IX alikata hamu ya mwanzilishi ya kuiona kanuni kama kituo cha kuanzia safari tu, si cha mwisho. Kwa namna hiyo aliwaingiza zaidi Ndugu Wadogo ndani ya kawaida ya Kanisa.

Upande wa ufukara kwa jumla alitetea msimamo wa mwanzilishi (kwa jinsi alivyomheshimu hata akamtangaza mtakatifu karibu bila kufuata taratibu za kesi), ila aliulegeza kiasi, kwa lengo la kufanikisha zaidi utume wa Ndugu Wadogo na hivyo kurekebisha Kanisa lililokuwa na hali mbaya kiroho.

Kwa ajili hiyo Gregori IX aliwapa pia hati na ruhusa nyingi za pekee dhidi ya mamlaka ya maaskofu na maparoko. Hivyo njia ikawa wazi kuligeuza shirika la wadogo wanaohubiri toba kwa unyenyekevu chini ya padri yeyote, liwe shirika imara lililo chini ya maaskofu kwa machache tu.

Mageuzi hayo, yaliyosababisha kwa muda mrefu upinzani mwingi wa maaskofu na mapadri wanajimbo, yalichangiwa pia na ustawishaji wa elimu ndani ya shirika uliozidi kuwalinganisha Ndugu Wadogo na watawa wengine na kuongeza idadi ya mapadri kati yao.

Katika hayo yote, inasadikika kuwa Antoni alichangia kiasi chake.

Baada ya kusafiri sana, hatimaye alirudi Padova kumalizia maisha yake. Huko alihubiri kwa mara ya mwisho Kwaresima ya mwaka 1231, iliyo kilele cha kazi yake na iliyozingatia sana masuala ya jamii, akafariki ameishiwa nguvu tarehe 13 Juni 1231, akiwa na umri wa miaka 36 tu.

Alitangazwa mtakatifu na Papa Gregori IX mapema sana tarehe 13 Mei 1232, na mwalimu wa Kanisa na Papa Pius XII mwaka 1946 kwa jina la *Doctor Evangelicus* (Mwalimu wa Kiinjili), kutokana na mafundisho yake kujaa roho na maneno ya Injili ya Yesu Kristo.

Sikukuu yake inaadhimishwa kila mwaka tarehe 13 Juni.

Antoni ametuachia mifululizo miwili ya hotuba juu ya masomo ya Biblia yalivyopangwa na liturujia, mmoja kwa ajili ya Jumapili, mwingine kwa ajili ya sikukuu za watakatifu. Humo anaelekeza kwa usahili na uzuri wa Kiinjili safari ya Kiroho ya kumfuata Yesu Kristo. Akitambua ubinadamu ulivyo, anahimiza mfululizo kupiga vita dhidi ya kiburi, uroho na uchafu ili kutekeleza maadili ya unyenyekevu na utiifu, ukarimu na ufukara, kiasi na usafi wa moyo.

Mada kuu ya mahubiri yake ni kwamba mtu wa sala tu anaweza kupiga hatua katika maisha ya Kiroho. Humo anafundisha juu ya sala kama uhusiano wa mapendo na Bwana unaohitaji hali ya kimya, si cha nje tu, bali hasa cha moyoni. Kwake inahitajika misimamo minne: kwanza, kuweka wazi moyo wetu kwa Mungu; pili, kutambua uwemo wake na kuongea naye kwa upendo; tatu, kumueleza shida zetu; nne, kumsifu na kumshukuru.

Katika mafundisho kama hayo inajitokeza tayari tabia maalumu mojawapo ya teolojia ya Kifransisko: kusisitiza upendo, ambao kutoka kwa Mungu unaenea rohoni upande wa utashi na unakuwa chemchemi ya ujuzi wa Kiroho unaopita ujuzi mwingine wowote. Kwa sababu ni kwa kupenda kwamba tunakuja kufahamu. “Upendo ndiyo roho ya imani na kuipa uhai; bila upendo, imani inakufa”.


Tabia nyingine ni kumpa Kristo nafasi yake kama kiini cha mpango wa Mungu na cha mambo yote. “Ukimhubiri Yesu, atalainisha mioyo migumu; ukimlilia atapunguza ukali wa vishawishi; ukimfikiria ataangaza uelewa wako; ukisoma habari zake atashibisha akili yako”.

Katika kuzingatia kwa mshangao unyenyekevu wa umwilisho na upendo wa mateso yake, Antoni kama Fransisko alitambua zaidi wajibu wa kumshukuru Mungu na kuheshimu kila mtu.

“Kristo, aliye uhai wako, ametundikwa mbele yako, uweze kuutazama msalaba kama kwamba ni kioo. Humo utaweza kujua majeraha yako yalivyokuwa ya kukufisha, kiasi kwamba Damu ya Mwana wa Mungu ilikuwa dawa pekee ya kukuponya. Ukitazama kwa makini zaidi utaweza kutambua ukuu wa hadhi yako kama mtu na wa thamani yako… Hakuna mahali ambapo mtu ataweza kuelewa vizuri zaidi ubora wake kuliko kwa kujitazama katika kioo cha msalaba”.

Mbele ya ustawi wa miji na biashara, uliofanya wengi wasijali mahitaji ya mafukara, alielekeza utajiri wa kweli, ule wa moyo wenye huruma: "Enyi matajiri, mwatendee kwa wema… maskini, mwapokee nyumbani mwenu: kesho wenyewe ndio watakawaowapokeeni katika maskani za milele palipo uzuri wa amani, hakika ya usalama na utulivu tajiri wa shibe ya milele".

## Alberto Mkuu (1205 hivi - 1280)



Alberto Mkuu (Lauingen, Donau, leo nchini Ujerumani,1205 hivi - Cologne, Ujerumani, 15 Novemba 1280) ni jina alilopewa kwa heshima askofu Alberto wa Bollstädt (au wa Cologne) kutokana na mchango wake mkubwa upande wa elimu ya kawaida na ile ya dini, na vilevile upande wa uchungaji na wa upatanisho wa watu na watawala.

Mtawa wa Shirika la Wahubiri, anahesabiwa kuwa mwanafalsafa na mwanateolojia bora ya Ujerumani katika Karne za Kati. Alijitahidi kulinganisha imani na akili akiingiza falsafa ya Aristoteli katika Ukristo, jambo lililoendelezwa na mwanafunzi wake bora, Thoma wa Akwino.

Alberto, mtoto mdogo wa mtawala wa Bollstädt, alizaliwa Lauingen (Svevia, Ujerumani) lakini mwaka haujulikani: 1205, 1206 kama si 1193.

Vilevile hakuna hakika kuhusu elimu yake ya msingi, kama aliipata nyumbani au shuleni, lakini ujanani alitumwa kwenye chuo kikuu cha Padova (Italia), maarufu kwa masomo yaliyompendeza zaidi: lugha, hoja, hisabati, falaki na muziki.

Akiwa huko, alikuwa anahudhuria ibada katika kanisa la Wadominiko, ambao utakatifu wa maisha yao ulichangia, pamoja na uhusiano wake wa dhati na Mungu, kumfanya atamani kuwa mmojawao hata akaweza kushinda upinzani wa familia yake.

Mwaka 1223, baada ya kusikia hotuba ya mwenye heri Jordano wa Saksonia, mwalimu mkuu wa pili katika historia ya Shirika la Wahubiri, alijiunga na utawa huo ulioanzishwa na Dominiko Guzman. Jordano mwenyewe alimvika kanzu ya shirika.

Alipomaliza masomo yake, ama Padova ama kwingine, na kupata upadrisho, alitumwa kufundisha katika vituo vya teolojia vilivyounganika na konventi za shirika huko Hildesheim, Freiburg in Brisgau, Regensburg, Strasburg na Cologne, mmoja kati ya miji mikuu ya mikoa, ambapo aliishi kwa awamu kadhaa na hatimaye ukawa mji wake.

Alipokuwa katika konventi ya mji huo, akisoma *Liber Sententiarum* ya Petro Lombardo mwaka 1245, aliagizwa kwenda Paris (Ufaransa) alipojipatia digrii katika kituo kikuu cha huko, maarufu kuliko vyote upande wa teolojia.

Tangu hapo alianza kazi yake kubwa ya kuandika, mbali ya kutekeleza majukumu makubwa aliyozidi kupewa.

Akiwa safarini alisikilizwa na Thoma wa Akwino, kijana mkimya mwenye kutafakari, ambaye Alberto alitambua ukuu wa akili yake akamtabiria umaarufu wa kimataifa. Kati yao kukawa na heshima na urafiki mkubwa hadi mwisho. Huyo mwanafunzi mpya aliongozana naye hadi Paris halafu (1248) Cologne, ambapo Alberto alikuwa amechaguliwa kuwa gombera wa kwanza, wakati Thoma akawa mwalimu wa pili na *Magister Studentium* ("mwalimu wa wanafunzi").

Katika mkutano mkuu wa Wadominiko uliofanyika Valenciennes mwaka 1250, pamoja na Thoma na Petro wa Tarentaise, Alberto alitunga taratibu za masomo na za stahili shirikani.

Mwaka 1254 alichaguliwa mkuu wa kanda ya Ujerumani, wadhifa mgumu alioushughulikia vizuri sana. Alijitokeza kwa ari yake katika kutembelea jumuia za eneo lake kubwa, lililojumlisha Ulaya Kaskazini na Kati , huku akihimiza uaminifu kwa mafundisho na mifano ya Mt. Dominiko.

Mwaka 1256 alikwenda Roma ili kutetea mashirika ya Ombaomba dhidi ya mashambulizi ya Wiliamu wa Saint-Amour, ambaye kitabu chake *De novissimis temporum periculis* hatimaye kililaaniwa na Papa Aleksanda IV tarehe 5 Oktoba 1256.

Akiwa Roma, vipawa vyake viligunduliwa na Papa aliyetaka awe naye ili kufaidika na mashauri yake ya kiteolojia. Hivyo Alberto alishika nafasi ya mwalimu wa nyumba ya Papa na kufafanua Injili ya Yohane.

Mwaka 1257 alijiuzulu kama mkuu wa kanda ili ajitose kusoma na kufundisha.

Mwaka 1260, kwa uamuzi wa Papa huyohuyo, alipewa daraja takatifu ya uaskofu kwa ajili ya Jimbo la Regensburg, ambalo lilikuwa kubwa na maarufu, lakini wakati huo lilipitia matatizo mbalimbali. Basi, aliliongoza kwa bidii isiyokoma, akifaulu kurudisha amani mjini, kupanga upya parokia na nyumba za kitawa pamoja na kuchochea upya huduma za huruma.

Mwaka 1262 alijiuzulu, halafu miaka 1263-1264 alihubiri katika Ujerumani na Ucheki wa leo kwa agizo la Papa Urbano IV akarudia kazi ya kufundisha na kuandika huko Cologne.

Kama mtu wa sala, elimu na upendo, aliingilia kwa mafanikio matukio mbalimbali ya Kanisa na jamii: hasa alipatanisha watu wa Cologne na askofu mkuu wao aliyekuwa ameharibu sana.

Mwaka 1270 alimuandikia Thoma, aliyekuwa Paris, ili kumsaidia dhidi ya hoja za Sigieri wa Brabante na wafuasi wa Averroe. Ilikuwa kitabu cha pili dhidi ya huyo mwanafalsafa Mwarabu (cha kwanza kiliandikwa mwaka 1256 kwa jina *De Unitate Intellectus Contra Averroem*).

Mwaka 1274 aliitwa na Papa Gregori X ashiriki Mtaguso II wa Lyon, ambamo alifanya kazi kubwa ili kurudisha umoja kati ya Kanisa la Kilatini na lile la Kigiriki. Huko alipata taarifa ya kifo cha Thoma akasema, "Mwanga wa Kanisa umezimika".

Alijitokeza tena kwa nguvu mwaka 1277, ilipotangazwa nia ya Etienne Templier, askofu mkuu wa Paris, pamoja na wengine ya kulaani maandishi ya Thoma kama yenye uzushi. Ili kumtetea alifunga safari kwenda Paris kuyafafanua.

Mwaka 1278 (alipoandika wasia wake) alianza kusahausahau mambo, na mwili wake, uliodhoofishwa na maisha magumu ya kujinyima na ya kazi, ulizidi kushindwa na uzee hadi akafa tarehe 15 Novemba 1280 katika chumba chake konventini. Alizikwa katika kanisa la parokia ya Mt. Andrea ya Cologne.

Vitabu vyake vingi vinahusu fani zote za elimu ya wakati ule: mantiki, sayansi mbalimbali, elimunafsia, falsafa, maadili, siasa, teolojia, ufafanuzi wa Biblia n.k. Orodha yake inashangaza kwa upana wa mada alizozikabili kitaalamu. Ndiyo sababu Papa Pius XII alimpangia jina la “Doctor universalis” (yaani Mwalimu wa kila jambo).

Akiwa mtaalamu mkuu wa biolojia wakati wake, aliunganisha vizuri sayansi na ufunuo wa Mungu, falsafa na teolojia. Ulinganifu huo unamfanya awe karibu na watu wa leo katika maswali wanayojiuliza kuhusu asili na maendeleo ya ulimwengu.

Upana wa mawazo yake ulijitokeza hasa katika kuelekeza Kanisa lipokee falsafa ya Aristoteli katika ufafanuzi wa ulimwengu, kutokana na hakika ya kwamba kila kinachokubaliwa na akili nyofu kinapatana na imani katika ufunuo wa Mungu. Kwa namna hiyo Alberto aliwezesha falsafa kuwa fani inayojitegemea, ikishirikiana na kuunganika na teolojia katika umoja wa ukweli tu, bila kuchanganyikana.

Yeye alifaulu kushirikisha hata mawazo hayo kwa namna sahili na ya kueleweka, kama alivyofanya katika mahubiri aliyowapa watu wa kila kiwango cha elimu, waliovutiwa na maneno yake na mfano bora wa maisha yake.

Alitangazwa na Papa Gregori XV kuwa mwenye heri mwaka 1622, halafu na Papa Pius XI kuwa mtakatifu na mwalimu wa Kanisa tarehe 16 Desemba 1931.

Mwaka 1941 Papa Pius XII alimtangaza msimamizi wa wanasayansi.

Sikukuu yake inaadhimishwa kila mwaka tarehe 15 Novemba.

# Bonaventura (1217 hivi - 1274)



Bonaventura (Bagnoregio, Italia, 1217 hivi – Lyon, Ufaransa, 15 Julai 1274) alikuwa mtawa wa shirika la Ndugu Wadogo, halafu padri, askofu na kardinali.

Mtu wa sala na utendaji, alijitokeza hasa katika uongozi, ufundishaji na uandishi kama mmojawapo kati ya wale waliochangia zaidi ulinganifu wa imani na utamaduni katika karne XIII, ambapo Ukristo wa Magharibi ulizaa matunda bora hata upande wa elimu na sanaa mbalimbali.

Mwaka aliozaliwa haujulikani kwa hakika, bali ni kati ya 1217 na 1221. Mahali ni Civita di Bagnoregio, karibu na Viterbo, leo katika mkoa wa Lazio, Italia ya Kati.

Wazazi wake walikuwa mganga Yohane Fidanza na Maria wa Ritello; kwanza aliitwa kwa jina la baba yake, lakini alipoingia utawani aliitwa Bonaventura (yaani Bahati Njema). Inasemekana jina hilo lilikuwa shangilio la Fransisko wa Asizi alipomuona bado mtoto kabla hajamponya kimuujiza ulemavu wake baada ya kufa na kutangazwa mtakatifu.

Alizidi kumfahamu Fransisko alipokwenda Paris (Ufaransa) kwa masomo (1235) na kukuta huko Ndugu Wadogo waliokuweko tangu mwaka 1219. Baada ya kupata stashahada ya Arts, aliamua kujiunga nao, kwa kutambua kazi ya Kristo ndani ya tapo lao, akavikwa kanzu ya shirika mwaka 1243.

"Nakiri mbele ya Mungu kwamba kilichonifanya zaidi nipende maisha ya mwenye heri Fransisko ni kuwa yalifanana na mwanzo na ustawi wa kwanza wa Kanisa. Kanisa lilianza na wavuvi sahili, halafu likatajirika na walimu maarufu na wenye hekima sana; utawa wa mwenye heri Fransisko haukuanzishwa na busara ya watu bali na Kristo".

Aliendelea kusoma katika chuo kikuu cha Paris hadi mwaka 1253, akipata digrii ya Biblia na teolojia, halafu akafundisha huko (1253-1257) akifuata falsafa ya Plato na teolojia ya Augustino wa Hippo. Mazingira ya chuo hicho yalimwezesha kufahamiana na walimu na wanafunzi kutoka nchi mbalimbali za Ulaya na kustawisha mtazamo wake wa pekee, uliokuwa na Kristo kama kiini.

Upinzani wa maaskofu na maparoko dhidi ya Ndugu Wadogo na ya Wadominiko ulipoungwa mkono na chuo hicho hazikupingwa tu ruhusa kadhaa walizopewa, na haki yao ya kufundisha chuoni, bali msingi wenyewe wa mtindo wa maisha wao. Upya ulioletwa na mashirika hayo mawili haukueleweka kwa urahisi wakati huo, lakini pia kulikuwa na kijicho na wivu.

Baada ya Bonaventura na Thoma wa Akwino kuutetea kwa kuonyesha ulivyolingana na Injili, Papa Aleksanda IV alilaani upinzani na kusifu sana mtindo huo wa maisha (1257).

Mwaka huohuo mwalimu huyo kuchaguliwa kuwa Mtumishi mkuu wa shirika lake kukawa ushindi mwingine mkubwa chuoni.

Ni kwamba Mtumishi mkuu aliyemtangulia, Yohane wa Parma (1247-1257), alipoamua kujiuzulu, hakurudi nyuma ingawa mkutano mkuu ulitaka aendelee. Hatimaye walimuomba walau amchague mwandamizi wake, naye akamtaja Bonaventura, mtu wa Mungu na wa watu, mwema kwa wote na mwenye kipawa cha uongozi.

Kufuatana na tabia yake chanya, alikubali hali halisi ya shirika na kujitahidi kuliepusha na hatari za nje na za ndani alizoziona mapema kabla hajachaguliwa.

Basi, kwa miaka 17 (1257-1274) alikuwa Mtumishi mkuu wa shirika, akatembelea na kuwaandikia barua ndugu zake za kiroho, waliokuwa tayari zaidi ya 30,000 na kuenea Ulaya, Afrika Kaskazini, Mashariki ya Kati na hata China, akijitahidi kudumisha umoja kwa kulinganisha misimamo tofauti ya watawa walioelekea zaidi sala na ufukara na ya wale walioelekea zaidi elimu na utume.

Chini yake mkutano mkuu wa Narbone (1260) ulitunga katiba maarufu ambayo ilikusanya na kusawazisha taratibu za maisha ya kila siku ikawa msingi wa katiba za karne zilizofuata. Lakini alijua kwamba sheria haziwezi kutosha zisipoendana na umoja wa vipeo na malengo.

Mzizi wa uongozi wake ulikuwa daima sala na tafakuri. Muungano na Kristo ulimfanya asiishie kuagiza, bali aangaze watawa na kuwaleta kwa Yesu. Hivyo vitabu mbalimbali vya maisha ya Kiroho alivyoviandika vinatokeza namna yake ya kuongoza.

Kati yake, maarufu zaidi ni "Itinerarium Mentis in Deum" (yaani "Safari ya Akili kwa Mungu"), kinachoongoza kwa hatua sita kutoka ujuzi wa Mungu unaopatikana kwa kuchunguza ulimwengu na vipawa vya roho yetu hadi shibe ya muungano na Utatu kumpitia Kristo, kama alivyojaliwa Fransisko.

Sawa na huyo, Bonaventura alifurahia uzuri wa viumbe, alivyoandika mwanzoni mwa kitabu: "Asiyeangazwa na mng'ao huo wa vitu vilivyoumbwa ni kipofu; asiyeamshwa na kelele hiyo ni kiziwi; asiyemsifu Mungu kwa kazi hizo zote ni bubu; asiyegeukia Asili Kuu kutokana na maelekezo hayo ni mpumbavu".

Ulimwengu wote unatangaza upendo wa Mungu mwema, na maisha ya binadamu ni safari ya kumuendea. Lakini hawawezi kupanda kwake kwa nguvu zao bila kuvutwa naye. Ndiyo sababu sala ni ya lazima kama mama na chanzo cha kwenda juu.

Karibu na mwisho aliandika: "Ukitaka kujua jinsi mambo hayo yote yanavyotokea, uiulize neema, si elimu; uiulize hamu, si akili; uuulize mlio wa sala, si juhudi ya kusoma; umuulize bwanaarusi, si mwalimu; umuulize Mungu, si mtu; uuulize ukungu, si weupe; usiulize mwanga, bali moto unaowasha nafsi yote na kuizamisha ndani ya Mungu kwa mpako wake tamu sana na mapendo motomoto zaidi".

Mashambulizi ya kutisha yalitokea pia ndani ya shirika, upande wa ndugu "wa Kiroho" walioelekea kufuata uzushi wa abati Yohakimu wa Fiore, aliyefariki mwaka 1202, baada ya kutabiri umonaki mpya utakaoleta hali mpya katika Kanisa na jamii. Hao walidhani Ndugu Wadogo ndio waliotimiza utabiri huo wakajiona hawahitaji tena kuwa chini ya miundo ya zamani, wala chini ya uongozi wa shirika na wa Kanisa, kinyume cha utiifu mnyenyekevu wa Fransisko.

Dhidi ya upotoshaji huo, Bonaventura alisoma kwa makini maandishi yote ya abati huyo, na hatimaye akawafafanulia wanashirika wa Paris teolojia ya historia kwa usahihi. Mafundisho yake hayakutimia ila yalikusanywa na wasikilizaji katika kitabu "Hexaëmeron", yaani ufafanuzi wa uumbaji kwa siku sita ambazo toka zamani zilitazamwa kumaanisha vipindi sita vya historia.

Hata hivyo yeye alivitafsiri upya kwa kumuonyesha Kristo kama kiini cha historia, si mwisho wake. Ndiyo sababu karne XIII ilipiga hatua kubwa upande wa ujuzi, wa utakatifu na wa umisionari vilevile, hasa kwa njia ya mashirika mapya ya Ombaomba. Karama ya Fransisko ilithibitisha kwamba Kristo anaweza kusababisha daima hali mpya kwa njia ya Roho Mtakatifu.

Basi, ndani ya Kanisa lilelile kuna maendeleo, na teolojia yenyewe haiwezi kuishia katika kurudiarudia tu mafundisho ya mababu wa Kanisa. Kwake teolojia inalenga hasa hekima, nayo inakumbatia kwanza ujuzi unaopatikana hasa kwa sala, halafu wema unaotokana na ujuzi huo kupitia matendo. "Imani imo akilini namna ambayo inasababisha mapendo".

Kwa mfano, ujuzi wa kwamba Kristo alikufa kwa ajili yetu haubaki ujuzi, bali unakuja kugeuka upendo. Ni upendo huo, si kiburi cha akili, unaotakiwa kuchochea teolojia kwa lengo la kuzidi kumjua Mpenzi. Hivyo kwa Bonaventura upendo unashika nafasi ya kwanza, kwa kuwa lengo la binadamu ni kuungana na Mungu katika upendo, na humo kupata heri.

Katika msimamo huo na katika teolojia yake yote aliathiriwa sana na Fransisko aliyechanganyikiwa na Yesu na kuwaka moto kama Serafi, aina bora ya malaika kadiri ya Pseudo-Denis. Katika maandishi ya Msiria huyo wa karne VI Bonaventura alichota hasa wazo la kwamba, katika kumuelekea Mungu, mtu anaweza akafikia hatua ambapo akili haioni tena, ila upendo unakwenda mbele na kupenya fumbo la Mungu. Hilo linalingana kabisa na karama ya Kifransisko inayopita michakato ya akili kwa kumpenda Kristo msulubiwa.

Katika uongozi wake, Bonaventura alijipangia kulinganisha uaminifu kwa kanuni na mabadiliko shirikani, akionyesha hayo hayaendi kinyume cha nia ya mwanzilishi. Kwa ajili hiyo ilimpasa kuziondolea lawama za hao

ndugu “wa Kiroho” msingi wowote kwa kupigania uaminifu kwa wito wa shirika. Mwenyewe alikubali kwa moyo matamko ya Mapapa juu ya kanuni kama ufafanuzi rasmi wa wachungaji wakuu wa Kanisa na wa shirika pia.

Kielelezo cha Fransisko wa Asizi kilitakiwa kuzingatiwa na wote kwa umoja, bila kupishana kuhusu namna ya kukitazama. Kwa ajili hiyo alitunga kitabu rasmi cha maisha yake kilichopitishwa na mkutano mkuu hata ukaagiza maandishi yote yaliyotangulia juu ya Fransisko yateketezwe. Ndivyo shirika lilivyopotewa kwa muda mrefu na habari nyingi muhimu juu ya mwanzilishi.

Bila kusema uongo, kitabu alichokiandika (“Legenda Maior”, kilichofupishwa katika “Legenda Minor”) kinaleta baadhi tu ya matendo na mafundisho ya Fransisko yaliyochaguliwa kwa makini ili kumchora kama mfano kamili wa Yesu msulubiwa na kusisitiza mang’amuzi yake bora ya kiroho, lakini kwa kuficha mambo fulanifulani kuhusu kipeo cha udogo.

Aliheshimu ufukara kama sifa kuu na utukufu wa shirika, ingawa alikubali mabadiliko yaliyotokea, yaani konventi kubwa mijini n.k. Kwake elimu pamoja na utume ni sehemu ya lazima ya utendaji wa Kifransisko. Kwa ajili hiyo alikubali ruhusa lilizopewa shirika, ingawa kwa udogo alipenda kupatana na maaskofu na maparoko.

Basi, chini ya uongozi wake shirika likatulia, kwa jinsi alivyoweza kulinganisha upendo kwa Fransisko na furaha kwa mabadiliko, hamu ya kuishi upwekeni muda mrefu pamoja na ndugu “wa Kiroho” na utetezi wa konventi za mijini.

Baada ya kuteuliwa na Papa Gregori X kuwa kardinali mnamo Mei 1273, akiwa askofu wa Albano Laziale, kwa agizo lake aliandaa kwa bidii Mtaguso II wa Lyon ulioanza mwaka 1274 hasa kwa lengo la kurudisha umoja kati ya Wakatoliki na Waorthodoksi, lakini katikati yake akafa, na muungano uliofikiwa ukaja kuvunjika tena.

Mwaka 1434 walipohamisha masalia yake, walikuta kichwa hakijaoza. Jambo hilo liliharakisha hatua ya kumtangaza mtakatifu iliyochukuliwa na Papa Sisto IV tarehe 14 Aprili 1482.

Halafu tarehe 14 Mei 1588 akatangazwa na Papa Sisto V kuwa mwalimu wa Kanisa kwa jina la Doctor Seraphicus, yaani Mwalimu wa Kiserafi. Hilo lilitokana na umotomoto wa upendo, uliokuwa tunda la maisha yake ya sala ya dhati na unaojitokeza katika maandishi yake mengi.

Sikukuu yake inaadhimishwa kila mwaka tarehe 15 Julai.

## Thoma wa Akwino (1225 hivi - 1274)



Thoma wa Akwino (Roccasecca, katika eneo la watawala wa Aquino, leo katika wilaya ya Frosinone, Italia, 1224 au 1225 - Fossanova, wilaya ya Latina, Italia, 7 Machi 1274) alikuwa mtawa wa Shirika la Wahubiri na padri wa Kanisa Katoliki.

Mnyofu, mkimya, aliyekuwa tayari kutumikia, kiutu alipendwa na wote, naye alipendelea watu wa chini, akihubiria mafukara kwa usahili na wema hata zaidi ya mara moja kwa siku.

Kuliko wengine wote, Thoma aliona elimu na masomo kama njia ya kufikia utakatifu; ni kati ya watu bora upande wa nadharia, hasa wa teolojia ya shule, iliyofikia kilele chake katikati ya karne XIII.

Mwanafunzi wa Alberto Mkuu, alitumia hasa mawazo ya mwanafalsafa wa Ugiriki Aristoteli, na ya Waarabu waliomtafsiri, lakini pia ya Plato: ili kufafanua imani, alikubali ukweli ulioweza kutolewa na yeyote, kwa sababu kweli zote zinatoka kwa Mungu; kinyume chake alikanusha udanganyifu wowote.

Hivyo aliweza kufanya usanisi mpana ambao mpaka leo Kanisa Katoliki linautambua kama tokeo bora la mafundisho yake lenyewe na kama kielelezo cha namna ya kufikiri na ya kufanya teolojia.

Anajulikana hasa kwa vitabu vyake "Jumla ya Teolojia" (kwa Kilatini *Summa Theologiae*) na "Jumla Dhidi ya Wapagani" (*Summa Contra Gentiles*).

Alizaliwa na Landolfo, sharifu mwenye asili ya Kilombardi, na mke wake, Teodora, katika ngome ya familia yao.

Akiwa mtoto wa miaka 5 tu, alitumwa kuishi na Wabenedikto katika abasia jirani ya Monte Cassino ili apate malezi ya msingi kwa watawa.

Alipofikia umri wa miaka 14 alihamia Napoli, mji mkuu wa Ufalme wa Sicilia, aliposoma katika chuo kikuu maarufu kilichoanzishwa na Kaisari Federiko II. Humo mawazo mbalimbali kama yale ya Aristoteli yalifundishwa bila vizuio vilivyokuwepo sehemu nyingine.

Basi, Thoma alianza kutambua thamani ya falsafa ya Mgiriki huyo iliyokuwa imesahaulika kwa muda mrefu lakini wakati huo ilikuja inajulikana upya kupitia wafafanuzi wake wa Kiarabu, Avisena na Averoe.Ilikuwa na mpango mzima wa mawazo kuhusu ulimwengu, roho na maadili ambao ulikamilika kabla ya Kristo kwa kutumia akili tu, na ambao ulionekana kujitosheleza na kuridhisha kama mtazamo sahihi.

Jambo lingine muhimu la miaka hiyo ni kwamba alikuwa karibu na konventi ya Mt. Dominiko akavutiwa na karama ya shirika lililoanzishwa na mtakatifu huyo. Ingawa alipingwa sana na familia, mwaka 1244 aliamua kujiunga na Wadominiko.

Wakubwa wa shirika, kisha kuhisi ukuu wa akili yake, walimtuma Paris aweze kukamilisha masomo yake, lakini kabla hajafika huko alikamatwa na wanafamilia na kufungwa katika ngome ya baba yake huko Monte San Giovanni Campano alipokaa mwaka mzima, akishinikizwa aoe.

Hatimaye, akiwa amefikia umri wa kujiamulia maisha, alitoroka au alifunguliwa kwa ombi la Papa Inosenti IV.

Baada ya kukaa kidogo Napoli na Roma, alifika Paris ili kufundishwa na Alberto Mkuu, mwanasayansi, mwanafalsafa na mwanateolojia wa shirika lake.

Mapema walianza kuheshimiana na kupendana, hivyo mwaka 1248 Thoma alimfuata Alberto huko Cologne (Ujerumani) alipokuwa ametumwa na viongozi wa shirika aanzishe kituo cha teolojia.

Baadaye, Thoma aliamua kutekeleza mpango wa mwalimu wake wa kulinganisha Ukristo na falsafa ya Aristoteli iliyokuwa inazidi kuathiri Ulaya Magharibi na ustaarabu wake uliotegemea imani, ingawa wengine waliipinga falsafa hiyo hasa kwa sababu wafafanuzi wake wa Kiarabu walikuwa wameipendekeza tofauti, wakisema, k.mf., kwamba ulimwengu ni wa milele kama Mungu.

Hapo Thoma alifanya jambo la maana sana kwa historia yote ya falsafa, teolojia na elimu kwa jumla: kusoma kikamilifu vitabu vya Aristoteli na vya wafafanuzi wake, kisha kujipatia tafsiri mpya kutoka Kigiriki ili asitegemee tu walivyoelewa Waarabu hao.

Hapo alifafanua mwenyewe sehemu kubwa ya maandishi ya Aristoteli, akitofautisha kweli za kudumu zilizomo, mambo yanayotia shaka na yale yasiyo sahihi kabisa, akionyesha yanavyolingana na Ufunuo wa Kimungu na jinsi yanavyoweza kutumika katika teolojia ya Kikristo.

Kifupi, Thoma alithibitisha hivyo ulinganifu wa imani na hoja za akili, wakati ambapo hizo mbili zilionekana kupingana moja kwa moja, hata kusababisha watu wajione ni lazima waachane na imani na kufuata akili.

Kwa usanisi huo, Thoma aliunda msimamo wa karne zijazo, kwamba kweli haziwezi kupingana kamwe; ikionekana hivyo maana yake ama akili imekosea katika hoja zake, ama kinachodaiwa kuwa ukweli wa imani hakifundishwi nayo.

Kutokana na vipawa vyake kuanzia mwaka 1252 aliitwa kufundisha teolojia kwenye Chuo kikuu cha Paris, akianza kama *baccalarius biblis*, na baada ya miaka 4 aliweza kufundisha kama profesa.

Wakati huo Thoma alianza kazi ya kutunga vitabu ambayo aliendelea nayo hadi karibu na kifo na ambayo ni ya ajabu hata tukizingatia kwamba alisaidiwa na karani kadhaa, kati yao akiwemo hasa rafiki yake Rejinaldo wa Piperno.

Alipinga falsafa ya wafuasi wa Mwarabu Averroe waliosema imani haiwezi kupatana na akili: "Imani ni kwa watu wanyofu, falsafa ni kwa wasomi".

Thoma alipambana pia na Waagustino ambao walifuata falsafa ya Plato hata kusema ile ya Aristoteli haipatani na imani.

Mwaka 1259 alishiriki mkutano mkuu wa shirika huko Valenciennes, akaingizwa katika jopo la kupanga masomo ya Wadominiko wote.

Baadaye alirudi Italia na kushirikiana na Papa Urbano IV, akiishi kwenye konventi ya Orvieto (1261-1265).

Kwa agizo lake, Thoma alitunga au kupanga matini ya liturujia yote ya sikukuu mpya ya *Corpus Domini* (Mwili na Damu ya Kristo) iliyoanzishwa tarehe 8 Septemba 1264. Kati ya matini hayo, ambamo zinajitokeza imani na hekima yake, maarufu zaidi kimataifa mpaka leo ni utenzi *Pange Lingua*, hasa sehemu ya mwisho inayoanzia na maneno *Tantum Ergo (Sakramenti Kubwa Hiyo)*.

Waliomfahamu walisisitiza heshima yake kwa fumbo la Ekaristi; pengine alikuwa akiegemeza kichwa chake penye tabenakulo, kama kwa kusikia mapigo ya Moyo wa Yesu na kupata majibu ya maswali magumu aliyojiuliza. Akiadhimisha Misa aliweza akalia machozi ya huruma, furaha na shukrani kwa Bwana aliyejitoa kafara kwa ajili ya binadamu. “Kwa kuwa hii ndiyo sakramenti ya Mateso ya Bwana wetu, ndani yake ina Yesu aliyeteseka kwa ajili yetu. Basi, tokeo lolote la Mateso ya Bwana wetu ni pia tokeo la sakramenti hii.”

Halafu alihamia Roma (1265-1268) ili kuongoza chuo cha Mt. Sabina; ila katikati, mwaka 1267 Papa Klemens IV alimuita kwake Viterbo, alipohubiri mara nyingi katika kanisa la Santa Maria Nuova.

Akiwa Italia ndipo alipoandika vitabu vingi kama vile *Summa Contra Gentiles*, *De Regimine Principium*, *De Unitate Intellectus Contra Averroistas* na sehemu kubwa ya kazi yake bora, *Summa Theologiae*, inayotumika hadi leo katika teolojia, kama ilivyoagizwa na Mtaguso II wa Vatikano katika hati mbili, Optatam Totius na Gravissimum Educationis.

Mwaka 1269 alirudishwa Paris; huko wanafunzi wake walikuwa wengi hata kujaza kabisa ukumbi; mmojawao alishuhudia kwamba, “kumsikiliza kulimjaza heri ya dhati”. Hata waliompinga walikiri mafundisho yake ni bora na yanasahihisha yale ya walimu wengine.

Huko akaanza pia kutetea kiteolojia mashirika ya Ombaomba na kupinga Uplato mpya wa Waagustino.

Mwaka 1272, akiitwa na mfalme Karolo I wa Angiò, alirudishwa Napoli na kupanga upya masomo ya teolojia kwenye chuo kikuu karibu na konventi yake asili. Huko alijitosa pia kuhubiria watu wa kawaida, nao walimiminika kumsikiliza. Mahubiri ya Kwaresima yake ya mwisho, aliyoyatoa katika kanisa la Mt. Dominiko, yametunzwa kwa jina la “Opusculi” (yaani “Vijitabu”). Humo tunasoma alivyofafanua kwa usahili Kanuni ya Imani ya Mitume, sala ya Baba Yetu, Amri Kumi na sala ya Salamu Maria.

Kwa mfano, kuhusu imani, alieleza thamani yake: kwa njia yake roho inaungana na Mungu na kuzaa uzima wa milele; maisha yanapata mwelekeo wa kufaa nasi tunashinda vishawishi kwa urahisi.

Dhidi ya hoja ya kwamba imani ni upumbavu kwa sababu inamfanya mtu asadiki kitu kisichofikiwa na hisi zake, Thoma alijibu kwamba akili yetu ina mipaka, haiwezi kujua yote. Ingeweza kufahamu kikamilifu mambo yote yanayoonekana na yasiyoonekana, hapo tu ingekuwa upumbavu kukubali ukweli fulani kwa imani. Kumbe hatuwezi kuishi bila kutegemea ushahidi wa wengine kila tunaposhindwa kujua kitu wenyewe. Kama ni hivyo, basi, inafaa tumsadiki Mungu anayejifunua na pia ushahidi wa Mitume wa Yesu. Ni kati ya maajabu ya historia kwamba mapema watu wengi wenye mali na hekima waliwasadiki hao watu wachache, fukara na wanyofu waliovunjwa moyo na kifodini cha mwalimu wao. Lisingetokea kama wasingekutana naye mfufuka.

Thoma alieleza pia kwamba tafakuri juu ya umwilisho wa Mwana wa Mungu inaimarisha imani na tumaini kwa wazo la ujio wake kati yetu kama mmojawetu kwa lengo la kuwashirikisha watu umungu wake; pia inachochea upendo kwa sababu hakuna ishara wazi zaidi ya upendo wa Mungu kuliko kumuona Muumba wa ulimwengu kujifanya kiumbe kama sisi; hatimaye inawasha hamu ya kumfikia Kristo katika utukufu: “Kama ndugu wa mfalme angeishi mbali sana naye, bila shaka angetamani kuishi karibu naye. Basi, Kristo ni ndugu yetu; kwa hiyo tunapaswa kutamani tuwe naye na kuwa moyo mmoja naye”.

Akifafanua Baba Yetu, alionyesha ni sala kamili kutokana na kuwa na sifa tano zinazohitajika: tumaini tulivu, maombi ya kufaa, mpangilio mzuri wa maombi, ari ya upendo na unyofu wa unyenyekevu.

Kuhusu Bikira Maria, alimuita "Triclinium totius Trinitatis", yaani "mahali ambapo Utatu Mtakatifu unastarehe", kwa maana Nafsi tatu za Mungu hazifurahii kukaa ndani ya mtu yeyote kuliko ndani ya roho yake iliyojaa neema.

Miezi ya mwisho ya maisha yake iliathiriwa na tukio la pekee lililofanya azidi kuzama katika tafakuri. Ni kwamba tarehe 6 Desemba 1273, katika kanisa la Mt. Dominiko, alitoka nje ya nafsi yake na tangu siku hiyo aliacha kuandika, akimueleza kwa unyenyekevu ndugu Reginaldo wa Piperno, msaidizi na muungamishi wake: ""Yale yote niliyoyaandika naona ni fungu dogo la majani makavu kulingana na yale ambayo nimeyaona na kufunuliwa. Ndio mwisho wa kuandika kwangu na natumaini umekaribia pia mwisho wa maisha yangu"."

Ndiyo sababu *Summa Theologiae* haikukamilika (inaishia kwenye mada ya *Kitubio,* baada ya kukabili masuala 512 katika hoja 2,669 kwa kuchimba mafundisho ya Biblia na ya mababu wa Kanisa, hasa Augustino).

Humo Thoma anazingatia kwanza kwamba Mungu yupo kwa namna tatu: 1) ndani mwake, akiwa asili na lengo la vyote, hivi kwamba viumbe vyote vinatokana naye na kumtegemea; 2) kwa njia ya neema katika uhai na utendaji wa watu anaowatakasa; 3) kwa namna ya pekee kabisa katika nafsi ya Kimungu ya Mwana iliyounganika kweli na ubinadamu wa Yesu na inayotenda katika sakramenti zinazotokana na kazi yake ya ukombozi.

Ndiyo sababu kitabu hicho kikubwa kimegawanyika katika sehemu tatu: "Kwa kuwa lengo kuu la teolojia ni kufundisha ujuzi wa Mungu, si tu jinsi alivyo mwenyewe, bali pia kama asili na lengo kuu la vitu, na hasa la viumbe wenye akili, ilivyo wazi katika yale tuliyoyasema tayari, basi tutafafanua: 1) Mungu; 2) maendeleo ya kiumbe mwenye akili kumuelekea Mungu; 3) Kristo ambaye kama mtu ndiye njia yetu kwa Mungu".

Ni kama duara inayorudi ilipoanzia: Mungu alivyo anajitokeza kwa nje na kutushika mkono hivi kwamba pamoja na Kristo tumrudie yeye na kuungana naye awe yote katika wote.

Sehemu ya kwanza ya Summa Theologiae inamchunguza Mungu mwenyewe, fumbo la Utatu na kazi yake ya kuumba. Humo tunakuta tafakuri ya dhati juu ya mtu pia, kama kiumbe aliye tunda la upendo wake. Uhai wetu unamtegemea Mungu, lakini ni wa kweli kwa sababu yeye ametaka kututia thamani.

Sehemu ya pili inazidi kumzingatia mtu ambaye, akisukumwa na neema, anatamani kumjua na kumpenda Mungu ili awe na heri sasa na milele. Thoma anafafanua kiteolojia matendo maadilifu, ambayo yanachangiwa na akili, utashi na maono ya mtu, pamoja na uwezo wa neema ya Mungu kupitia maadili na vipaji vya Roho mtakatifu, mbali ya msaada wa sheria yake. Kwa msingi huo, Thoma anamchora mtu ambaye anaongozwa na Roho Mtakatifu na hivyo kuwa mfano wa Mungu. Hapo anasimama kufafanua maadili matatu ya Kimungu na zaidi ya maadili hamsini ya kiutu, yanayotegemea maadili bawaba manne. Hatimaye anatafakari juu ya miito mbalimbali yaliyopo ndani ya Kanisa.

Sehemu ya tatu inachunguza fumbo la Kristo, aliye njia na ukweli, ambalo linatuwezesha kumfikia Mungu Baba. Humo Thoma anaeleza vizuri ajabu umwilisho na Mateso ya Yesu, akiongeza maelezo marefu kuhusu sakramenti ambazo Kristo anatushirikisha faida ya ukombozi. Akitumia vitu alivyochagua, anatugusa mpaka ndani.

Asubuhi moja, Thoma alipokuwa anasali mbele ya Msalaba wa kikanisa cha Mt. Nikola mjini Napoli, mtunzasakristia Dominiko wa Caserta alisikiliza maongezi yake na Yesu. Thoma alikuwa anauliza kwa fadhaiko kama aliyoyaandika kuhusu mafumbo ya imani ni sahihi au sivyo. Msulubiwa alimjibu: "Umeandika vema juu yangu, Thoma. Unataka tuzo gani?" Hapo Thoma alisema, "Si kitu kingine, ila wewe mwenyewe".

Mnamo Januari 1274 Papa Gregori X alimuagiza ashiriki Mtaguso II wa Lyon, na Thoma akafunga safari ingawa hali yake haikuwa nzuri.

Alilazimika kusimama kwenye ngome ya Maenza, lakini alipoona hali inazidi kuwa mbaya asiweze kufikia konventi ya shirika, akitaka kufia monasterini, aliagiza aletwe kwenye abasia ya Wasitoo ya Fossa Nuova (leo Fossanova, karibu na Priverno), ambapo alifariki baada ya wiki chache.

Masalia yake yanatunzwa katika konventi ya Wadominiko *des Jacobins* huko Tolosa (Ufaransa).

Alitangazwa na Papa Yohane XXII kuwa mtakatifu tarehe 18 Julai 1323, halafu na Papa Pius V kuwa mwalimu wa Kanisa mwaka 1568. Kwa Kilatini anaitwa Doctor Angelicus (Mwalimu wa Kimalaika) au Doctor Communis (Mwalimu wa wote).

Ni msimamizi wa wanateolojia, wanachuo, watoaji na wauzaji wa vitabu, wanafunzi na shule. Sababu si mafundisho yake tu, bali mbinu alizozitumia katika kusanisi falsafa na teolojia bila kuzichanganya kama ilivyotokea kabla yake. Falsafa kama ile ya Aristoteli iliweza kujitegemea katika hoja zake, badala ya kumezwa na teolojia ambayo ilitegemea imani katika Ufunuo wa Mungu na kuja kukamilisha falsafa pale ambapo hiyo haiwezi kufika.

Msingi wa hakika hiyo ya Thoma ni kwamba falsafa na teolojia vilevile zinatokana na chanzo cha kweli zote, ambacho ni Neno wa Mungu, aliyehusika na kazi ya uumbaji na ya ukombozi pia. Ingawa fani hizo zinafuata taratibu tofauti katika kulenga ujuzi sahihi, hazitakiwi kutengana, bali kushirikiana.

Kadiri yake, kwa mfano, akili ya binadamu kwa njia ya hoja inaweza kufikia hakika kuhusu uwepo wa Mungu mmoja, ila imani tu, kwa kupokea Ufunuo kutoka juu, inaweza kuchota katika fumbo la Upendo wa Mungu Utatu.

Wakati imani inakamilisha ujuzi wa akili, hoja pia inasaidia imani kwa namna tatu: "kwa kuthibitisha kweli zinazoandaa kusadiki; kwa kufafanua wazi zaidi kweli za imani kwa njia ya mifano kadhaa; kwa kupinga wale wanaosema dhidi ya imani, ama kwa kuonyesha kauli zao ni za uongo, ama kwa kuonyesha si hakika kuwa za kweli".

Ulinganifu huo wa msingi kati ya hoja za akili na imani ya Kikristo unajitokeza tena katika wazo lingine muhimu la Thoma: kwamba neema ya Mungu haibatilishi umbile la binadamu, bali inalitumia na kulikamilisha. Hiyo ni kwa sababu, hata baada ya kutenda dhambi, umbile hilo halijaharibika kabisa, ila limejeruhika na kudhoofika. Neema ambayo tunakirimiwa na Mungu na kushirikishwa kwa njia ya Neno aliyefanyika mwili, ni zawadi tu ya hiari yake ambayo umbile letu linaponywa, linatiwa nguvu na kusaidiwa lifikie heri ile linayotamani tu kwa dhati, hata bila kutambua na kuamua. Vipawa vyote vya mtu vinatakaswa, vinageuzwa na kuinuliwa na neema ya Mungu.

Fundisho hilo juu ya uhusiano wa umbile na neema ndani mwetu linatumiwa hasa katika maadilidini ya Thoma. Kiini chake ni sheria mpya, ambayo ni Roho Mtakatifu, yaani neema yake wanayopewa wale wanaomuamini Kristo. Mafundisho yote ya Kanisa kuhusu imani na maadili yameunganika na neema hiyo ambayo ni ya msingi katika kuishi kwa uadilifu: kutoka kwake yanapatikana maadili ya Kimungu na ya kiutu. Hivyo Wakristo wote wanaweza kufikia ukamilifu uliopendekezwa na Yesu katika hotuba ya mlimani, ikiwa wanaishi naye katika uhusiano wa imani na wako wazi kupokea kazi ya Roho Mtakatifu.

Pamoja na hayo, "ingawa neema ina nguvu kuliko umbile, hata hivyo umbile linamhusu mtu zaidi, na kwa hiyo ni la kudumu zaidi". Ndiyo maana kuna nafasi kwa hoja za akili katika kutambua maadili yanayodaiwa na utu kwa jinsi ulivyo. Akili inaweza kuyatambua kwa kutofautisha yanayofaa na yasiyofaa kufikia ile heri inayotamaniwa na mioyo yetu.

Hayo yanahusika pia na majukumu kwa ajili ya wengine, mmojammoja na kwa jumla (ustawi wa jamii). Watungasheria wanapaswa kuzingatia hayo katika kazi yao ya kuratibu maisha ya jamii. Ndio msingi wa kuorodhesha na kutetea haki za binadamu. Si ajabu kwamba fundisho la hadhi ya nafsi ya mtu, inayomfanya kila mmoja awe na haki za msingi kwa sababu tu ni mtu, lilistawi kwanza kati ya waliozingatia urithi wa Thoma katika kuthamini umbile letu: "ndilo lililo kamili kuliko yote yanayopatikana ulimwenguni, yaani mmoja anayeishi akiwa na akili".

Basi, Thoma alipendekeza mtazamo mpana na lenye tumaini kuhusu akili ya binadamu. Mpana kwa sababu hauishii katika ujuzi wa sayansi zinazotegemea upimaji wa vitu vinavyoonekana, bali unakabili yote yaliyopo, kuanzia Mungu, na hivyo unahimizwa kutafuta maana ya maisha yetu. Lenye tumaini kwa sababu akili, hasa ikiangazwa na imani ya Kikristo, inapigania ustaarabu ambao unathamini hadhi ya kila mtu, unatetea haki zake pamoja na kumhimiza kuwajibika kwa wengine.


Dhati ya mawazo ya Thoma ilitokana daima na maisha yake ya imani na sala yaliyojitokeza katika maneno kama haya: "Ee Bwana, Mungu wangu, unijalie akili ya kukufahamu, moyo wa kukutafuta, hekima ya kukupata, mwenendo wa kukupendeza, udumifu mwaminifu katika kukutarajia, na tumaini la kukukumbatia mwisho".

Sikukuu yake inaadhimishwa kila mwaka tarehe 28 Januari.

**Kwa Kiswahili**

GEROLD SCHMID, Toma na Marieta – ed. Benedictine Publications Ndanda-Peramiho – Peramiho 1978

## Katerina wa Siena (1347 - 1380)



Katerina Benincasa wa Siena alikuwa mwanamke mwenye vipaji na karama za pekee aliyemfuata tangu ujanani Yesu Kristo katika familia ya kiroho iliyoanzishwa na Dominiko Guzman.

Ingawa hakusoma, alishika nafasi muhimu katika historia ya Kanisa, akisababisha wongofu na urekebisho, na katika historia ya Italia, akileta amani wakati wa vita na fujo nyingi za siasa.

Katerina alizaliwa Siena, Italia, tarehe 25 Machi 1347 kama mtoto wa 24 kati ya 25 wa Jacopo Benincasa na Lapa Piagenti (au Piacenti). Pacha wake Giovanna (kitindamimba) aliishi miezi tu.

Mwaka uliofuata (1348) Siena na Ulaya kwa jumla zilipatwa na tauni iliyopunguza sana idadi ya watu.

Alisimulia kwamba alipokuwa na miaka sita alianza kupata njozi na akiwa na miaka saba aliweka nadhiri ya ubikira akianza safari ya toba yenye saumu na malipizi mengine.

Kwenye umri wa miaka 12 wazazi, wasiojua nadhiri yake, walianza kufikiria wamuoze. Katerina aliitikia kinyume hata kwa kunyoa kipara na kujifungia nyumbani. Ili kumshurutisha wazazi walimuagiza kazi nzito nyingi, lakini bure.

Siku moja baba alimkuta akisali ana njiwa akielea kichwani pake. Hapo alikubali kumuacha huru ajichagulie maisha.

Alipokuwa na miaka 16, baada ya kutokewa na Dominiko Guzman, alijiunga na Utawa wa Tatu wa Mt. Dominiko, ambao wanachama wanawake walijulikana kama “Mantellate” kwa sababu ya kuvaa joho maalumu. Hapo alirudia nadhiri yake ya ubikira na kushika maisha magumu ya sala, malipizi na huduma za huruma, hasa kwa wagonjwa, bila kuhama nyumbani.

Sifa ya kuwa mtakatifu ilienea hata kandokando yake walikusanyika marafiki wengi kama kundi la wanafunzi wake wa kiroho, wakiwemo watu wa kila aina, hata masharifu, wanasiasa na wasanii, mbali ya watawa wa kiume na wa kike.

Hao walimuita “mama” kwa kuwa aliwalisha kiroho kwa mamlaka iliyotokana na ubora wa maisha yake na iliyothibitishwa na majaliwa ya pekee waliyoyashuhudia, kama vile kutoka kwake nje ya nafsi mara nyingi. Naye aliwaelekea kama watoto, akiwaandikia k.mf. mapadri watawa: “Mpendwa sana na wa thamani kwangu ndugu na mwana katika Kristo Yesu mtamu”. “Kwa vile nilikuzaa kwa sala za kudumu na hamu mbele ya Mungu, kama mama anavyozaa mtoto”.

Alijaribu kusoma vitabu vitakatifu bila kufundishwa, mpaka akajaliwa kipawa cha kusoma. Baadaye tena akajaliwa kuandika, lakini maandishi yake mengi aliyaandikisha tu.

Kati yake, muhimu zaidi ni “Maongezi ya Maongozi ya Mungu”. Humo tunakuta mafundisho ya hali ya juu, iliyojaa matunda ya sala yake ya dhati. Pia tuna mikusanyo ya barua na sala zake.

Katika kipindi hicho cha vurugu tele, alisafiri sana na kutuma mara nyingi ujumbe wake wa amani kwa miji na makundi yaliyogombana, akilenga daima upendo na umoja.

Alisimulia kwamba kabla ya Kwaresima ya mwaka 1367 alitokewa na Yesu akiwa pamoja na Bikira Maria na watakatifu wengine ili kumuoa kiimani, akamvika pete yenye rubi aliyoweza kuiona yeye tu: “Mimi, Muumba na Mwokozi wako, nakuoa katika imani, uweze kubaki safi hata utakapoadhimisha arusi yako ya milele na mimi mbinguni”.

Kwake Kristo alikuwa bwanaarusi ambaye aishi naye kwa umoja na uaminifu wa dhati, naye alimpenda kweli kuliko yeyote na chochote.

Muungano huo unaangazwa na tukio lingine la pekee ambalo Katerina alimshirikisha muungamishi wake: mabadilishano ya mioyo. Yesu alimtokea “akishika katika mikono yake mitakatifu moyo wa mtu mwekundu sana tena angavu”, akafungua kifua cha Katerina na kumtia moyo huo akisema, “Binti mpenzi kabisa, kama vile majuzi nilikuondolea moyo wako, tazama, nakupa wa kwangu uweze kuendelea kuishi nao milele”.

Karama nyingine ya Katerina ilikuwa kutokwa na machozi, yaliyodhihirisha wema wake uliokuwa tayari kuguswa na kuhurumia kama vile Yesu mbele ya kaburi la Lazaro. Kwa maelezo yake, machozi ya watakatifu yamechanganyikana na damu ya Kristo, ambayo aliizungumzia kwa maneno motomoto na mifano miangavu: “Umkumbuke Kristo msulubiwa, Mungu na mtu pamoja… Umlenge Kristo msulubiwa, fichama katika madonda ya Kristo msulubiwa na zama katika damu ya Kristo msulubiwa”.

Kwa ubunifu wa pekee Katerina alimfananisha Yesu na daraja linalounganisha mbingu na dunia ambalo lina ngazi tatu: miguu, ubavu na kinywa cha Yesu. Kupitia ngazi hizo roho inapiga hatua tatu za kuelekea utakatifu: kubandukana na dhambi, kutekeleza maadili na upendo, muungano mtamu wa upendo na Mungu.

Mwishoni mwa sura hiyo, aliandika: “Kwa huruma umetuosha katika damu hiyo, kwa huruma umetamani kuongea na viumbe. Kichaa kwa upendo! Haikukutosha utwae mwili, bali ulitamani kufa pia! Lo, huruma! Moyo wangu unazama katika kukufikiria: kwa sababu kila ninapogeuka niwaze, naona huruma tu”.

Katerina hakuogopa watu wakubwa bali aliwaelekea uso kwa uso bila unyonge. Pamoja na kwamba aliheshimu daima mamlaka ya viongozi vya Kanisa, hasa ya Papa, aliyemuita “Kristo mtamu aliyepo duniani”, mwaka 1372 hivi alimueleza balozi wa Papa huko Italia, Pietro d'Estraing, haja ya kurekebisha maadili ya wakleri, ya kumrudisha Papa toka Avignone (watangulizi wake na yeye walipokaa tangu mwaka 1309) hadi Roma na ya kuendesha vita vya msalaba dhidi ya wasioamini.

Pamoja na hayo, ilimbidi ateseke sana, kwa sababu wengi hawakumuamini.

Viongozi wa juu wa Kanisa, wakichukizwa na ushujaa wa mwanamke huyo asiye na elimu, walimuita mwaka 1374 huko Firenze mbele ya mkutano mkuu wa Wadominiko. Shirika lao lilitambua usahihi wa imani yake na kumkabidhi kwa uongozi wa kiroho wa Raimondo wa Capua (1330-1399), padri msomi na mnyenyekevu ambaye baadaye alikuwa wa kwanza kuandika maisha yake.

Inasemekana kuwa tarehe 1 Aprili 1375 huko Pisa alijaliwa madonda matakatifu yasiyoonekana hadi kifo chake.

Baada ya majaribio mengi, hatimaye alifaulu katika juhudi kuu ya maisha yake: tarehe 17 Januari 1377 Papa Gregori XI alihamia Roma bila kujali upinzani wowote.

Mwanzoni mwa mwaka 1378 aliagizwa kupatanisha Ukulu mtakatifu na mji wa Firenze.

Lakini tarehe 20 Septemba wa mwaka huohuo, huko Fondi, lilianza Farakano la Magharibi ambalo lilimsikitisha sana likadumu miaka 40 kwa madhara makubwa.

Alifariki Roma, Italia, tarehe 29 Aprili 1380, akiwa na miaka 33 tu, baada ya kushindwa muda mrefu kula na kunywa chochote isipokuwa Ekaristi, kutokana na njozi ya Yesu Kristo aliyemjalia kufyonza damu ubavuni mwake.

Kabla hajafa alisema, “Katika kuhama mwili wangu, kweli nimemaliza na kutoa maisha yangu ndani ya Kanisa na kwa ajili ya Kanisa takatifu”.

Katerina alitangazwa na Papa Pius II kuwa mtakatifu bikira mwaka 1461. Papa Paulo VI alimtangaza mwalimu wa Kanisa tarehe 4 Oktoba 1970.

Kutokana na umuhimu wake katika historia ya Kanisa na ya jamii pia, ni msimamizi (pamoja na wengine) wa Italia (kwa uamuzi wa Papa Pius XII mwaka 1939) na wa Ulaya (kwa uamuzi wa Papa Yohane Paulo II mwaka 1999).

Mfano wake unafundisha kwamba urekebisho wa hali iliyopo unatakiwa kuletwa na upendo, si uasi. Upande wa Kanisa unatakiwa kutokana na juhudi ya kutekeleza ufalme wa Mungu na kuelekea utimilifu wake.

Sikukuu yake inaadhimishwa kila mwaka tarehe 29 Aprili.

# Yohane wa Avila (1500 hivi- 1569)



Yohane wa Avila alikuwa padri mwanajimbo wa Hispania aliyeathiri sana Kanisa Katoliki la nchi hiyo na urekebisho wa Kikatoliki katika karne XVI hasa kwa njia ya mahubiri yake yaliyotegemea Biblia, ya uongozi wa kiroho na ya vyuo alivyovianzisha.

Kwa namna ya pekee mkoa wa Andalusia na watakatifu Teresa wa Yesu, Yohane wa Mungu na Fransisko Borja walifaidika na utume wake.

Yohane wa Avila alizaliwa huko Almodóvar del Campo (Ciudad Real, katika Jimbo Kuu la Toledo, Hispania) tarehe 6 Januari 1499 au 1500 katika familia tajiri na yenye imani ya Kikristo ingawa yenye asili ya Kiyahudi. Baba yake aliitwa Alonso Avila na mama Katalina Gijon.

Akiwa mtoto pekee, alipofikia umri wa miaka 14 alitumwa masomoni kwenye chuo kikuu cha Salamanca ili ajifunze sheria, lakini baada ya miaka miwili akarudi nyumbani kutokana na wongofu wa dhati akatumia miaka mitatu kufanya toba kali, kusali na kutafakari.

Utakatifu wake ulimvutia Mfransisko ambaye alipitia Almodóvar, akamshauri aanze masomo ya falsafa na teolojia kwa ajili ya upadri huko Alcalá de Henares, alipofundishwa na Mdominiko maarufu, Domingo de Soto.

Chuo hicho kilikuwa wazi kwa mitazamo mbalimbali ya wakati ule na kwa tapo la Renaissance lililojali sana binadamu na mambo yake yote.

Wakati wa masomo hayo alifiwa wazazi; hivyo baaada ya upadrisho wake (1526) aliuza mali ya familia na kuwagawia maskini mapato yake.

Yeye aliona vifo hivyo kuwa ishara ya Mungu kumwita awe mmisionari akajiandaa kwenda Meksico.

Mwaka 1527, akiwa Sevilia ili kupata nafasi nzuri ya kusafiri baharini, alijitosa kuhubiri mjini na kandokando yake.

Namna yake bora ya kuishi, kuadhimisha Misa na kuhubiri ilimshangaza padri Hernando de Contreras, mwalimu wa Alcalà maarufu upande wa katekesi, ambaye alimuarifu askofu mkuu wa Sevilia, na pia hakimu mkuu Alonso Manrique de Lara.

Askofu alitambua kwamba huyo padri kijana anafaa kuchochea imani mkoani Andalusia, na baada ya kumshauri sana alimfanya akubali kuacha mpango wa kwenda Amerika.

Basi, akabaki na Hernando, akishiriki naye maisha ya ufukara na sala na kuendelea na masomo yake katika Chuo cha Mt. Thoma. Labda ndipo alipopewa jina "Mwalimu", lililoendelea kutumika kwa ajili yake hata kisha kufa.

Alianza kuhubiri tarehe 22 Julai 1529, akapata mara umaarufu.

Katika miaka tisa aliyofanya utume huko Andalusia, mahubiri yake yote yalisikilizwa na umati wa watu waliobanana.

Hata hivyo, nguvu ya maneno yake kwa ajili ya urekebisho na dhidi ya mwenendo wa matabaka ya juu katika jamii ilisababisha mwaka 1531 afikishwe mbele ya Hakimu mkuu wa Sevilia.

Shtaka lilikuwa kwamba alizidisha hatari ya kiroho inayotokana na utajiri na hivyo kuwafungia matajiri milango ya mbinguni. Lakini aliweza kujitetea vizuri na kuachiliwa mwaka 1533, baada ya kufungwa gerezani zaidi ya mwaka mmoja, akateuliwa kuhubiri tena kwa watu wa kawaida na kwa wale wenye mamlaka.

Akiwa gerezani alianza kuandika kitabu chake bora; pia alijaliwa kuzama katika fumbo la upendo wa Mungu uliofunuliwa kumpitia Yesu Kristo na katika fadhili ambazo binadamu wamepata kutoka kwa Mkombozi huyo.

Tangu hapo hizo mbili zikawa nguzo za maisha yake ya Kiroho na mada kuu za mahubiri yake, pamoja na kutangaza nafasi ya kwanza ya neema, inayohimiza matendo mema, na kuhamasisha tumaini kwa Mungu na itikio kwa upendo wake unaoita wote wawe watakatifu.

Kama wanasala wengine wa Hispania wakati huo, alishukiwa mara kadhaa kuhusika na Alumbrados, waliotazamwa kama wazushi.

Pamoja na kwamba Yohane aliwahi kuelekeza wote kwenye utakatifu, alichangia sana ustawi wa teolojia ya upadri, akisababisha kati ya wanajimbo juhudi kubwa za Kiroho na kuathiri waandishi waliofuata. Kiini cha mafundisho yake kuhusu jambo hilo ni kwamba "wakati wa Misa sisi (mapadri) tunajiweka juu ya altare katika nafsi ya Kristo ili kutekeleza kazi ya Mkombozi mwenyewe"; hiyo inadai kutimiza kwa unyenyekevu upendo wa kibaba na wa kimama wa Mungu, kwa hiyo kuwa na mtindo wa maisha wa pekee.

Yohane wa Avila anakumbukwa hasa kwa kurekebisha Kanisa kwa kuboresha maisha ya mapadri nchini Hispania, ingawa hakuanzisha shirika lolote kwa ajili yao. Wakleri watakatifu ni haja ya msingi kwa urekebisho wa Kanisa, na hilo linadai uchambuzi makini na malezi ya kufaa kwa walioelekea upadri. Hivyo alihimiza uanzishaji wa seminari na wa vyuo maalumu kwa elimu ya Biblia. Mapendekezo hayo yalikuja kuathiri Kanisa lote.

Ni kwamba, kwa kutia maanani sana malezi, alianzisha mwenyewe vyuo kadhaa ambako wanafunzi wake walijitosa kufundisha vijana. Baada ya Mtaguso wa Trento, hivyo vikawa seminari kadiri ya maagizo ya mtaguso huo.

Umuhimu wa pekee kati ya mafanikio yake unacho Chuo kikuu cha Baeza kilichoanzishwa naye mwaka 1538 kwa hati ya Papa Paulo III na ambacho akawa gombera wake wa kwanza hata bila kufundisha mwenyewe, isipokuwa Biblia kwa walei, watawa na wakleri, kwa sababu alitamani sana ijulikane na wote.

Chuo hicho katika karne zilizofuata kikawa kielelezo kwa seminari na kwa shule za Wajesuiti, ambao wanamheshimu kwa namna ya pekee kwa kuwasaidia kustawi Hispania, hasa kwa kuelekeza kwao wanafunzi wake bora 30 hivi. Mwenyewe alitamani kujiunga nao, asiweze ingawa alikaribishwa na Ignasi wa Loyola aliyemheshimu sana.

Kati ya watakatifu rafiki zake kuna pia padri Mfransisko Petro wa Alcantara na maaskofu Thoma wa Villanova na Yohane wa Ribera.

Baada ya utume wake wa miaka tisa mkoani Andalusia, alirudi Sevilia, ambako aliondoka tu kwa kazi kubwa zaidi huko Cordoba, alipojiunga na jimbo moja kwa moja, Granada (1536), alipohitimu masomo ya chuo kikuu, Baeza, Montilla na Zafra.

Miaka kumi na nane ya mwisho aliugua mfululizo, kutokana na ugumu wa maisha na wa kazi alizofanya kwa miaka arubaini. Mwaka 1554 alihamia nyumba ndogo ya Montilla, alipoendeleza utume wake kwa kuandika barua nyingi na vitabu kadhaa.

Askofu mkuu wa Granada alitaka aende naye kama mtaalamu wa teolojia kwenye vikao vya mwisho vya Mtaguso wa Trento, lakini afya haikumruhusu kusafiri. Hata hivyo "Memoriales" ("Kumbukumbu") alizoziandika kwa ajili hiyo, ziliathiri sana mtaguso huo.

Alifariki tarehe 10 Mei 1569 asubuhi huko Montilla, akishika msalaba na kuzungukwa na wafuasi na marafiki.

Kati ya mengineyo, Yohane alipendekeza ianzishwe mahakama ya kimataifa ya usuluhishi ili kuepa vita, pia alibuni na kusajili vifaa kadhaa vya uhandisi.

Akiishi kifukara sana, alijitosa hasa kuhimiza maisha ya Kikristo kati ya wale waliomfuata kila mahali ili kumsikiliza.

Wale wote walioongozwa naye kiroho walitambua mapema kipaji chake cha pekee cha kupenya fumbo la Kristo, kwamba baraka zote zinatujia kwa njia yake; kwamba tunachuma matunda ya ukombozi kadiri tunavyoungana naye; kwamba muungano huo unaanza na imani na ubatizo na kukamilishwa na ekaristi; na kwamba kujitoa kabisa kwake kunazaa ndani mwetu tumaini na furaha.

"Fungua moyo wako mdogo upokee ile pumzi ya upendo ambao kwao Baba anatupatia Mwanae, na kwa njia yake anajitoa kwetu pamoja na Roho Mtakatifu na vingine vyote".

Maandishi yake yalikusanywa huko Madrid miaka 1618, 1757, 1792 na 1805; yote yanang'aa kwa kufafanua mada kwa dhati, kwa mbinu rahisi na kwa mifano mingi; kati yake, maarufu zaidi ni: *"Audi Filia, et vide"* ("Sikiliza, binti, na uone") kuhusu ukamilifu wa Kikristo, na *"Barua za Kiroho"* kwa wafuasi wake zilizotafsiriwa mapema katika lugha mbalimbali.

Pia kuna katekisimu kwa watoto na watu wazima inayoitwa "Mafundisho ya Kikristo", "Insha juu ya Upendo wa Mungu", inayoshirikisha dhati ya fumbo la Kristo, "Insha juu ya Upadri", "Maelekezo kuhusu Urekebisho", "Hotuba", "Maongezi" na ufafanuzi wa vitabu mbalimbali vya Biblia, kama vile barua kwa Wagalatia na ile ya kwanza ya Yohane.

Katika kusoma Biblia alitumia na kulinganisha tafsiri mbalimbali, alichunguza maneno yenyewe na maana yake ya Kiroho, pamoja na kutegemea sala na kuwa na uzoefu na maelezo ya mababu wa Kanisa.

Pengine hakuandika zaidi kwa kuogopa hukumu kali za Mahakama ya Imani ya wakati ule.

Papa Leo XIII alimtangaza mwenye heri tarehe 6 Aprili 1894, halafu Papa Paulo VI akamtangaza mtakatifu tarehe 31 Mei 1970.

Hatimaye Papa Benedikto XVI akamtangaza mwalimu wa Kanisa tarehe 7 Oktoba 2012.

Sikukuu yake inaadhimishwa kila mwaka tarehe 10 Mei.

## Teresa wa Yesu (1515 - 1582)



Teresa wa Yesu ni jina la kitawa la Teresa Sánchez de Cepeda Ávila y Ahumada, maarufu pia kama Teresa wa Avila.

Mwanamke halisi, utu wake ulikomaa: alikuwa na tabia ya kupendeza, uchangamfu na busara sana, uhodari na msimamo, uwezo wa kukabili hali iliyopo kwa kupanga vizuri na kufanikisha mambo.

Ni kati ya watu muhimu zaidi katika historia ya Kanisa ya karne XVI, katika historia yote ya utawa na katika teolojia ya Kiroho kutokana na urekebisho aliouanzisha katika shirika la Wakarmeli (wanawake na wanaume vilevile) na kutokana na maandishi yake juu ya maisha ya kiroho yanayomfanya mwalimu wa sala aliye bora kuliko wote.

Alizaliwa Avila, Hispania, tarehe 28 Machi 1515, katika familia kubwa, yenye watoto 9 wa kiume na 4 wa kike.

Akisaidiwa na mfano wa wazazi wake "waliokuwa waadilifu na wacha Mungu" (alivyosema mwenyewe), tangu utotoni alionekana kuelekea sana maisha ya sala hasa upwekeni.

Kabla ya kufikia umri wa miaka 9 alisoma habari za wafiadini kadhaa ambazo zilimfanya atamani kufia dini hivi kwamba alitoroka nyumbani ili akashiriki kifo chao na kwenda mbinguni. Aliwaambia wazazi wake, "Nataka kumuona Mungu".

Katika masomo yake ya utotoni aliona njia ya ukweli aliyoijumlisha katika mawazo mawili ya msingi: "Vitu vyote vya ulimwengu huu watapita", kumbe Mungu tu ni "wa milele, milele, milele". Mawazo hayo akaja kuyatumia baadaye katika shairi lake maarufu zaidi: "Usivurugwe na lolote, Usitishwe na lolote, Yote yanapita: Mungu habadiliki kamwe. Subira inapata yote. Aliye na Mungu hakosi kitu; Mungu tu anatosha". (Shairi, 9)Alipofikia umri wa miaka 12, alifiwa mama yake, akamuomba Bikira Maria ashike nafasi hiyo.

Akiwa na miaka 13 akatumwa kusomea shule ya bweni ya masista Waaugustino hadi alipoweza kukabili kazi ya kutunza familia ya baba yake.

Vitabu vya kidunia vilikuwa vinamuelekeza kutawanyika, lakini vile vya Kiroho, hasa vya Wafransisko, vilimuingiza katika maisha ya umakinifu na sala.

Mpenzi wa kusoma vitabu vya mababu wa Kanisa, hasa Augustino na Gregori Mkuu, alipata wito wake wa kitawa kwa kusoma vile vya Jeromu.

Mwaka 1536, akiwa amefikia hakika ya kuitwa utawani, aliingia monasterini, ingawa kwanza baba yake hakukubali, akajichagulia jina la "Teresa wa Yesu".

Alipojiunga na Wakarmeli wa mji wake, alikuta juhudi za masista wamonaki zilikuwa za kiasi.

Mwenyewe, kisha kuweka nadhiri zake, aliamua kulenga ukamilifu, lakini kwa kukosa busara katika juhudi zake, miaka 3 baadaye aliugua sana, ikambidi baba ampeleke kwa matibabu kwenye mji wa jirani, na hatimaye amrudishe nyumbani ili kusubiri kifo. Monasterini waliandaa kaburi, ila baba alikataa asizikwe.

Kumbe, baada ya siku nne za kupotewa kabisa na ufahamu, alianza kupata nafuu hata akaweza kurudi utawani, ingawa kwa muda fulani alikuwa amepooza tu. Mwenyewe alifananisha hali hiyo ya afya yake na ile ya roho yake kutokana na yeye kukaidi neema nyingi za Mungu.

Hatimaye, alipopona kabisa, alisema ni kwa maombezi ya Mt. Yosefu, ambaye tangu hapo alimheshimu sana.

Mwaka 1543 alipotewa na familia yake: baba alikufa na ndugu zake wote walihamia Amerika, mmoja baada ya mwingine.

Baada ya kipindi cha ulegevu, alipopoteza muda mwingi sebuleni, bila kujali maonyo ya muungamishi wake, na alipojiona anafanana na Augustino wa Hippo katika mapambano dhidi ya udhaifu wake, katika Kwaresima ya mwaka 1554 aliguswa sana na sanamu iliyomuonyesha Yesu katika uhalisia wa mateso yake. "Ghafla hisi ya uwepo wa Mungu ilinijia, nisiweze kabisa kutia shakani kwamba alikuwa ndani mwangu wala kwamba mimi nilikuwa nimevutwa kabisa ndani yake".

Tangu hapo alishika maisha magumu kabisa, akijitahidi kujikusanya peke yake mbele ya Mungu.

Baadaye aliishi karibu miaka mitatu katika nyumba ya mwanamke mjane mwenye ibada sana aliyeongozwa na Wajesuiti.

Mwaka 1560, pamoja na wenzake wachache, alitambua haja ya kutengeneza upya maisha ya Karmeli, na alijisikia kuitwa na Mungu kuongoza kundi lao, akaanza kazi yake kubwa ya kurekebisha shirika kwa msaada wa Yohane wa Msalaba upande wa wanaume.

Mwaka 1562, baada ya kushinda shida mbalimbali, kwa msaada wa askofu wa jimbo, Alvaro de Mendoza, alianzisha monasteri ya kwanza ya urekebisho mjini Avila chini ya usimamizi wa Mt. Yosefu. Muda si muda alipata pia kibali cha mkuu wa shirika lote, Yohane Mbatizaji Rossi.

Pamoja na Yohane wa Msalaba mwaka 1568 alianzisha huko Duruelo konventi ya kwanza ya wanaume.

Mwaka 1580 alipata kutoka Roma kibali cha kuunda kanda huru kwa monasteri za urekebisho wake: ndio mwanzo wa shirika la Wakarmeli Peku.

Ingawa alipaswa kusafiri na kushughulika sana ili kuanzisha monasteri nyingine 16 huko na huko, pamoja na kukabiliana na matatizo mengi makubwa, Teresa alifikia vilele vya maisha ya sala na kujaliwa neema nyingi za pekee.

Hiyo inashuhudiwa na maandishi yake, yaliyokusudiwa kufundisha hasa masista wenzake, na ambayo ni kati ya vitabu bora vya Kanisa Katoliki:

*Maisha Yake Mwenyewe*, yaliyoandikwa mwaka 1565 chini ya padri Pedro Ibáñez, muungamishi wake, ili amuombe Yohane wa Avila aifanyie utambuzi safari yake ya Kiroho; alikiita "kitabu cha rehema za Bwana" kwa kuwa kililenga kuonyesha uwepo na utendaji wa Mungu mwenye huruma katika maisha yake; ndiyo sababu mara nyingi kinaripoti maongezi yake na Bwana katika sala.

*Safari ya Ukamilifu*, kilichoandikwa mwaka 1566 chini ya muungamishi wake; Teresa alikiita "Maonyo na mashauri ambayo Teresa wa Yesu anawapa dada zake" kwa sababu alikiandika kwa ajili ya wanovisi 12 wa monasteri yake ili kuwahamasisha wawe na maisha ya maadili na ya sala ya dhati kwa ajili ya Kanisa; kati ya sehemu bora za kitabu hicho upo ufafanuzi wa Baba Yetu kama kielelezo cha sala.

*Jumba la Ndani, Makao*, kitabu chake bora, kilichoandikwa mwaka 1577, ambamo anamfananisha mtu wa sala na jumba lenye vyumba 7 vinavyofikiwa kimoja baada ya kingine kadiri ya maendeleo ya kiroho; ni mtazamo mpya juu ya safari yake mwenyewe lakini pia kinaeleza taratibu za ustawi wa maisha ya Kikristo kuelekea utakatifu chini ya Roho Mtakatifu; vilevile anafananisha badiliko la mtu kutoka maisha ya kawaida hadi yale ya Kimungu na lile la mdudu anayegeuka kipepeo; hatimaye, katika kufafanua hali za juu zaidi, anatumia mfano wa Bwanaarusi na Bibiarusi unaopatikana kwanza katika Biblia.

*Kitabu cha Monasteri Zilizoanzishwa,* alichokiandika katika miaka 1573-1582, kinasimulia maisha ya mwanzo ya urekebisho wake, kikisisitiza nafasi ya Mungu.

*Ripoti*, nyongeza ya kitabu cha maisha yake kwa mtindo wa barua juu ya mang'amuzi yake ya ndani na ya nje.

*Mawazo ya Upendo*

*Mishangao*

*Barua* (342 nzima na sehemu 87 za nyingine).

Humo inaonekana wazi kwamba juhudi za Kikristo ni hasa kupokea na kuitikia kazi ambayo Roho Mtakatifu anaifanya ndani ya mtu kuanzia ubatizo ili kumlinganisha na Yesu.

Mafundisho yake hayakutokana na vitabu alivyosoma, bali na mang'amuzi yake binafsi pamoja na uchunguzi wa yale ya wengine. Ndiyo maana si ya nadharia tu, bali hasa yanafafanua kinachotokea, yakiingia mpaka ndani ya nafsi.

Maisha yake yalimalizika usiku wa kuamkia tarehe 15 Oktoba 1582 katika shughuli za kuanzisha monasteri, kwa kuwa alifariki Alba de Tormes akiwa njiani kurudi Avila baada ya kuanzisha Karmeli ya Burgos. Maneno yake ya mwisho yalikuwa: "Hatimaye ninakufa kama binti wa Kanisa… Saa niliyoitamani imefika, Bwana wangu na Bwanaarusi wangu. Ni wakati wa kukutana na wewe".

Alitangazwa na Papa Paulo V kuwa mwenye heri tarehe 24 Aprili 1614, na Papa Gregori XV kuwa mtakatifu bikira tarehe 12 Machi 1622, na hatimaye na Papa Paulo VI kuwa mwalimu wa Kanisa tarehe 4 Oktoba 1970.


Sikukuu yake inaadhimishwa kila mwaka tarehe 15 Oktoba.

Kama msingi wa maisha yote Teresa alipendekeza maadili ya Kiinjili (kutoambatana na kitu, kupendana, kunyenyekea kwa kupenda ukweli, kuwa na msimamo, kutumaini) bila kusahau yale ya kiutu (upendevu, usemakweli, utaratibu, adabu, uchangamfu, ujuzi).

Pia alipendekeza usikivu kwa Neno la Mungu na ulinganifu na watu wa Biblia: mwenyewe alijisikia kufanana na Bibiarusi wa Wimbo Ulio Bora, na Mtume Paulo na Kristo katika Mateso na katika Ekaristi.

Alisisitiza hasa umuhimu wa sala ambayo kwake "ni kuhusiana kirafiki na Mungu kwa kuongea mara nyingi kwa siri na yeye ambaye tunajua anatupenda". Hatua kwa hatua uhusiano huo unastawi na kutawala maisha yote.

## Yohane wa Msalaba (1542 - 1591)



Yohane wa Msalaba ni jina la kitawa la Juan de Yepes Álvarez, padri wa Kanisa Katoliki na mwanzilishi (pamoja na Teresa wa Yesu) wa urekebisho wa shirika la Wakarmeli maarufu kama Wakarmeli Peku.

Yohane alizaliwa Fontiveros, kijiji cha mkoa wa Castilia kilicho karibu na Avila (Hispania), tarehe 24 Juni 1542.

Baba yake, Gonzalo de Yepes, wa ukoo maarufu wa Toledo, alifukuzwa na familia yake na kunyimwa urithi kwa sababu ya kumuoa mfumaji maskini, Catalina Álvarez. Hivyo hali yao ilikuwa ngumu sana kiuchumi.

Tangu utotoni Yohane alielekea huruma kwa maskini na hasa sala.

Kati ya 1551 na 1559 alipata elimu na ufundi huko Medina del Campo (kituo cha biashara na masomo karibu na Valladolid), ambapo familia yake ilikuwa imehamia kufuatana na kifo cha baba yake.

Baadaye akawa seremala, mshonaji, mchoraji, mchongaji, nesi msaidizi na mtumishi wa altare, kufuatana na vipawa vyake na maendeleo yake katika masomo.

Akiwa na miaka 18 aliingia shule mpya ya bweni iliyoanzishwa na Wajesuiti huko Medina del Campo akasoma lugha na mengineyo kwa miaka mitatu. Alipomaliza alikuwa na hakika kuhusu wito wake wa kitawa.

Mwaka 1563 alijiunga na shirika la Wakarmeli, wakati maisha ya jumuia yalipokuwa yamelegea sana, na wakati wa joto wa mwaka huo alianza unovisi hukohuko Medina del Campo akichukua jina la Yohane wa Mt. Matia.

Kati ya 1564 na 7 akasoma lugha na falsafa katika chuo kikuu maarufu cha Salamanca.

Mwaka 1567 alipata upadrisho akarudi Medina del Campo kuadhimisha Misa ya shukrani kati ya wanafamilia.

Huko akakutana na Teresa wa Yesu, ambaye alimfanya amuunge mkono kabisa katika kurekebisha shirika hilo lirudi kwenye juhudi za awali "kwa utukufu mkubwa zaidi wa Mungu". Upande wake Teresa alianza kumheshimu sana akamuita "baba wa roho" yake, ingawa alimtania pia kutokana na silika yake ngumu na makini.

Kwa miezi kadhaa walishirikishana mawazo na malengo kwa ajili ya kuanza urekebisho mapema iwezekanavyo.

Tarehe 9 Agosti 1568, alikwenda Valladolid ilipoanzishwa monasteri ya kwanza ya Masista Wakarmeli Peku akabaki huko hadi Oktoba ili kujifunza maisha ya urekebisho, halafu akaenda Duruelo (Segovia), akageuza nyumba ya wakulima kuwa konventi ya kwanza ya Wakarmeli Peku wanaume (28 Desemba). Mwanzoni walikuwa wanne. Waliporudia nadhiri zao kadiri ya kanuni asili ya shirika, kila mmoja alijichagulia jina jipya, naye akajiita "Yohane wa Msalaba".

Mwishoni mwa mwaka 1572, kwa ombi la Teresa, akawa muungamishi na makamu wa monasteri ya Umwilisho mjini Avila iliyongozwa na Teresa mwenyewe.

Ilifuata miaka ya urafiki wa kiroho na ushirikiano mkubwa kwa faida ya wote wawili. Ndipo vitabu bora vya Teresa na vile vya kwanza vya Yohane vilipoandikwa.

Kati ya mateso ya kimwili na ya kiroho yaliyompata kwa kupigania urekebisho, mbali ya kufukuzwa konventini, mojawapo ni lile la kufungwa miezi minane kwa tuhuma ya uongo katika gereza la shirika la Toledo (kuanzia tarehe 2 Desemba 1577 hadi alipotoroka usiku wa kuamkia tarehe 17 Agosti 1578). Humo alinyanyaswa kwa namna mbalimbali.

Hata hivyo humohumo aliangaziwa na Mungu kutunga baadhi ya mashairi yake bora, yaliyompatia nafasi kati wa washairi mashuhuri wa lugha ya Kihispania.

Kisha kujisalimisha katika nyumba ya Wakarmeli Peku ya Toledo, Teresa na wenzake walishangilia sana uhuru wake. Baada ya muda mfupi wa pumziko kwa ajili ya kupata tena nguvu, alipangiwa kwenda katika mkoa wa Andalusia, alipoishi miaka 10 katika konventi mbalimbali, hasa Granada.

Alizidi kupewa vyeo muhimu shirikani hata kuwa makamu wa mkuu wa kanda, pia alikamilisha maandishi yake ya kiroho.

Halafu akarudi katika mkoa wake asili kama mmoja wa halmashauri kuu ya shirika la Teresa ambalo lilikuwa limeshapata uhuru kamili kisheria. Aliishi katika Karmeli ya Segovia kama mkuu wa jumuia.

Miaka ya mwisho ya maisha yake alijikuta ameachwa na wafuasi wake walio wengi.

Mateso hayo yote yalimfundisha kuvumbua fumbo la msalaba na kusonga mbele katika njia ya sala ya juu kabisa, hata akaweza kuielekeza kwa kufafanua hatua zake.

Mwaka 1591 aliondolewa majukumu yote na kupangiwa aende katika kanda mpya ya Meksiko barani Amerika. Akiwa anajiandaa kwa safari hiyo ndefu pamoja na wenzake 10, tarehe 28 Septemba 1591 akiwa mgonjwa alisafiri kwenda kujifungia katika konventi ya Úbeda (karibu na Jaén), alipozidi kuugua kwa mateso makali na uvumilivu mkubwa hadi alipofariki usiku kati ya tarehe 13 na 14 Desemba 1591.

Wakati wenzake walipokuwa wanaimba Kipindi cha Masomo, aliaga, "Leo naenda kuimba Masifu mbinguni".

Masalia yake yalihamishiwa Segovia.

Pamoja na kuwa mshairi, Yohane alikuwa hasa mwanateolojia, aliyetunga vitabu mbalimbali kuhusu maisha ya Kiroho, yaani sala na safari ya kumuelekea Mungu kwa njia ya mkato (kupitia hatua ya utakaso, hatua ya mwanga na hatua ya muungano).

Kufuatana na mapokeo ya Ukristo, alifundisha namna ya kubandukana na wote na vyote ili kuungana na Mungu tu aliye kwa pamoja "mwanga wenye giza na giza angavu", kwa kuwa mwanga wake ni mkali mno kwa macho yetu mabovu.

Mojawapo ya semi zake ilikuwa kwamba: "Mungu anamnyenyekesha sana mtu ili kumuinua sana".

Maandishi yake ni kama ifuatavyo:

- Wimbo wa Kiroho
- Usiku Wenye Giza wa Roho
- Kupanda Mlima Karmeli
- Mwali Hai wa Upendo
- Mawazo Juu ya Upendo na Amani
- Barua

Katika "Wimbo wa Kiroho", Yohane anaeleza maendeleo ya utakaso wa roho kama njia ya kuzidi kumpata Mungu kwa furaha, hadi mtu anapotambua kwamba anampenda kwa upendo uleule ambao anapendwa naye.

"Mwali Hai wa Upendo" kinaendeleza mada hiyo kwa kufafanua zaidi hali ya muungano na Mungu unaomgeuza mtu ndani yake. Mfano unaotumika tena na tena ni ule wa moto: kama vile huo unavyozidi kuwaka kwa nguvu na kushika ukuni hata kuugeuza mwali, Roho Mtakatifu naye, kisha kutakasa roho katika usiku wenye giza, anaiangaza na kuiwasha kama mwali wa moto. Maisha ya roho ni adhimisho la mfululizo la Roho Mtakatifu ambalo mtu anaanza kuonja utukufu wa kuungana na Mungu milele.

"Kupanda Mlima Karmeli" kinaelekeza roho katika utakaso wake wa hatua kwa hatua, unaohitajika ili kupanda hadi vilele vya ukamilifu wa Kikristo, unaomaanishwa na mlima huo. Utakaso huo unapendekezwa kama safari ambapo mtu anashirikiana na Mungu ili kubandukana na lolote lililo kinyume na matakwa yake matakatifu.

Utakaso huo, unaotakiwa kuwa kamili uweze kufikia muungano wa upendo na Mungu, unaanza na hisi, halafu unaendelea na maadili makuu ya Kimungu (imani, tumaini na upendo) ili kutakasa pia akili, kumbukumbu na utashi.

"Usiku Wenye Giza wa Roho" kinafafanua kazi ya Mungu mwenyewe katika kuitakasa kikamilifu roho ya mtu na kuiandaa iweze kuungana naye kwa upendo. Hiyo inahitajika kwa sababu juhudi za binadamu haziwezi kutosha kufikia mizizi mirefu ya maelekeo na mazoea mabaya aliyonayo. Mtu anaweza kuyadhibiti, lakini si kuyang'oa kabisa. Hiyo ni kazi ya Mungu tu: mtu anapaswa kukubali afanyiwe, lakini ni Roho Mtakatifu ambaye kama mwali wa moto anateketeza uchafu wowote. Katika hali hiyo mtu anajaribiwa kwa kila namna, kama kwamba angejikuta katika usiku wenye giza nene.

Mihtasari hiyo ya vitabu muhimu zaidi vya Yohane wa Msalaba inatusaidia kutambua mafundisho yake makuu kuhusu maisha ya Kiroho, yaliyoelekeza kwa hakika njia ya utakatifu ambao Mungu anawaitia wote,

Kwake viumbe vyote ni vyema, na kwa kuvipitia tunaweza kumfahamu Muumba aliyeacha athari yake ndani ya hivyo vyote. Lakini ni imani tu inayotuwezesha kumjua Mungu jinsi alivyo kwa ndani, yaani katika umoja wa Nafsi tatu. Yale yote aliyotaka kuwashirikisha binadamu aliyatoa katika Yesu Kristo, Neno wake aliyefanyika mwili: ndiye njia pekee ya kumfikia Baba.

Viumbe vyote si kitu kabisa vikifananishwa na Mungu, kwa hiyo ili tufikie upendo kamili wa Mungu, ni lazima mapendo mengine yote yalinganishwe nao ndani ya Kristo. Ndiyo sababu Yohane anasisitiza haja ya utakaso na uvuaji kamili ili kugeuzwa ndani ya Mungu, lengo la ukamilifu.

Safari ndefu na ngumu ya utakaso inadai juhudi za mtu, lakini mtendaji mkuu ni Mungu: mtu anapaswa hasa kujiandaa afanyiwe kazi bila kuizuia. Hasa atekeleze maadili ya Kimungu ambayo yanakua pamoja na maendeleo ya utakaso na muungano na Mungu, hadi mtu ageuzwe ndani ya Mungu.

Akifikia lengo hilo, mtu anazama ndani ya Utatu Mtakatifu na kumpenda Mungu kwa upendo uleule anaopendwa naye, yaani anampenda kwa Roho Mtakatifu. Anajisikia amezama katika upendo wa Mungu na kuufurahia bila kipimo. Anafahamu yote kumpitia Mungu, asihitaji tena kuvipitia viumbe ili kumfikia.

Maandishi yake yalitolewa kwa mara ya kwanza mwaka 1618, akatangazwa kuwa mwenye herina Papa Klementi X tarehe 25 Januari 1675, halafu mtakatifu na Papa Benedikto XIII tarehe 27 Desemba 1726 na hatimaye mwalimu wa Kanisa na Papa Pius XI tarehe 24 Agosti 1926.

Sikukuu yake inaadhimishwa kila mwaka tarehe 14 Desemba.

Tangu tusome mara ya kwanza maandishi ya Teresa wa Yesu na Yohane wa Msalaba, ni rahisi tutambue tofauti ambazo zimesisitizwa mara nyingi. Zinatokana na tofauti za mitazamo yao. Teresa alitegemea mang'amuzi yake binafsi, akidokeza neema za pekee alizojaliwa (njozi n.k.) asiwe makini kuzitofautisha na mambo yaliyo ya lazima katika "makao saba" ya jumba la Kiroho. Hivyo alitia maanani kuliko wengine matukio ya kihisi, ya nje na ya ziada yanayoweza yakaendana na sala ya kumiminiwa; vilevile alisisitiza kuzingatia ubinadamu wa Yesu.

Yohane pia alisema kwa mang'amuzi yake binafsi na ya watu aliowaongoza, lakini hakuyataja, akijitahidi kuyachimba kiteolojia, jambo ambalo ni muhimu ili kutofautisha yaliyo ya kawaida na yaliyo ya ziada. Alieleza sababu za hali mbalimbali za sala kwa mafundisho juu ya maadili ya Kimungu na ya vipaji vya Roho Mtakatifu vinavyoendana nayo.

Kwa mtazamo huo alizingatia yaliyo ya lazima katika safari ya kuelekea utakatifu, hasa matakaso ya Kimungu yanayohitajika kwa usafi kamili wa upendo. Hivyo hakuelekea kujali neema za pekee zinazoendana pengine na sala ya kumiminiwa, wala hakusisitiza kuzingatia ubinadamu wa Yesu, akilenga moja kwa moja shabaha kuu ya sala, yaani Mungu aliyemo mwetu, tunayemfikia katika giza la imani kwa njia ya ujuzi ambao anatumiminia na unafanana na mang'amuzi.

Kwa kufanya hivyo amekamilisha maandishi ya Teresa na kutusaidia tuyaelewe.

Hata hivyo, chini ya tofauti hizo kuna msingi mmoja, kwa kuwa Teresa alijua vya kutosha mang'amuzi ya wafuasi wake aweze kuelewa na kueleza nini inatokea kwa kawaida kwa watu wanaopitia hayo makao saba. Tukitumia maelekezo aliyoyatoa huko na huko tunaweza kubainisha zaidi yaliyo ya lazima na yaliyo ya ziada.

Kimsingi watakatifu hao walielewa vilevile sala ya kumiminiwa, muungano na Mungu unaotokana nayo, na matakaso ya Kimungu yanayohitajika ili kuufikia ule kamili.

Ikifaa kuonyesha tofauti zao, inafaa zaidi kuonyesha wanavyolingana na kutambua teolojia inavyoweza kusaidia katika masuala hayo magumu.

# Petro Kanisi (1521 - 1597)



Petro Kanisi, kwa Kiholanzi Pieter Kanijs, au Kanisius, au Kanîs, alikuwa mtawa, mwanateolojia na padri wa Kanisa Katoliki.

Petro alizaliwa na meya wa Nijmegen, katika mji huo wa Dola takatifu la Roma, leo nchini Uholanzi, tarehe 8 Mei 1521.

Akiwa mwanafunzi wa chuo kikuu cha Cologne, Ujerumani, alikuwa akitembelea mara kwa mara Wakartusi wa Mt. Barbara, wamonaki waliochangia sana maisha ya Kiroho ya Wakatoliki, akishirikishana hasa na Yohane Lansperger na Nikola wa Esche; vilevile alishirikiana na watu walioishi Kikristo kadiri ya "Devotio moderna" (yaani Juhudi za kisasa).

Tarehe 8 Mei 1543, siku ya kutimiza miaka 22, akiwa huko Mainz, Ujerumani, baada ya kushiriki mazoezi ya kiroho yaliyoongozwa na Petro Favre, alikuwa Mholanzi wa kwanza kujiunga na Shirika la Yesu na mwanashirika wa nane.

Alipewa upadrisho huko Cologne mwaka 1545.

Mapema, mnamo Juni 1546 aliitwa na askofu wa Augsburg, kardinali Otto Truchsess von Waldburg, ashiriki Mtaguso wa Trento kama mtaalamu wa teolojia.

Mwaka 1548, mwanzilishi wa shirika, Ignasi wa Loyola, alimuita Roma, Italia, akamilishe malezi yake ya kiroho, halafu akamtuma kwenye shule ya bweni ya Messina, Italia, atoe huduma duni za nyumbani.

Tarehe 4 Oktoba 1549 alipata udaktari wa teolojia huko Bologna, Italia, alipofundisha pia kwa muda mfupi.

Kabla ya hapo, tarehe 2 Septemba alimtembelea Papa Paulo III ili kupata baraka kwa ajili ya utume mpya aliopangiwa Ujerumani, akahiji katika Basilika la Mt. Petro huko Vatikano ili mitume Petro na Paulo wamuimarishie moja kwa moja baraka hiyo.

"Huko nilihisi kujaliwa faraja kubwa na uwepo wa neema kupitia waombezi hao. Walithibitisha utume wangu Ujerumani na walionekana kunishirikisha msaada wa wema wao kama mtume wa Ujerumani. Ee Bwana, wewe unajua kwa njia nyingi kiasi gani, na mara ngapi siku hiyohiyo ulinikabidhi Ujerumani, ambao baadaye niliendelea kuushughulikia nikiwa tayari kuishi na kufa kwa ajili yake".

Ni kwamba kazi aliyopangiwa, yaani kuhuisha imani Katoliki katika nchi kubwa na ndogo zilizounda Dola la Kijerumani, ilionekana haiwezekani kwa sababu ya Urekebisho wa Kiprotestanti uliozidi kuenea. Iliwezekana tu kwa njia ya sala, kutokana na urafiki wa dhati na Yesu Kristo katika mwili wake, yaani Kanisa, uliolishwa na fumbo la mwili wake, yaani Ekaristi. Ndiyo sifa ya maisha ya Kiroho ya Petro.

Kwa mfano katika shajara yake, tarehe 4 Septemba 1549 aliandika kwamba alialikwa na Yesu kunywea Moyo wake wazi halafu akapewa nguo yenye vipande vitatu vilivyoitwa amani, upendo na udumifu: ndizo silaha alizozitumia katika utume wake huo.

Kwanza alifanya kazi kwa miaka kadhaa katika Ufalme mdogo wa Bavaria.

Baada ya kuteuliwa mkuu wa kwanza wa kanda ya Ujerumani ya Wajesuiti, wadhifa alioushika hadi mwaka 1569, alitoa mchango mkubwa katika urekebisho wa Kikatoliki hasa kwa kuanzisha vyuo vingi vya shirika, hata mwaka 1897 Papa Leo XIII alimtaja "mtume wa pili wa Ujerumani" baada ya Mt. Bonifas. Uwepo wa Wakatoliki wengi Ujerumani na Austria hadi leo unatokana kwa kiasi kikubwa na kazi yake.

Kanisi alikuwa gombera na mwalimu wa teolojia katika chuo kikuu cha Ingolstadt, akifanya pia kazi ya kuimarisha imani na kurekebisha maadili ya waamini wa kawaida.

Kwa muda mfupi (1554-1555) aliongoza jimbo la Wien, Austria, ingawa alikataa kuwa askofu ili aweze kuendelea na utume wake huko na huko. Akiwa Wien alifanya uchungaji katika hospitali na magereza hata nje ya mji, akaandaa Katekisimu yake.

Mwaka 1556 alianzisha shule ya bweni huko Praha, leo mji mkuu wa Ucheki.

Mwaka 1557 huko Worms, Ujerumani, alishiriki majadiliano ya kiimani na wataalamu wa Kiprotestanti, akiwemo Filipo Melanchthon.

Mwaka 1558 alikuwa balozi wa Papa nchini Polandi, na mwaka 1560 aliongozana na balozi mwingine, kardinali Stanislaw Hozjusz, kuongea na Kaisari Ferdinandi I.

Mshauri wa Mapapa na watawala, alishiriki mara mbili Bunge la Augsburg (1559 na 1565).

Alishiriki pia vikao vya mwisho vya Mtaguso wa Trento alipochangia masuala mbalimbali (1562).

Aliheshimiwa kwa adabu yake, iliyomfanya akwepe kuita Waprotestanti "wazushi" katika mahubiri yake. Alijua kutofautisha sababu za kukosa imani sahihi, hata aliarifu uongozi wa Kanisa la Roma kuwa wengi katika umati wa Wajerumani walioingia Uprotestanti hawakustahili kulaumiwa.

Alipenda elimudini na kusoma hasa Biblia na vitabu vya mababu wa Kanisa. Alikusanya na kutoa kitaalamu maandishi yote ya Sirili wa Aleksandria na ya Leo Mkuu, mbali ya barua za Jeromu na sala za Nikola wa Flue.

Pia alitoa vitabu vingi vya ibada kwa lugha mbalimbali, akisisitiza kushiriki liturujia lakini pia kufanya sala ya binafsi. Hatimaye aliandika maisha ya watakatifu wa Uswisi na hotuba nyingi.

Vilevile aliandika vitabu vingine ili kufundisha imani na maisha ya Kiroho kulingana wa mahitaji ya walengwa.

Lakini kitabu chake bora ni Katekisimuambayo ilitungwa kama jibu kwa Martin Luther na kutolewa kuanzia mwaka 1555 hadi 1558 kwa jina la *Summa Doctrinae Christianae*, ilirudia kuchapwa mara 200 hivi wakati wa maisha yake tu. Ilitafsiriwa pia katika lugha mbalimbali na kutolewa mara 400 na zaidi. Ilikuwa na matoleo matatu kulingana na kiwango cha elimu cha wasomaji. Ilieleza imani Katoliki kwa ufupi na uwazi, kwa mtindo wa maswali na majibu na kwa kutegemea misamiati ya Biblia, bila kubishana na Waprotestanti.

Mwaka 1580 alianzisha huko Freiburg (Uswisi) chuo cha Mtakatifu Mikaeli, ambapo alielekeza nguvu zake za mwisho kuhubiri na kuandika na ambapo alifariki tarehe 21 Desemba 1597 na hatimaye kuzikwa.

Alitangazwa na Papa Pius IX kuwa mwenye heri mwaka 1864, halafu na Papa Pius XI kuwa mtakatifu na mwalimu wa Kanisa tarehe 21 Mei 1925.

Sikukuu yake inaadhimishwa kila mwaka tarehe ya kifo chake 21 Desemba, lakini Ujerumani tarehe 27 Aprili.

Kwa kawaida anachorwa akiwa na fuvu la kichwa, Yesu msulubiwa na katekisimu.

## Roberto Bellarmino (1542 - 1621)



Roberto Francesco Romolo Bellarmino alikuwa mtawa wa Shirika la Yesu, halafu padri, askofu na kardinali wa Kanisa Katoliki, anayeshika nafasi muhimu katika historia ya karne ya 16 na 17.

Roberto alizaliwa Montepulciano, wilaya ya Siena nchini Italia, tarehe 4 Oktoba 1542, katika familia kubwa, akiwa mtoto wa kiume wa tatu kati ya watano; wazazi wake walikuwa na asili ya kisharifu, lakini hali ya uchumi ilikuwa tofauti. Baba yake, Vincenzo Bellarmino, alikuwa jaji, na mama yake, Cinzia Cervini, alikuwa dada wa Papa Marcello II. Badala ya kujivunia undugu wake na Papa, alidumu kuwa na unyenyekevu na bidii.

Tangu utotoni alikuwa na afya mbovu na mwelekeo mkubwa kwa mambo ya dini kama mama yake. Baada ya kupata malezi nyumbani, alitumwa Padova kwa masomo.

Alipofikia umri wa miaka 18, akifuata wito wake wa upadri, na kuvutiwa na mfano wa Ignasiwa Loyola, aliamua kujiunga na Shirika la Yesu alilolianzisha, na tarehe 21 Septemba 1560 aliweka nadhiri zake za kwanza.

Alisomea Roma tangu mwaka 1560 hadi 1563, halafu alianza kufundisha Firenze na Mondovì, katika shule za shirika lake.

Mwaka 1567 alianza kusoma kwa mpango teolojia huko Padova, lakini kutokana na sifa yake kama mhubiri, mwaka 1569 mkuu wa shirika, Fransisko Borja, alimtuma Louvain (leo katika Ubelgiji), kwenye chuo kikuu maarufu cha mji huo. Ndipo alifahamu kwa karibu Uprotestanti na kuanza kujitokeza hasa katika mabishano na Walutheri na Wakalvini.

Baada ya kupewa upadrisho huko Gand tarehe 25 Machi 1570, alibaki Louvain miaka sita kama mwalimu wa teolojia na mhubiri, akizidi kupata wanafunzi na wasikilizaji kutoka kila upande.

Mwaka 1576 Papa Gregori XIII alimuita Roma afundishe hoja dhidi ya uzushi, kama alivyofanya hadi mwaka 1586, akiandika vitini ambavyo baadaye vikaunda kitabu “Controversiae” (“Mabishano”), ambacho kilisifiwa mara kwa utajiri, uwazi na msingi wa kihistoria katika kutoa msimamo wa Kikatoliki juu ya Ufunuo, Kanisa, sakramenti na neema. Humo alisisitiza muundo wa Kanisa, kama ilivyohitajiwa na hali tete ya imani wakati huo, asisahau roho yake inayohuisha kwa ndani muundo huo. Pia alikwepa kushambulia Waprotestanti, akikazia kutetea mafundisho ya Kanisa kwa hoja za akili na za mapokeo.

Mtaguso wa Trento ulikuwa umemalizika tangu miaka, na Kanisa Katoliki lilikuwa bado na haja ya kujiimarisha kielimu na kiroho. Kazi ya Roberto iliingia moja kwa moja katika juhudi hizo za Urekebisho wa Kikatoliki.

Kuanzia mwaka 1588, akiwa kiongozi wa kiroho wa Wajesuiti wanafunzi wa Collegio Romano, alishirikiana na Papa Sisto V, ingawa huyo hakumpenda sana yeye wala shirika lake. Kati ya vijana aliowalea huko, maarufu zaidi ni Alois Gonzaga, ambaye alifariki mwaka 1591 kutokana na tauni aliyoambukizwa na mtu aliyemuokota barabarani. Baada ya kushughulikia kesi ya kumtangaza mwenye heri, aliomba azikwe karibu naye, kama ilivyotokea baadaye.

Tangu mwaka 1592 hadi 1594 alikuwa gombera wa seminari hiyo, halafu mwaka 1595 akawa mkuu wa shirika katika kanda ya Napoli.

Mwaka 1597 Papa Klementi VIII alimrudisha Roma kama mshauri wake katika masuala ya teolojia n.k.

Miaka ya 1597-1598 alitunga katekisimu kubwa na ndogo, ambazo ziliathiriwa na mazingira ya mabishano kati ya madhehebu ya Kikristo, na kuenea sana hadi mwisho wa karne XIX. Mchango wake huo katika malezi ya vizazi vipya vya Kikatoliki ulimstahilia sifa ya mwalimu wa Kanisa.

Tarehe 3 Machi 1599 Papa alimteua kuwa kardinali akieleza kwamba, "Kanisa la Mungu halina mwingine sawa naye katika elimu". Bellarmino alijaribu kwa kila njia kumfanya Papa abadili uamuzi, lakini mwishoni alilazimika kukubali. Pamoja na hayo, hakuacha maisha yake magumu, na mapato ya cheo hicho aliyaelekeza karibu yote kwa maskini.

Kama kardinali aliongoza idara mbalimbali za Papa na, baada ya kupewa uaskofu tarehe 21 Aprili 1602, akawa askofu mkuu wa jimbo la Capua (1602-1605), alipojitokeza kwa bidii yake ya kuhubiri katika kanisa kuu, kwa kutembelea parokia kila wiki, kwa sinodi 3 za jimbo alizoendesha na kwa kuanzisha mtaguso wa kanda.

Alikuwa anajua kujilinganisha na watu wa kawaida, nao walifurahia usahili wa mtu msomi kiasi hicho.

Baada ya kushiriki uchaguzi wa Papa Leo XI na wa Papa Paulo V, aliitwa tena Roma kushughulikia idara mbalimbali, lakini pia alitumwa kama balozi huko Venezia na Uingereza akatetee haki za Kanisa.

Mzigo wa majukumu na ubovu wa mazingira havikumsahaulisha juhudi kwa ajili ya utakatifu aliodaiwa na hadhi yake kama mtawa na askofu, akimlenga Yesu ili kumjua, kumpenda na kumuiga kwa dhati. Kwake ilikuwa furaha kubwa kujikusanya kwa utulivu na unyofu asali na kumzingatia Mungu.

Miaka ya mwisho alitunga vitabu mbalimbali kuhusu maisha ya Kiroho alipokusanya matunda ya mazoezi yake ya kiroho ya kila mwaka, kama vile “Akili Kupanda kwa Mungu”, “Ufundi wa Kufa Vema” na “Mlio wa Njiwa”. Humo inajitokeza hisia yake kubwa ya wema usio na mipaka wa Mungu, ambaye alijisikia mwanae mpendwa. “Ee roho,mfano wako ni Mungu, uzuri usio na mipaka, mwanga usio na kivuli, uangavu unaopita ule wa mwezi na jua… Yeyote anayempata Mungu, amepata yote, yeyote anayemkosa Mungu amekosa yote”.

Katika kuhimiza kwa nguvu urekebisho wa Kanisa, kuanzia wakleri hadi walei, alielekeza kwanza wongofu wa moyo kadiri ya mafundisho ya Biblia na ya watakatifu.


Alifariki Roma tarehe 17 Septemba 1621.

Alitangazwa na Papa Pius XI kuwa mwenye heri tarehe 13 Mei 1923, mtakatifu tarehe 29 Juni 1930 na mwalimu wa Kanisa tarehe 17 Septemba 1931.

Sikukuu yake inaadhimishwa kila mwaka tarehe 17 Septemba.

Opera Omnia zilizokusudiwa kukusanya maandishi yake yote zilitolewa Cologne (1617), Venezia (1721), Napoli (1856), Paris (1870).

## Laurenti wa Brindisi (1559 - 1619)



Laurenti wa Brindisi ni jina la kitawa la Giulio Cesare Russo, padri na mkuu wa shirika la Ndugu Wadogo Wakapuchini (1602-1605).

Laurenti alizaliwa Brindisi, leo nchini Italia, tarehe 22 Julai 1559.

Baada ya kufiwa baba yake utotoni, alipokuwa na miaka 7 tu mama alimtuma aishi utawani, hivyo alisoma kwenye shule ya Wafransisko Wakonventuali hukohuko Brindisi, akavaa kanzu yao tangu mwaka 1565 hadi 1567 kama maandalizi ya kujiunga nao. Tangu hapo alivutiwa na karama ya Fransisko wa Asizi. Wakati huo ndipo alipoanza kuhubiri, kadiri ya desturi yao.

Kisha kupatwa na hali ngumu kiuchumi katika familia alihamia kwa ndugu yake padri huko Venezia, alipoendelea kusoma na kuzingatia wito wa Kifransisko hadi kujiunga na urekebisho wa Wakapuchini tarehe 18 Februari 1575 kwa kuvaa kanzu yao na kubadilishiwa jina. Wakati huo shirika hilo lilikuwa limekomaa, anavyoonyesha mwenyewe ambaye ni tunda lake kamili zaidi pande nyingi.

Huko Padova aliendelea kusoma mantiki na falsafa, halafu akarudi Venezia kusomea teolojia. Kwa wakati huohuo alikuwa anafundisha pia, kutokana na ujuzi wake mkubwa ajabu, hasa wa Biblia katika lugha zote asili, uliomsaidia hata kuhubiria kwa mafanikio Wayahudi.

Kuhusu umuhimu wa Neno la Mungu alisema, "Neno la Bwana ni mwanga wa akili na moto wa utashi, hivi kwamba binadamu aweze kumjua na kumpenda Mungu. Kwa mtu wa ndani, anayeishi kwa neema hai ya Roho wa Mungu, ni mkate na maji, lakini mkate mtamu kuliko asali na maji yanayopendeza kuliko divai au maziwa… Ni silaha dhidi ya moyo ulioshupaa katika vilema. Ni upanga dhidi ya mwili, ulimwengu na shetani ili kuangamiza kila dhambi".

Tarehe 18 Desemba 1582 alipata upadrisho, akaendelea kutumia utaalamu wake kwa ajili ya Urekebisho wa Kikatoliki baada ya Mtaguso wa Trento. Kwa kuwa alijua lugha mbalimbali, kama vile Kifaransa na Kijerumani, aliweza kufanya utume mpana sana akahubiri katika nchi nyingi za Ulaya.

Kwa ujuzi wake wa Biblia na mababu wa Kanisa aliweza kufafanua kwa utulivu na uwazi mafundisho ya Kikatoliki kwa Waprotestanti hasa wa Ujerumani, akionyesha misingi ya yale yaliyopingwa na Martin Luther, kama vile nafasi ya kwanza ya Mtume Petro na ya askofu wa Roma kati ya wenzao, asili ya uaskofu, utakaso wa dhati wa binadamu na haja ya kutenda mema ili kuokoka milele.

Hata waamini wa kawaida, wasio na elimu kubwa, walifaidika na maneno yake alipowaelekea ili kuwahimiza washike imani yao kimaisha. Ni ajabu alivyofululiza kuhubiri katika miji mingi ya Italia na ya nchi nyingine hata alipotwishwa majukumu mengine mazito, kama vile mwalimu wa teolojia na mlezi wa wanovisi.

Mwaka 1589 alianza kupata vyeo vikubwa shirikani, kama vile mkuu wa kanda na mshauri wa mkuu wa shirika. Pamoja na hayo, alitumwa Ujerumani kuongoza wanashirika wanaokwenda kuishi na kufanya utume huko.

Mnamo Oktoba 1601 aliomba kuwa mmojawapo wa mapadri wa kuhudumia kiroho wanajeshi wa Kikristo wakipambana na Waturuki wavamizi.

Tarehe 24 Mei 1602 alichaguliwa kuwa mkuu wa shirika, mwenye jukumu la kutembelea kanda zake zote. Aliendelea na wadhifa huo hadi mwaka 1605.

Kati ya majukumu mazito ndani ya shirika na ya Kanisa kwa jumla aliendelea kuwa mfuasi mnyenyekevu wa Fransisko wa Asizi, mbali ya kuandika vitabu vingi - vya ufafanuzi wa Biblia, vya maadili, vya hoja za kidini, pamoja na hotuba nyingi, kama zile maarufu juu ya Bikira Maria - vilivyomstahilia jina la "Doctor Apostolicus", yaani Mwalimu wa Kitume.

Katika maandishi yake, alizungumzia mara nyingi liturujia. Mwenyewe anakumbukwa pia kwa ibada yake kwa ekaristi na kwa neema za pekee alizokuwa anazipata wakati wa kuiadhimisha, zilizomfanya achukue masaa kila siku kuadhimisha Misa, ambayo kwake ilikuwa hai. Alikuwa kama akitekwa na huo ukumbusho wa mateso, kifo na ufufuko wa Bwana.

Pamoja na kutumia muda mwingi kusali, kwa ari yake ya pekee alikuwa akihimiza mapadri na waamini wengineo kuyapa kipaumbele maisha ya sala, kwa kuwa ndiyo njia ya kuongea na Mungu. "Lo, kama tungezingatia ukweli huu! Yaani kwamba Mungu yupo kweli na sisi tunaposema naye katika sala; kwamba yeye anasikiliza kweli sala zetu, hata tukisali kwa mioyo na akili yetu tu. Tena si tu kwamba yupo nasi na kutusikiliza, bali yuko radhi na kufurahi sana kutujalia tunachomuomba".

Laurenti alionyesha kazi ya Roho Mtakatifu katika maisha ya waamini, akiwaangaza na kuwaimarisha kwa vipaji vyake waweze kuishi Injili kwa furaha. "Roho Mtakatifu anasaidia ubebaji wa nira ya sheria ya Mungu na kupunguza uzito wake, ili tuweze kushika amri za Mungu kwa urahisi mkubwa na hata kwa furaha".

Vilevile aliangazia nafasi ya pekee ya Bikira Maria, akithibitisha kuwa alitungwa bila dhambi ya asili akashiriki kazi ya ukombozi iliyofanywa na Kristo.

Heshima iliyomfuata kila mahali ilimfanya awe anatafutwa na kusikilizwa kama mshauri.

Sifa yake nyingine ni juhudi kwa ajili ya amani. Mara nyingi Mapapa na watawala wa nchi Katoliki walimchagua kama balozi ili kutatua matatizo na kustawisha uelewano kati ya nchi za Ulaya ambazo wakati huo zilikuwa zinatishwa kuvamiwa na Dola la Waturuki Waosmani.

Mwaka 1618 alitumwa na wananchi wa Napoli walionyanyaswa na makamu wa mfalme wa Hispania akawatetee kwa mfalme mwenyewe, Filipo III. Baada ya kukwepa njama mbalimbali, alitabiri kuwa mwenyewe atakufa mapema, na mfalme atamfuata kabla ya miaka miwili kwisha, kama ilivyotokea.

Alifariki Belém, Ureno, tarehe 22 Julai 1619, labda kwa sumu wakati wa usuluhishi huo.

Alitangazwa mwenye heri na Papa Pius VI mwaka 1783, mtakatifu na Papa Leo XIII mwaka 1881, hatimaye mwalimu wa Kanisa na Papa Yohane XXIII mwaka 1959.

Sikukuu yake inaadhimishwa kila mwaka tarehe 22 Julai.

## Fransisko wa Sales (1567 - 1622)



Fransisko wa Sales alikuwa askofu wa Geneva (Uswisi). Akijumlisha ndani mwake matunda bora ya karne XVI, ni kati ya watu muhimu zaidi katika Urekebisho wa Kikatoliki na katika teolojia ya maisha ya kiroho.

Fransisko, mtoto wa kwanza wa mtawala wa Boisy, sharifu wa Savoy, alizaliwa Thorens-Glières, leo nchini Ufaransa, tarehe 21 Agosti 1567.

Alipata mapema elimu bora ambayo aliikamilisha akisoma sheria za Kanisa na za serikali.

Baba yake, akimtaka awe mwanasheria, ndiye aliyemtuma kwenye chuo kikuu cha Padova (Italia), ambako Fransisko alipata digrii, lakini pia wito wa upadri.

Baada ya kurudi kwao, aliteuliwa kuwa wakili wa Seneti ya Chambéry.

Katika ujana wake safi, tafakuri juu ya mafundisho ya Augustino wa Hippo na ya Thoma wa Akwino zilimfanya afadhaikie wokovu wake kuhusiana na suala la uteule lililojadiliwa sana wakati huo. Alisali kwa bidii, lakini wasiwasi kuhusu hali yake mbele ya Mungu ulimfanya ashindwe kwa wiki kadhaa hata kula na kulala, isipokuwa kwa shida.

Katika kilele cha jaribu hilo, aliingia katika kanisa la Wadominiko la Paris akasali moyo wazi: "Ee Bwana, unayeshika yote mkononi mwako na ambaye njia zako ni haki na ukweli, lolote litakalotokea, lolote ulilonipangia… nitakupenda ee Bwana, uliye daima hakimu mwenye haki na Baba mwenye huruma… Nitakupenda hapa, Mungu wangu, nami nitatumainia daima huruma yako na nitarudia daima sifa zako… Ee Bwana Yesu, utakuwa daima tumaini langu na wokovu wangu katika nchi ya walio hai".

Hivyo akiwa na umri wa miaka 20 alipata amani moyoni kwa kujiachia katika upendo wa Mungu, bila kudai chochote zaidi wala kumuuliza atamfanyia nini: ndiyo siri ya maisha yake yote.

Kisha kushinda upinzani wa baba yake, alisoma teolojia huko Paris, akapewa upadrisho tarehe 18 Desemba 1593, akatumwa kwenye eneo la Chablais, lililotawaliwa na madhehebu ya Yohane Calvin.

Huko alijitosa hasa kuhubiri, akitumia mbinu ya majadiliano. Alipoona itikio hafifu, alitambua umuhimu wa uchapaji akabuni uandishi wa "matangazo" yaliyomwezesha kuwafikia hata watu wa mbali. Alikuwa anayabandika kutani na kuyasambaza nyumbani kwa watu kupitia chini ya milango. Hata hivyo matunda hayakuwa mengi.

Akiwa na nia ya kuzuia uenezi wa Uprotestanti kati ya Wakatoliki, na kurudisha wengi iwezekanavyo katika ushirika wa Kanisa, aliongea na askofu wa Geneva ili kumuomba amtume akahubiri katika mji huo, makao makuu ya Wakalvini.

Kisha kufika alijadiliana na Waprotestanti ili kuwarudisha kwenye umoja kamili na Kanisa la Roma.

Wazo lake lilielekea daima walei, ili kuwapa mafundisho na miongozo ya maisha ya Kikristo.

Juhudi zake na mafanikio aliyopata kwa ubora wa mahubiri yake vilifanya ateuliwe kuwa askofu mwandamizi wa Geneva mwaka 1599, akiwa na umri wa miaka 32 tu.

Baada ya miaka mitatu akawa askofu wa jimbo hilo ambapo alijitahidi kutekeleza maagizo ya Mtaguso wa Trento.

Lakini mji kwa jumla ulibaki mikononi mwa Wakalvini, hivyo ilimpasa aishi Annecy, katika utawala wa Savoy.

Kama mchungaji wa jimbo fukara lenye matatizo katika mazingira ya milimamilima, aliandika: “Nimemkuta Mungu mtamu na mpole katika milima yetu mirefu mizuri, ambapo watu wengi sahili wanampenda na kumuabudu kwa ukweli na unyofu”. Hata hivyo athari ya maisha na mafundisho yake ilienea sana wakati huo na baadaye kutokana na utimilifu na utamu wake.

“Kama ni kukosea, napenda kukosea kwa kuzidisha wema kuliko ukali”: kauli yake hiyo inaeleza alivyoweza kujivutia watu wengi. Kuliko hoja za kupinga uzushi, ni ufafanuzi wake wa upendo wa Mungu uliowafanya Wakalvini wengi wajiunge na Kanisa Katoliki na hatimaye kurudisha Chablais nzima. Walisema juu yake, “Jinsi gani Mungu ni mwema, ikiwa Fransisko ni mwema hivyo!”

Katika nafasi mbalimbali alitumiwa pia kama balozi na mpatanishi wa jamii.

Mstaarabu na mwenye elimu kubwa, alipata umaarufu hasa kwa kuongoza kiroho watu wengi (zimetubakia barua zake 2000 hivi!); kati yao watakatifu Vinsenti wa Paulo na Yoana Fransiska wa Chantal, aliyemsaidia kuanzisha Shirika la Maonano. Katika mpango wake, uliozuiwa kwa kuwa nyakati hazikuwa tayari, masista hao hawakutakiwa kubanwa na ugo bali kutembelea na kusaidia mafukara na wagonjwa. Aliwaelekeza waishi kweli kwa Mungu tu katika usahili na unyenyekevu, wakitenda vizuri kabisa mambo ya kawaida: “Nataka mabinti wangu wasiwe na kipeo kingine isipokuwa kumtukuza Bwana kwa unyenyekevu wao”.

Huko Thonon, ili kueneza utakatifu kati ya Wakristo wote, alianzisha pia tawi la Oratorio ya mtakatifu Filipo Neri na “chuo kikuu” cha kazi.

Kati ya vitabu alivyotunga, muhimu zaidi ni "Kuingia Maisha ya Juhudi" na "Kitabu cha Upendo wa Mungu", ambavyo ni kati ya vitabu bora vya kidini vya nyakati zote na vinaelekeza walei pia kufuata njia ya utakatifu, yaani ya upendo wa Mungu, ambaye alimtambulisha kama “Mungu wa moyo wa binadamu”.

Katika kitabu “Kuingia Maisha ya Juhudi” Fransisko alitoa wito ulioonekana wa kimapinduzi kwa wakati ule: kila mtu kuwa kabisa mali ya Mungu huku akiishi ulimwenguni na kutimiza kitakatifu majukumu maalumu ya hali yake. “Nia yangu ni kufundisha wanaoishi mijini, katika ndoa na ikuluni” kwa sababu moyo wa ibada unatakiwa kung’aa kila mahali: juu ya viti vya enzi vya wafalme, katika mahema ya majemadari, katika mahakama na ofisi za ushuru, viwandani na machungani.

Kipeo cha binadamu mwenye umoja wa dhati kilionyeshwa katika ulinganifu wa sala na utendaji ulimwenguni, katika kulenga ukamilifu bila kuacha maisha ya kawaida, kwa msaada wa neema ya Mungu ambayo inampenya mtu bila kuangamiza umbile lake, bali kwa kulitakasa na kuliinua hadi vilele vya Kimungu.

Miaka baadaye, “Kitabu cha Upendo wa Mungu” kilimpa Mkristo aliyekomaa Kiroho fundisho kamili zaidi, kikianzia mtazamo sahihi kuhusu binadamu: akili yake, yaani roho kadiri inavyoweza kufikiri, inaonekana humo kama jengo zuri kabisa, kama hekalu lenye nyua mbalimbali kandokando ya kiini ambacho ni “kilele cha roho yetu” na ambamo akili, kisha kupanda ngazi zote, “inafumba macho yake” na ujuzi unakuwa mamoja na upendo.

Mtazamo huo mpana hauna mpasuko: “Binadamu ndiye ukamilifu wa ulimwengu; roho ndiyo ukamilifu wa binadamu; mapendo ndiyo ukamilifu wa roho, na upendo ndio ukamilifu wa mapendo”. Hivyo safari ya kumuendea Mungu inaanza kwa kutambua “elekeo la kimaumbile” lililomo moyoni mwa mtu - hata kama ni mkosefu - la kumpenda Mungu kuliko yote.

Akifuata Biblia, Fransisko anazungumzia muungano wa Mungu na mtu kwa mifano mbalimbali ya mahusiano: Baba, Bwana, mume na rafiki, ambaye ana sifa za mama na nesi mwenye hisani na ni jua linalotambulishwa na usiku pia.

Mungu huyo anamvuta binadamu kwake kwa vifungo vya upendo, si kwa shuruti: "Upendo hauna wafungwa wala watumwa, bali unaleta yote chini yake kwa nguvu ya kupendeza hivi, hata hakuna chenye nguvu kuliko upendo, lakini pia hakuna kitamu kuliko nguvu yake".

Kwa sababu hiyo alimuandikia Yoana Fransiska wa Chantal: "Hii ndiyo kanuni ya utiifu wetu, ninayokuandikia kwa herufi kubwa: FANYA YOTE KWA UPENDO, HATA MOJA KWA SHURUTI; UPENDE UTIIFU KULIKO KUOGOPA UKAIDI. Nakuachia roho ya uhuru, si ile inayokataa utiifu, ambayo ndiyo uhuru wa kidunia, bali uhuru ule unaokataa matumizi ya nguvu, mahangaiko na mafadhaiko".

Ni roho hiyo iliyoathiri malezi na maisha ya Kiroho ya wengi katika karne zilizofuata: bila hiyo tusingepata "malezi kinga" ya Yohane Bosco wala "njia ndogo" ya Teresa wa Mtoto Yesu. Kwa ajili hiyo anahesabiwa kama baba wa maisha ya kiroho ya nyakati zetu, yaliyofuatwa na watakatifu wengi, hasa Yohane Bosco, mwanzilishi wa shirika alililoliita la Wasalesiani kwa heshima yake.

Alifariki Lyon, Ufaransa, tarehe 28 Desemba 1622.

Alitangazwa na Papa Aleksanda VII kuwa mwenye heri tarehe 8 Januari 1662, na mtakatifu tarehe 19 Aprili 1665. Halafu Papa Leo XIII mwaka 1887 alimtangaza kuwa mwalimu wa Kanisa.


Ni msimamizi wa waandishi wa habari, watunzi na wanafasihi, magazeti ya Kikatoliki na mabubu-viziwi.

Sikukuu yake inaadhimishwa kila mwaka tarehe 24 Januari.

**Kwa Kiswahili**

MT. FRANSISKO WA SALES, Mwanzo wa Maisha ya Kumcha Mungu – tafsiri ya Fr. Severin L. Njako na Cornelius D. Nsalanga – ed. Vincentians – Mbinga 1996 – ISBN 9976-67-091-5

# Alfonso Maria (1696 - 1787)



Alfonso Maria wa Liguori -, pamoja na kuwa padri na mtawa mwanzilishi wa shirika la Mkombozi Mtakatifu Sana, halafu askofu wa Kanisa Katoliki, anajulikana kama mwanateolojia wa maadili, mwalimu wa maisha ya Kiroho kwa wote, hasa watu wa chini, mwandishi wa vitabu vingi sana, mwanashairi, mchoraji na mwanamuziki.

Alikuwa kielelezo cha mchungaji mwenye ari na wema katika kutangaza Neno la Mungu na kuadhimisha sakramenti ili kuokoa watu, akitia maanani hisia na miguso, si hoja za akili tu, ili kuwaelekeza wawapende Mungu na majirani.

Alfonso alizaliwa Marianella, leo katika jiji la Napoli, nchini Italia, tarehe 27 Septemba 1696, akiwa mtoto wa kwanza kati ya wanane wa sharifu tajiri Giuseppe de' Liguori na Anna Maria Caterina Cavalieri.

Baba yake alimpatia mapema walimu bora, hivi kwamba alipofikia umri wa miaka 12 aliweza kujiandikisha kwenye chuo kikuu cha Napoli ambapo miaka 4 baadaye akapata udaktari wa sheria za nchi na za Kanisa

(1713). Kwa ruhusa ya pekee aliweza kuanza kazi kama wakili akiwa na miaka 16 tu. Akiwa na sifa kubwa kuliko mawakili wengine wote wa mahakama ya Napoli, kwa miaka 8 mfululizo alishinda kesi zote.

Mwaka 1718 alifanywa hakimu wa "Regio Portulano" ya Napoli, na miaka michache baadaye akawa balozi wa kardinali Altan, naibu wa mfalme.

Pamoja na hayo alimtamani Mungu na ukamilifu hata akaja kuacha kazi yake, ikiwa ni pamoja na umaarufu na utajiri.

Kushindwa kesi muhimu, kuchukia uovu uliozidi kuenea mahakamani, kuhudhuria Chama cha Madaktari kwenye Oratorio wa Wafiliponeri pamoja na kutembelea na kuhudumia wagonjwa wa hospitali kuu ya Napoli, iliyoitwa ‵degli Incurabili′ (yaani 'ya Wasioponyeka'), ndiyo chanzo cha wito wa upadri, aliouitikia kwa kujiunga na seminari mwaka 1723, bila kujali upinzani wa baba aliyemtaka aoe.

Huko pia alipata walimu bora waliomuingiza katika ujuzi wa Biblia, historia ya Kanisa na maisha ya Kiroho, akajipatia elimu pana ya teolojia aliyoitumia baadaye katika uandishi.

Alipewa upadrisho tarehe 17 Desemba 1726, akiwa na umri wa miaka 30, akaendelea kuishi nyumbani kwa mzazi, lakini kwa kutekeleza huduma zake mpya alijiunga na chama cha kijimbo cha Misheni za Kitume.

Mbali ya mahubiri makanisani, alianzisha mikutano ya jioni kwa ajili ya watu duni zaidi ili kuwaeleza Injili kwa unyofu mkubwa. Wengi wao walikuwa wametekwa na vilema mbalimbali, kama vile ujambazi, lakini yeye kwa wema wa ajabu aliwafundisha kusali na kuongoka akipata mafanikio makubwa. Katika mitaa mibovu zaidi ya Napoli yalizidi kuongezeka makundi ya watu waliokutana jioni katika nyumba za binafsi na maduka ili kusali na kutafakari Neno la Mungu chini ya makatekista wengi aliowaandaa pamoja na mapadri wengine ili wayatembelee mara kwa mara asiache kuwasimamia na kuwasaidia kiroho mwenyewe.

Baada ya kushinda upinzani wa wengi, mikutano hiyo iliidhinishwa na kardinali Fransisko Pignatelli ikaanza kufanyika katika vikanisa vingi vya mji huo. Ilikuwa nafasi ya kufaa kwa malezi ya kimaadili, kwa maendeleo ya kijamii na kwa mshikamano kati ya mafukara: wizi, mapigano na ukahaba karibu vilitoweka.

Mwaka 1730, ili apone vizuri baada ya kuugua ugonjwa wa mapafu, alifuata agizo la waganga la kwenda kwenye vilima vya Scala na Ravello, alipoanza kuwahubiria wakulima na wachungaji fukara. Akiguswa na ujinga wao upande wa dini, pamoja na ugumu wa maisha yao kwa jumla, aliamua kuacha mji mkuu na kujitosa kwa ajili ya watu hao, ingawa awali alikuwa amefikiria kwenda kuinjilisha mataifa ya Kipagani.

Kutokana na tetemeko la ardhi ambalo mwaka 1731 liliupata mji wa Foggia na kutaka kusababisha waamini waasi, alikwenda huko. Umati uliokusanyika mbele ya kanisa kuu ulishuhudia kwamba alionekana kuelea hewani (tarehe 30 Novemba 1735).

Mwaka 1732, akiwa na miaka 36, alihama Napoli akaanzisha shirika la Mkombozi Mtakatifu Sana (Waredentori) huko Villa degli Schiavi (leo Villa dei Liberi katika wilaya ya Caserta) akiliweka chini ya usimamizi wa askofu Tomaso Falcoia. Shirika hilo, ambalo baadaye akawa mkuu wake, lilikuwa na lengo la kuinjilisha maskini walioishi mashambani, na likaja kukubaliwa na Papa Benedikto XIV mwaka 1749.

Chini yake, watawa hao waliinjilisha huko na huko, wakifikia hata vijiji vya porini, wakihimiza watu kuongoka na kuishi Kikristo hasa kwa njia ya sala.

Maisha ya shirika yalikabiliwa na majaribu na upinzani mkali, lakini mwanzilishi aliweza kulidumisha kwa uvumilivu usiokata tamaa na kwa kutumia ujuzi wake wa sheria. Hivyo Waredentori walieneza Neno la Mungu kwa unyofu hadi Polandi.

Miaka iliyofuata Alfonso aliandika vitabu vingi vya maisha ya kiroho, teolojia ya dogma, maadili na utetezi wa imani. Lakini pia alitunga nyimbo nyingi kwa lugha rasmi ya Kiitalia na kwa lahaja ya Kinapoli, kama ule maarufu zaidi, "Tu scendi dalle stelle" kwa ajili ya Noeli.

Mwaka 1762 Papa Klemens XIII, akizingatia wema na ari yake katika uchungaji, alimfanya akubali kuwa askofu wa jimbo la Sant'Agata de' Goti.

Wakati wa njaa ya kutisha iliyoupata Ufalme wa Napoli mwezi Januari 1764, Alfonso aliweza kuzuia mateso ya watu wake kwa kiasi kikubwa, akihimiza mikopo na kupambana na ulanguzi pamoja na kuchochea uchumi uliokwama tangu miaka 2.

Mwaka 1774 alionekana mahali pawili kwa wakati mmoja, yaani huko Roma katika kumhudumia na kumzika Papa Klemens XIV na huko Sant'Agata de' Goti akiwa ameganda siku mbili kwenye kochi.

Mwaka 1775, baada ya kufanya kazi kubwa (alikuwa ameweka nadhiri ya kutopoteza muda kamwe) na kupata lawama nyingi, pamoja na kudhoofika kiafya, aliacha uongozi wa jimbo kwa sababu za afya akahamia kwenye nyumba ya shirika huko Nocera de' Pagani (leo sehemu hiyo ni katika kijiji cha Pagani, wilaya ya Salerno), alipobaki akiendelea kuandika hadi kufariki kwake tarehe 1 Agosti 1787.

Alitangazwa mapema na Papa Pius VII kuwa mwenye heri tarehe 15 Septemba 1816, halafu Papa Gregori XVI alimtangaza mtakatifu tarehe 26 Mei 1839, na Papa Pius IX kuwa mwalimu wa Kanisa mwaka 1871. Yeye tu alipewa cheo hicho kabla ya miaka mia tangu afe.

Sifa hiyo ilimfaa kwa sababu nyingi, hasa utajiri wa mafundisho yake kuhusu maadilidini yaliyotoa sawasawa msimamo wa Kikatoliki, hivi kwamba Papa Pius XII alimtangaza pia "msimamizi wa waungamishi na wa wanateolojia ya maadili".

Sikukuu yake inaadhimishwa kila mwaka tarehe 1 Agosti.

Inakadiriwa kuwa vitabu vyake vimetafsiriwa katika lugha 72, na kuwa vimetolewa mara 21,500, kuliko vile vya Wakatoliki wengine wote. Kati yake, maarufu zaidi ni "Utekelezaji wa Kumpenda Yesu Kristo", "Kauli za Milele", "Njia Kuu ya Sala" na "Utukufu wa Maria". Mtindo wake sahili na wa kupendeza, uliolenga hasa watu wa kawaida kabisa, ulichangia kumfanya aathiri maisha ya Kikristo ya umati katika karne zilizofuata.

Hasa katika kitabu chake muhimu zaidi, "Teolojia ya Maadili", Alfonso alipendekeza uwiano mzuri kati ya madai ya sheria ya Mungu - ambayo imeandikwa mioyoni mwetu, imefunuliwa kikamilifu na Kristo na kufafanuliwa rasmi na Kanisa - na nafasi ya dhamiri na hiari ya binadamu - ambaye anakomaa kwa kuambatana na ukweli na wema.

Dhidi ya ukali wa misimamo ya matapo ya wakati ule ndani ya Kanisa, hasa Ujanseni, uliokatisha tamaa tu, kwa kumchora Mungu wa kutisha, tofauti sana na habari njema aliyotangaza Yesu, alihimiza wote kutegemea bila kipimo huruma ya Mungu inayotuokoa.

Kwa msingi huo aliwaelekeza kwenye utakatifu kama lengo la maisha haya: "Mungu anataka wote wawe watakatifu, kila mmoja katika hali yake: mtawa kama mtawa, mlei kama mlei, padri kama padri, mtu wa ndoa kama mtu wa ndoa, mfanyabiashara kama mfanyabiashara, askari kama askari, na vilevile kwa hali yoyote ya maisha".

Pia alihimiza wachungaji na waungamishi kufuata kiaminifu mafundisho ya Kanisa kuhusu maadili pamoja na kuwa na upendo mpole ili waelewe watu na kuwafanya wajisikie wanasindikizwa, wanategemezwa na kutiwa moyo katika safari ya Kiroho.

Hakuchoka kukariri kwamba mapadri ni ishara wazi ya huruma isiyo na mipaka ya Mungu, ambaye anasamehe na kuangaza akili na mioyo ya wakosefu ili waongoke.

Alisisitiza nguvu ya sala kwa binadamu: ndiyo chombo kikuu cha wokovu, kwa sababu inatuweka wazi kwa Mungu na kwa neema yake ili tutimize kila siku matakwa yake na kufikia utakatifu. Kwa ajili hiyo aliandika: "Mungu hamnyimi mtu yeyote neema ya kusali, ambayo inamsaidia kushinda aina zote za tamaa na vishawishi. Nami nasema, tena nitaendelea kusema maisha yangu yote, kwamba wokovu wetu unategemea tu sala". Kifupi alitamka: "Anayesali ataokoka, asiyesali atapotea".

Alfonso alifundisha sana maadili na matendo ya ibada, akihimiza hasa kutembelea na kuabudu Ekaristi: "Hakika, kati ya ibada zote, baada tu ya ile ya kupokea sakramenti, kumuabudu Yesu katika Sakramenti Kuu ndiyo ile inayoshika nafasi ya kwanza, inayompendeza Mungu na kutufaa sisi zaidi… Lo, jinsi inavyopendeza kuwa na imani mbele ya altare… ili kumtolea mahitaji yetu kama anavyofanya rafiki kwa rafiki yake anayemtegemea kabisa".

Maisha ya Kiroho aliyoyafundisha kiini chake ni Kristo na Injili yake. Mara nyingi tafakuri juu ya mafumbo ya Umwilisho na Mateso ya Mwana wa Mungu zilikuwa mada za mahubiri yake, kwa sababu katika matukio hayo binadamu wote wanapewa ukombozi kwa wingi.

Kwa kuwa ibada yake ilimuelekea kwanza Kristo, ilienea pia katika kumheshimu Bikira Maria, aliye tunda bora la ukombozi na mshiriki wa kazi ya Mwanae. Alieleza kwamba heshima kwa Mama Maria ni faraja kubwa wakati wa kufa.

Kuhusu nafasi hiyo ya mwisho ya maisha duniani, alisisitiza kutafakari uzima wa milele tulioitiwa ili kushiriki moja kwa moja heri ya Mungu, na vilevile uwezekano wa kutisha wa kupotea milele: kwa kufikiria hayo tunaweza kuishi kwa utulivu na uwajibikaji mkubwa zaidi na hatimaye kukabili kifo kwa kutegemea wema wa Mungu.

**Kwa Kiswahili**

MT. ALFONSI MARIA WA LIGUORI, Kutimiza Mapenzi ya Mungu – tafsiri ya J. A. Sipendi – ed. Tanganyika Mission Press – Tabora

## Teresa wa Mtoto Yesu (1873 - 1897)



Teresa wa Mtoto Yesu na wa Uso Mtakatifu ni jina la kitawa la Thérèse Françoise Marie Martin, maarufu pia kama Teresa wa Lisieux, anayeheshimiwa na Kanisa Katoliki kama mtakatifu mwenye sifa za bikira na mwalimu wa Kanisa.

Akifurahia udogo wake, Teresa alijitokeza kama "mtaalamu wa elimu ya upendo" (Papa Yohane Paulo II) katika maandishi yake, hasa katika shajara alimosimulia kwa unyofu wa hali ya juu jinsi kwa neema alivyoelewa na kutekeleza Injili katika maisha yake yaliyofichika ndani ya monasteri ya Wakarmeli Peku.

Teresa, mtoto wa tisa na wa mwisho wa Louis Martin na Marie-Azélie Guérin (Zélie), ambao wanaheshimiwa kama wenye heri tangu tarehe 19 Oktoba 2008, alizaliwa tarehe 2 Januari 1873 huko Alençon, mkoa wa Normandie (Ufaransa).

Walipokuwa vijana wazazi wake walitaka kuingia utawani, wasiweze. Baada ya kuoana, maisha yao yote yaliongozwa na imani na maadili ya Ukristo.

Teresa alipozaliwa, watoto 4 walikuwa wameshafariki, naye aliyumba sana kinafsi alipofiwa mama yake alipokuwa na umri wa miaka 4 tu. Hapo mjomba wake, Isidore Guerin, aliteuliwa kuwa mlezi msaidizi wa mabinti watano walioachwa na marehemu ambao wote wakawa masista baadaye. Hivyo, tarehe 15 Novemba 1877, Louis Martin alihamia Buissonnets, kitongoji cha Lisieux, awe jirani na shemeji yake mwenye famasia.

Huko Teresa alijenga uhusiano mkubwa na binamu yake Maria. Lakini uhusiano wa pekee hasa alikuwa nao kwa dada zake Paulina na Maria, akiwaona kama mama zake.

Teresa alisimulia alivyoponywa ugonjwa wa nafsi yake kwa kutokewa na Bikira Maria akimtabasamu. Baadaye alipokea komunyo ya kwanza na katika kuungana hivyo na Yesu alimfanya kiini cha maisha yake.

Mwaka 1882, Paulina alipoingia monasteri ya Wakarmeli ya Lisieux, Teresa angetaka kumfuata, lakini hakuweza kutokana na umri wake mdogo. Zaidi tena alitaka kufanya hivyo Maria pia alipoingia monasteri hiyohiyo mwaka 1886.

Usiku wa Noeli iliyofuata, alishinda moja kwa moja huzuni yake iliyomfanya alielie daima. Alielewa anahitaji kumtafuta Mungu kwa ukomavu zaidi na kujipatia hivyo "elimu ya upendo" ambayo inajumlisha kweli zote za imani. Mwenyewe aliita neema hiyo "wongofu kamili", na tangu hapo alianza "kupiga mbio kama jitu".

Alipofikia umri wa miaka 14 Teresa alizidi kushikamana kwa imani na Yesu msulubiwa, akajitosa kwa "moyo wa kimama" kumuombea muuaji aliyeonekana kukabili adhabu ya kifo bila kutubu. "Nilitaka kwa gharama yoyote

kumzuia asiende motoni milele… Nilikuwa na tumaini kubwa kabisa katika Huruma ya Yesu isiyo na mipaka". Ndiyo mang'amuzi yake ya kwanza ya umama wa kiroho.

Teresa alianza kupigania wito wake dhidi ya upinzani wa watu mbalimbali waliotaka kuahirisha hatua ya kujiunga na utawa. Kwa ajili hiyo mnamo Novemba 1887 alisafiri hadi Roma akaombe ruhusa ya Papa Leo XIII, lakini alikataliwa kwa wema. Kitu hicho kilimsikitisha lakini bila kumhangaisha, kwa sababu alijua amefanya kila aliloweza ili kuitikia wito wake mapema.

Wakati wa kurudi Ufaransa, askofu wake alibadili msimamo na kumruhusu. Hivyo tarehe 9 Aprili 1888 msichana Teresa alingiia Karmeli "ili kuokoa roho za watu na kuombea mapadri", akiwa na miaka 15 tu. Ile tisa iliyofuata ikawa na maendeleo ya kiroho ya kasi ajabu.

Wakati huohuo baba yake alianza kusumbuliwa na ugonjwa wa akili uliomtia tabu na aibu sana. Huo ukawa sababu ya uchungu mwingi hata kwa binti yake mpendwa, ambaye lakini kwa njia hiyo alijaliwa kutazama uso wa Yesu katika mateso yake.

Aliweka nadhiri zake za kwanza tarehe 8 Septemba 1890, ikawa arusi ya kiroho katika udogo: "Ilikuwa siku ya Maria Kuzaliwa. Lo, sikukuu nzuri kweli kwa kuolewa na Yesu! Bikira mtakatifu katika udogo wake kama mtoto mchanga ndiye aliyemtoa aliye Ua lake dogo kwa Yesu mdogo".

Kwa Teresa, kuwa mtawa maana yake ilikuwa kuwa bibiarusi wa Yesu na mama wa roho za watu. Ndiyo maana siku hiyo aliandika sala iliyotokeza dira yote ya maisha yake, akimuomba Yesu, kama zawadi ya Upendo wake usio na mipaka, aweze kuwa mdogo kuliko wote, lakini hasa aliomba wokovu wa watu wote: "Leo kusiwe na roho yoyote ambayo ipotee milele".

Mwaka 1893 aliteuliwa kuwa mlezi msaidizi wa wanovisi, kazi aliyoifanya kwa bidii na ufanisi mkubwa. Baadaye kwa maandishi yake yaliyoenea upesi duniani kote akawa mlezi wa umati wa watu akiwaelekeza kufuata Heri 8 alizotangaza Yesu mlimani.

Mwaka 1894, baada ya ugonjwa wa muda mrefu, mzee Louis Martin alifariki, na binti yake mwingine, Selina, aliyekuwa anamtunza, aliweza kujiunga na monasteri hiyo. Kamera yake imetuachia picha halisi za Teresa.

Muhimu sana ni "Majitoleo kwa Upendo wenye Huruma" ambayo aliyafanya katika sikukuu ya Utatu Mtakatifu ya mwaka 1895 na yalifungua kipindi cha mwisho cha maisha yake mafupi kilichojaa mateso katika muungano na yale ya Yesu.

Mwezi Aprili 1896, alipatwa na TB, ugonjwa uliokuja kumuua baada ya miezi 18. Mateso ya mwili yaliendana na yale ya ndani yanayojulikana kama "usiku wa roho" na ni jaribu kali la imani. Pamoja na Bikira Maria chini ya msalaba wa Mwanae, Teresa alifaulu kulishinda katika giza nene lilioenea ndani mwake. Alitambua kwamba alipaswa kupatwa na jaribu hilo kwa ajili ya wokovu wa wakana Mungu wote wa ulimwengu wa kisasa, ambao aliwaita "ndugu".

Alizidi vilevile kutekeleza upendo wa kidugu: kwa masista wa jumuia yake, kwa wamisionari wawili aliokabidhiwa awaombee, kwa mapadri na kwa watu wote, hasa wale wa mbali zaidi, akawa kweli dada wa wote. Upendo wake wa kuvutia ulitokeza furaha ya dhati ambayo mwenyewe alifichua siri yake: "Ee Yesu, furaha yangu ni kukupenda wewe".

Katika hali hiyo ya mateso, akitekeleza upendo wa hali ya juu katika mambo madogo ya maisha ya kila siku, Teresa alitimiza wito wake wa kuwa upendo katika moyo wa mama Kanisa.

Katika barua yake ya mwisho, aliandika hivi juu ya picha ya Mtoto Yesu iliyochorwa ndani ya Hostie takatifu: "Siwezi kumuogopa Mungu aliyejifanya mdogo hivi kwa ajili yangu! … Mimi nampenda! Kwa kuwa yeye ni Upendo na Huruma tu!"

"Mimi amenipa Huruma yake isiyo na mipaka, na ni katika kioo hicho kisichosemeka kwamba nazingatia sifa zake nyingine za Kimungu. Hizo zote zinaonekana kwangu zinang'aa kwa upendo. Hata Haki yake, labda kuliko sifa nyingine, inaonekana kwangu imevikwa Upendo".

Ndani mwake yalitimia maneno aliyoyandika: "Watakatifu wote walielewa, na kwa namna ya pekee labda wale waliojaza ulimwengu kwa mwanga wa mafundisho ya Injili. Haikuwa katika sala kwamba Mt. Paulo, Mt. Augustino, Mt. Yohane wa Msalaba, Mt. Thoma wa Akwino, Fransisko, Dominiko na marafiki wa Mungu wengine wengi hivi walichota elimu ile ya ajabu ambayo iliteka akili bora?"

"Mimi nahitaji kufungua tu Injili takatifu ili ninuse mara manukato ya maisha ya Yesu, na hapo nijue njia ambayo nipige mbio juu yake; nami nakimbilia nafasi ya mwisho, si ile ya kwanza… Nahisi kwamba hata kama

dhamiri yangu ingelemewa na makosa yote ya jinai yanayoweza kufanyika… kwa moyo uliovunjika kwa uchungu ningejitupa mikononi mwa Yesu Mwokozi wangu, kwa sababu najua anampenda mwana mpotevu”.

Tarehe 10 Julai 1897 udhaifu wa mwili ulimzuia asiendelee kuandika habari za maisha yake kama alivyoagizwa. Neno la mwisho aliloliandika katika sentensi isiyomalizika ni "upendo".

Alifariki tarehe 30 Septemba 1897, mnamo saa 19:20, huku akitazama sanamu ya Msulubiwa aliyoishika mikononi na kusema, “Mungu wangu, nakupenda!”. Maneno hayo yalikuwa muhtasari wa maisha yake.

“Yesu, nakupenda” ndiyo yanayotawala maandishi yake yote. Kwa njia hiyo alizama katika Utatu Mtakatifu. Katika mashairi yake aliandika, “Lo, unajua, Yesu Mungu, kuwa nakupenda / Roho wa Upendo ananiwasha kwa moto wake / Ni kwa kukupenda kwamba nampendeza Baba”.

Mara baada ya kufa, maandishi yake yalianza kusambaa kwa namna ya ajabu na kumvutia heshima ya wengi. Pia ilitokea miujiza kwa maombezi yake. Ni kama alivyosema, kuwa atamimina mvua ya mawaridi kutoka mbinguni, akitumia uzima wa milele kutenda mema mengi duniani.

Papa Pius XI alimtangaza mwenye heri tarehe 29 Aprili 1923, tena mtakatifu tarehe 17 Mei 1925, na Papa Yohane Paulo II alimtangaza mwalimu wa Kanisa tarehe 19 Oktoba 1997 kutokana na mchango wake mkubwa katika teolojia ya Kiroho.

Tangu mwaka 1927 ni msimamizi wa wamisionari wote (pamoja na Fransisko Saveri), na tangu mwaka 1944 wa Ufaransa (pamoja na Yoana wa Arc).

Sikukuu yake inaadhimishwa kila mwaka tarehe 1 Oktoba.

“Njia ndogo ya tumaini na upendo”, njia ya “utoto wa kiroho”aliyoielekeza inafundisha kutimiza sharti la Yesu: “Msipoongoka na kuwa kama vitoto, hamtaingia katika ufalme wa mbinguni” (Mt 18:3). Njia hiyo inatia moyo wa kujitoa kikamilifu kama kikafara kwa wokovu wa ulimwengu. Mwenyewe aliifuata hata akasema: “Kupenda ni kutoa yote, na kujitoa pia”. “Sijawahi kumnyima chochote Mungu mwema!”

Siri yake ni nguvu ya upendo, ambao Teresa alitambua ndio wito wake katika Kanisa: kuwa moyo wa Mwili wa Kristo ili kusaidia viungo vyake vyote kufanya kazi vizuri.

**Kwa Kiswahili**

THERESIA WA MTOTO YESU, Ua la Upendo, Maisha ya Mtakatifu Theresia wa Mtoto Yesu Aliyoyaandika Yeye Mwenyewe – tafsiri ya J. J. Rwechungura – ed. Paulines Publications Africa – Nairobi 1992 – ISBN 9966-21-021-0

**Kwa Kihaya**

THEREZA OW’OMWANA YEZU – Akamuli k’engonzi, Oburora bw’Omutakatifu Thereza Ow’omwana Yezu Obwo Yayehandikire Wenene – tafsiri ya J. J. Rwechungura – ed. Marianum Press Kisubi – Kisubi 1960